# Nipashe

Jumatano Julai 24, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579978

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mambo 10 vigingi kwa Waziri Simbachawene

UKURASA 3


UCHAMBUZI: CUF zaranu kutubiri sera yao mpya 'Furaha Haki kwa Wote'

Kimataifa

siasa

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ruto, kinara Kenya 'anayeutesa' Urais

BAADA YA MIAKA 55 Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-6

Mwendesha mashtaka asulubiwa, kisa Rais Ramaphosa Afrika Kusini

Bunge Marekani lachoshwa uswahiba wa Trump na mtawala wa Saudia

UKURASA 13

# Bashiru ajitosa sakata la Kinana na Makamba

**ASEMA** ligi waliyoianzisha si saizi yao, Pinda naye awapasha kiaina, makada Arusha, wazee Moshi nao watoa neno...

*Endelea ukurasa wa 2 & 12*



## Matatani kwa kujifanya daktari, JWTZ , polisi

UKURASA 2

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akiwaonyesha waandishi wa habari koti la kidaktari alilokutwa nalo mkazi wa Area A, Rajabu Kambi (kulia, aliyeshika picha inayoonyesha akiwa katika sare za JWTZ), aliyekamatwa kwa tuhuma za kuwatapeli watu mbalimbali, akijifanya askari wa Jeshi la Wananchi, askari polisi na daktari. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**BOTI YAZAMA YAUA 1, WANANE WATAFUTWA**

MTU mmoja amekufa maji na wengine wanane wanaendelea kutafutwa baada ya boti waliyokuwa...

UKURASA WA 4

**BIBI ANAYEDAIWA KUUA MJUKUU ANA KESI YA KUJIBU**

DAKTARI Msaidizi Mwandamizi, Modesta Lasana (52), amedai mahakamani kwamba...

UKURASA WA 25

**BORIS AMRITHI MAY UINGEREZA**

MBIO za kuwania kiti cha uwaziri mkuu Uingereza zinafikia tamati baada ya Boris Johnson kushinda...

## Malinzi, wenzake wana kesi ya kujibu

UKURASA 3


MICHEZO **SIMBA YAANZA KWA KUTOA DOZI SAUZI** UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Bashiru ajitosa sakata la Kinana, Makamba

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amejitosa katika sakata la malumbano yanayoendelea ndani ya chama hicho akiyafananisha na chandimu, mchezo wa mpira wa miguu unaochezwa na watoto mchangani.

Kiongozi huyo wa CCM amesema ligi iliyotengenezwa ndani ya chama hicho si ya saizi yao, akisisitiza kiko madhubuti na viongozi wake wako imara.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi wa vibanda vya biashara wa CCM mkoani Dodoma jana, Bashiru alisema kuna taratibu za kukosoana kwa nidhamu na kuwataka wanaoendekeza malumbano hayo waache alichokiita utoto.

Bashiru ametoa kauli hiyo ikiwa ni siku chache baada ya makatibu wakuu wastaafu wa CCM, Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba kutoa waraka wao wakilalama kudhalilishwa na mtu anayejiita mwanaharakati huru.

Aliwataka wanachama wa CCM kutopoteza muda kwenye malumbano badala yake waache aliowalenga "wabwabwaje kitoto wenyewe".

"Msijifanye majasiri kupambana na malumbano, hakuna ruhusa hiyo, waacheni wenyewe wabwabwaje kitotototo, watachoka wenyewe, na ukitaka kujua huu ni mchezo wa kitoto, wapinzani wameanza kuuchangamkia," alisema.

"Maana wao wanacheza chandimu, sisi tupo ngazi ya juu, 'game' (mchezo) yetu ni ya viwango vya kimataifa, ukiona wapinzani wamechangamkia porojo na upuuzi ndani ya CCM, ujue hao walioanzisha hawakitakii mema chama chetu na hawajui vizuri taratibu za chama.

"Mchezo wa kitoto waachiwe upinzani ambao baada ya mchezo huo kutangazwa wanachangamkia kucheza 'kindimu ndimu' na wanachafuka, kama unavyojua mchezo huo hauna nyasi, ni matope, mavumbi, hawana viatu, hiyo ligi iliyotangazwa siyo saizi yetu.

"Mchezo tuliorithi kutoka kwa Baba wa Taifa ni kuweza kujitawala, kuwekeza katika huduma za afya ili watoto wetu na wake zetu wapate afya bora, tuzaliane, tuongezeke."

Bashiru alisema mpira wa cha ndimu siyo wa kiwango chake na kwamba hawawezi kutishwa na watu wanaocheza mpira kwenye mavumbi, huku kocha wao anajificha ndani ya CCM.

Alisema wanatakiwa kujadili masuala ya kitaifa na kuacha kuchonga matatizo na ni marufuku ndani ya CCM kushambuliana, kutukanana na kubezana.

"Sisi uongozi mzima wa chama chetu, chama ni imara kimuundo, kimfumo, kiitikadi, kifalsafa na kiuongozi, wapuuzeni hao wapumbavu, hatuogopi kukosolewa, hatupo tayari kudharauliwa, kutukanwa na kubezwa na kuitwa majina ya kejeli kwa watu ambao hawana shukrani, hatujafunzwa wala kuzoea hivyo.

INAENDELEA UK 8



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, akizungumza na viongozi na wanachama wa chama hicho, katika uzinduzi wa mradi wa vibanda vya biashara vya CCM mkoa wa Dodoma, jana. PICHA: PETER MKWAVILA

## DCI azungumzia mhandisi anayedaiwa kujinyonga

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JESHI la Polisi Zanzibar limesema linaendelea na uchunguzi wa tukio la kujinyonga kwa mhandisi wa umeme, Ali Haji Khatibu, lililotokea juzi katika boti.

Marehemu Khatibu, aliyekuwa mhandisi wa meli ya Mapinduzi 2, anadaiwa kujinyonga wakati boti hiyo ikiwa katika safari zake kutoka Unguja kwenda Pemba.

Akizungumza na Nipashe, Naibu Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), Ahmed Msangi, alisema ni kweli Khatibu alijinyonga, lakini chanzo cha kuchukua uamuzi huo hakijajulikana.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha kujinyonga kwake.

Alieleza kuwa tayari mwili wa marehemu umeshakabidhiwa kwa jamaa zake na tayari umeshazikwa kijijini kwao Bambi, Wilaya ya Kati Unguja.

Khatibu anadaiwa kujinyonga juzi wakati meli ya Mv Mapinduzi ikielekea Pemba na ilipofika katika Bahari ya Kisiwa cha Tumbatu ililazimika kusitisha safari yake na kurejea Unguja kwa ajili ya kushusha mwili wa marehemu.

Meli hiyo ilikuwa na abiria 448 na ilikuwa ikiendeshwa na nahodha Abubakar Mzee.



# Matatani kwa kujifanya daktari, Kanali wa JWTZ, askari polisi

**Na Mwandishi wetu, DODOMA**

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linamshikilia mkazi wa Area A jijini hapa, Rajabu Kambi (23), kwa tuhuma za kujifanya askari polisi, Kanali wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na daktari.

Mtuhumiwa huyo pia anadaiwa kuwatishia watu kwa silaha bandia.

Inadaiwa kuwa licha ya kujifanya polisi, Kambi anajifanya daktari na kuwatapeli wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Gilles Muroto, alisema kijana huyo alikamatwa na sare za polisi (jangle green) ambazo ni za Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) zikiwa na 'hoster' yake.

"Mtuhumiwa huyu kwa muda mrefu katika mji wetu alijipatia huduma mbalimbali kwa udanganyifu kwa kujifanya polisi, kibaya zaidi muda mwingi alikuwa akivaa kofia ya pikipiki, amekuwa akipata huduma mbalimbali kwa kujifanya polisi," alisema.

Makanda Muroto aliongeza: "Kijana huyo amekuwa akiwalaghai wapangaji wenzake, mwenye nyumba na kuchukua pikipiki kuzunguka kutwa nzima halafu anawarejeshea bila kuwapa malipo yoyote vijana wa bodaboda ambao amekuwa akichukua pikipiki zao."

Muroto alisema watu wanaweza kudhani ni askari polisi kumbe si kweli na inaonyesha picha mbaya kwa jeshi hilo kuonekana askari wake wanafanya vitendo vya ovyo.

"Tumeona tumuonyeshe hapa ili wananchi waliofanyiwa vitendo hivi wamwone kwa kuwa ameonyesha picha mbaya kwa wananchi kwa jeshi lao," alisema.

Alifafanua zaidi kuwa kijana huyo amekuwa akitembea na silaha bandia kwa kuwatishia watu.

"Ameweka kishikio chake mtu ambaye hajui anaweza kusema ni pisto (bastola) kumbe ni toi, mtu huyu si wa kawaida na amebuni kwa kujiwekea cheo kikubwa cha ofisa wa jeshi, utapeli huu umefika mwisho wake, polisi hapa hatuna mchezo Dodoma," alisema.

Aliwaonya watu wote wanaotapeli watu kwa kujifanya ni polisi watakipata cha mtema kuni kwa kuwa Dodoma si mahali pa kufanyia utapeli.

"Amekutwa na picha akiwa na sare za JWTZ, uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa kijana huyu aliwahi kuhudhuria mafunzo ya JKT na kufukuzwa kwa utovu wa nidhamu," alisema.

Muroto alieleza kuwa kijana huyo pamoja na kujifanya polisi pia amekuwa akijifanya daktari kwa kutembea na koti la kidaktari. "Kuna watu wa aina hii wanapita na makoti na kujifanya madaktari na matokeo yake wanaleta taswira mbaya kuonekana hospitali haitoi huduma nzuri, kumbe wanahudumiwa na matapeli," alisema.

Aliwataka waganga na wauguzi wa hospitali kuwa makini na watu wanaojifanya madaktari kumbe ni feki.

"Kijana huyu amejifanya polisi na amejifanya daktari sasa anaweza kutoa huduma za ovyo akaonekana ni daktari au polisi kumbe ni tapeli ambaye anaingia Dodoma kuchafua makao makuu ya nchi...fanya kazi inayokupa riziki yako usifanye kazi ambayo haikuhusu brother," alisema.

## HABARI KITAIFA



Msukuma mkokoteni akiwasafirisha watoto wawili katika eneo la Mtaa wa Karume, Mji Mdogo wa Kibwaigwa, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vigingi 10 vinavyomkabili Simbachawene

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI mpya wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, juzi aliapishwa kushika wadhifa huo kutokana na mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri yaliyofanyika Jumapili iliyopita.

Simbachawene anachukua nafasi ya January Makamba, ambaye amekuwapo katika wadhifa huo, tangu Rais John Magufuli alipotangaza Baraza la Mawaziri baada ya kuingia madarakani Novemba, 2015.

Hiyo haikuwa mara ya kwanza kuwa Waziri kwani amekuwa katika nafasi ya namna hiyo mara mbili. Sasa ameingia kwenye historia ya kuwa waziri wa kwanza kutumbuliwa na kukaa nje ya baraza kwa miezi 23. Awali alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa). Pia aliwahi kuwa Waziri wa Nishati na Madini wakati wa serikali ya awamu ya nne chini ya Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete.

Wakati wa serikali ya awamu ya tano, alikuwa miongoni mwa mawaziri 19 wa baraza la kwanza la Rais Magufuli alilolitangaza Desemba 10, 2015.

Aliondolewa baada ya kujiuzulu Septemba 7, 2017, kutokana na kutajwa kwenye ripoti ya kamati ya Bunge ya Kuchunguza Biashara ya Madini ya Tanzanite na Almasi.

Wakati Simbachawene anashika wadhifa huo mpya, huenda akakabiliwa na mambo 10 yanayohitaji utekelezaji kabla ya kumalizika kwa kipindi cha kwanza cha Rais Magufuli, mwakani.

**VIGINGI 10**

Mambo hayo ambayo Nipashe imebaini ni kama;-

**KERO ZA MUUNGANO**

Moja ya kazi za wizara hii ni kushughulikia changamoto za Muungano ambao umetimiza miaka 55, ambazo kwa mujibu wa Waziri aliyepita ni ngumu kuzimaliza.

Changamoto za Muungano zimeshaundiwa kamati mbalimbali ikiwamo ya Baraza la Mapinduzi (ya Amina Salum Ali), Kamati ya Rais ya Kupambana na Kasoro za Muungano (ya Juma Ali Shamhuna, 1997) na ya Rais iliyochambua Ripoti ya Jaji Robert Kisanga (Kamati ya Salim Juma Othman).

Zingine ni Kamati ya Rais ya kuandaa Mapendekezo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) juu ya kero za Muungano, Kamati ya Ramia (2000) na ya Rais ya Masuala ya Simu (1996-1999).

Kero mojawapo ni Zanzibar kuruhusiwa kukopa bila dhamana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imekuwa ikileta mawazo kinzani miongoni mwa wadau wa Muungano.

Changamoto zingine ni Zanzibar kuwa na rasilimali zake ikiwamo suala la uchimbaji wa mafuta na gesi, kodi mara mbili,

INAENDELEA UK 8

# PM avutiwa NMB kutenga bil. 500/- kufufua viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameipongeza Benki ya NMB kwa kutenga zaidi ya Sh. bilioni 500 ili kuunga mkono juhudi za serikali katika Tanzania ya viwanda na kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Alisema hayo jana katika ufunguzi wa mkutano wa 35 wa Chama cha Mamlaka ya Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT), uliofanyika jijini Mwanza na kubainisha benki hiyo imekuwa mstari wa mbele kuisaidia serikali kukusanya mapato hasa katika ngazi ya halmashauri ambako kuna upotevu mkubwa wa makusanyo.

"Hii ni benki yetu, lazima tufanye biashara na benki tunayoimiliki katika masuala mbalimbali kama kilimo. Mnafanya vizuri katika kilimo cha pamba, karafuu, korosho na mazao mengine ya kimkakati," alisema Majaliwa. Vile vile, alisema benki hiyo imetenga zaidi ya Sh. bilioni 500 ili kuunga mkono mipango mbalimbali ya serikali kufikia uchumi wa kati na kuimarisha ustawi wa viwanda nchini.

Kiasi hicho kilitengwa mwaka jana ili kuunga mkono kilimo kwa kipindi cha miaka mitano, hii ni mara ya pili benki hiyo kutenga kiasi kama hicho cha fedha, mwaka 2015 NMB ilitenga Sh. bilioni 500 kusaidia sekta ya kilimo. Licha ya kusaidia ukuaji wa uchumi, benki pia imeelezea kujitolea kwao katika kuhudumia Biashara ndogo na za kati (SMEs), zilizotawanyika katika mamlaka tofauti ya serikali za mitaa kote nchini na zaidi ya Sh. bilioni 600 zilizosaidia mitaji ya biashara ndogondogo nchini.

Awali akitoa maelezo kwa Waziri Mkuu, Mkuu wa Biashara za Rejareja katika benki hiyo, Filbert Mponzi alisema, malengo ya benki ni kufikia biashara ndogo na kati zaidi na kutoa suluhu ya kifedha kulingana na mahitaji ya wafanyabiashara hao.

Alisema, hadi sasa zaidi ya Sh. bilioni 700 imewekezwa katika sekta hiyo na benki tayari imeshatoa jumla ya Sh. bilioni 40 kila mwezi kwa vikundi tofauti vinavyoungana kwa kilimo kidogo na cha kati nchini.

Wakielezea namna walivyoguswa na msaada wa NMB, wanachama tofauti wa ALAT akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Njombe, Ally Juma Ally na mwenzake kutoka Chato, Eliud Mwaiteleke walieleza kuwa huduma ya kifedha ya NMB ina faida mbalimbali za kiuchumi.

# Mahakama yamkuta Malinzi na kesi ya kujibu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imesema Rais wa zamani wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Jamal Malinzi na wenzake watatu wana kesi ya kujibu dhidi ya tuhuma za kutakatisha Dola za Marekani 173,335.

Uamuzi huo umetolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Maira Kasonde baada ya kusikiliza mashahidi 15 wa Jamhuri.

Hata hivyo, mahakama hiyo imemwachia huru Meneja wa Ofisi TFF, Mariam Zayumba, baada ya ushahidi wa jamhuri kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yake hiyo.

"Baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi 15 wa jamhuri bila kuacha shaka, mahakama yangu imewaona washtakiwa wanne kati ya watano wana kesi ya kujibu na inamwachia huru Zayumba dhidi ya mashtaka hayo," alisema Hakimu Kasonde. Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo unaongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai.

Upande wa utetezi uliongozwa na wakili Richard Rweyongeza.

Washtakiwa hao kwa nyakati tofauti walidai kuwa watajitetea kwa njia ya kiapo. Hakimu alisema kesi hiyo itasikilizwa ushahidi wa upande wa utetezi Agosti 6, mwaka huu.

Washtakiwa waliokutwa na kesi ya kujibu mbali na Malinzi, ni Katibu Mkuu wa zamani wa Shirikisho Selestine Mwesigwa, Mhasibu wa TFF, Mwanga na Karani wa TFF, Flora Rauya, ambao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 30 katika kesi ya jinai namba 213 ya mwaka 2017.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa walikula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Dola za Marekani 173,335.

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wanaendelea kusota rumande kwa sababu wanakabiliwa na mashtaka ya utakatishaji fedha ambayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria.




## Boti yazama yaua 1, wanane watafutwa

**Na Suleiman Rashid Omar,**

**PEMBA**

MTU mmoja amekufa maji na wengine wanane wanaendelea kutafutwa baada ya boti waliyokuwa wamepanda kukumbwa na upepo mkali na kuzama.

Watu hao waliokwenda baharini kuvua wakiwa na boti mbili aina ya Faiba, walikumbwa na dhoruba ya upepo na vyombo vyao kuzama. Jitihada zilifanikiwa kuwaokoa watu wawili na mmoja akiwa ameshakufa maji.

Taarifa ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba, Omar Khamis Othuman, ilimtaja aliyepoteza maisha kuwa ni Hamadi Bakari Mwinyi, mkazi wa Washumba aliyekuwa na wenzake wanane ambao hawajaokolewa.

Wavuvi wanaoendelea kutafutwa ni Mohamed Makame Mwinyi, Omar Ali Hasan, Kombo Ali Hassan, Rashid Othuman Ali, Mwalim Bosi Hasan, Kombo Faki H. Malim, Omar Kombo Fakih na Said Ali Omar.

Alisema juhudi za kuwatafuta wavuvi zimekuwa ngumu kutokana na upepo mkali unaovuma baharini.

Akiahirisha zoezi la kutafuta watu hao, Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba, Omar Khamisi Othuman, alisema ingawa sio jambo la kawaida kwa mtu kuzama kwenye bahari muda mrefu na kukutwa akiwa hai, wataendelea na juhudi za kuwatafuta hadi watakapo fanikiwa kuwapata.

Naye Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Shamata Shame Khamis, alisema ana matumaini ya kuwapata wakiwa wazima kwa vile bahari katika maeneo ya visiwa yana sehemu nyingi.

"Inawezekana wamefanikiwa kwenda kujiokoa sehemu ya juu eneo la mbali ambapo bado hawajafikiwa kuokolewa," alisema.

# Kigwangalla 'ampa pole' Bashe

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, amempa pole Mbunge wa Nzega Mjini, Hussen Bashe, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo.

Dk. Kigwangalla alitoa pole hizo juzi katika kurasa zake za Instagram na Twitter ikiwa ni muda mfupi baada ya Bashe kuapishwa na Rais John Magufuli kushika wadhifa huo. Bashe aliteuliwa katika nafasi hiyo Jumapili iliyopita.

Katika ujumbe wake aliotuma kwenye ukurasa wake wa Twitter juzi, Dk. Kigwangalla aliandika hivi: "Nakupongeza kwa uteuzi na nakupa pole kwa kazi iliyo mbele yako. Sina shaka na uchungu ulio nao dhidi ya maskini. Napajua unapotoka, muhimu jua wazi kuwa Rais Magufuli ana uchungu na wanyonge na hana utani kwenye hili. Nenda kapige kazi kwa bidii."

Aidha, kupitia ukurasa wa Instagram alieleza kwa kina kumpongeza Bashe na kuteuliwa kushika nafasi hiyo na kuendelea kusisitiza kumpa pole kwa kazi iliyo mbele yake.

"Pacha (Hussen Bashe) kwanza kwa mara nyingine tena, nakupongeza kwa uteuzi na kwa imani aliyokupa Mh. Rais na pili nakupa pole kabisa kwa kazi iliyo mbele yako.

"Mungu amesikia kilio cha wazee wetu wengi wa Nzega, ambao wengi wao walishatangulia mbele ya haki. Wazee wa Nzega waliomba sana kupata Waziri tangu tupate uhuru, haikutokea mpaka nilipoteuliwa mimi na Rais Magufuli kuwa Naibu Waziri wa Afya. Leo na wewe umeingia, wazee wa Nzega wamepata majibu ya dua na maombi 'double' (mara mbili) sina shaka na uchungu ulio nao dhidi ya maskini," Dk. Kigwangalla alisema.

Alimtaka kwenda kufanya kazi kwa bidii, kuwa mbunifu, kufanya kazi wakati wote, kuwa mnyenyekevu kwa wadau wa watu wote kwa kuwa atapimwa kwa vitu vingi na jamii siyo kwa kujenga hoja nzito bungeni pekee.

"Usithubutu kushindana au kupingana na mkubwa awaye yote. Mara zote kumbuka zile kanuni tatu muhimu za mafanikio mahali pa kazi ambazo ya kwanza hadi ya tatu ni 'The boss is always right' (mkuu wakati wote yupo sahihi), 'be humble' (kuwa mnyenyekevu), hautapotea, 'all the best bruv' (kila la kheri kaka)," alisema Dk. Kigwangalla katika ukurasa wake huo wa Instagram.

Katika mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri aliyofanya Rais Magufuli Jumapili, alimteua Bashe kuchukua nafasi ya Innocent Bashungwa ambaye hivi karibuni aliteuliwa kuwa Waziri wa Viwanda.

Aidha, Mbunge wa Kibakwe, George Simbachawene, aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuchukua nafasi ya January Makamba ambaye uteuzi wake ulitenguliwa. Pia Rais Magufuli alimteua Balozi Matern Lumbanga kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).




Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Derick Lugemala (wa pili kulia), akitia saini mkataba wa makubaliano na kampuni ya Heifer International Tanzania, jijini Dar es Salaam jana, lengo likiwa ni kuendeleza na kukuza sekta ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bibi anayedaiwa kuua mjukuu ana kesi kujibu

**Na Hellen Mwango**

DAKTARI Msaidizi Mwandamizi, Modesta Lasana (52), amedai mahakamani kwamba uchunguzi wa kifo cha Naomi John (7), ulionyesha kwamba alikufa kutokana na mivunjiko mwilini ikiwamo fuvu la kichwa kupasuka, damu kuvilia kwenye ubongo na majeraha yaliyotoa usaha.

Kadhalika, shahidi amedai katika kesi ya mauaji ya Naomi inayomkabili bibi yake Ester Lyimo (41), kuwa mwili wa marehemu ulikuwa na majeraha yaliyotoa usaha sehemu zake za siri pamoja na vidonda kwenye makalio yake vilivyotokana na kuunguzwa moto.

Ushahidi huo ulitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji iliyoketi chini ya Naibu Msajili, Pamela Mazengo.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Cecilia Mkonongo, akisaidiana na Joyce Nyumayo.

Akiongozwa na Mkonongo, shahidi alidai kuwa alikabidhiwa mwili wa Naomi aufanyie uchunguzi na kwamba kazi yake ina hatua mbili tofauti ya kwanza nje ya mwili na pili ndani ya mwili.

"Nje ya mwili wa Naomi ulikuwa na makovu ya zamani na majeraha yaliyokuwa na vidonda vilivyotoa usaha ikiwamo sehemu zake za siri kuonyesha michubuko ya kitu kigumu, tumbo lilikuwa limesinyaa kwa kukosa chakula muda mrefu na makalio yalikuwa na vidonda vya kuunguzwa moto," alidai shahidi na kuongeza:


"Kwa upande wa ndani, kwa kuwa kichwa kilivimba nilifungua nikaona fuvu lilikuwa limekatika, damu mpya na ya zamani ilisambaa kwenye ubongo, mkono mmoja ulivunjika mara mbili na bega lilishuka," alidai Dk. Lasana aliyemfanyia uchunguzi marehemu Naomi.

Akifafanua zaidi alidai kuwa akiwa na daktari mwenzake katika uchunguzi huo, walifunua fuvu na kubaini kilichomuua Naomi ni, mivunjiko ya muda mrefu, majeraha mapya na ya zamani kutokana na kukosa matibabu kwa muda mrefu.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa umefunga ushahidi wake kwa kuita mashahidi wanane. Msajili Mazengo alisema mahakama yake imemkuta mshtakiwa na kesi ya kujibu na kwamba ushahidi wa utetezi utasikilizwa katika kikao kitakachopangwa tena na Msajili wa Mahakama Kuu.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Machi 25, 2017 Tuangoma Wilaya ya Temeke jijini Dar es Salaam mshtakiwa alimuua mjukuu wake kwa kumpiga.

# TANGAZO




Vigezo na masharti kuzingatiwa. Barclays Bank Tanzania yenye usajili namba 38557 inaendeshwa na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania. Barclays Bank Tanzania Limited inatumia chapa ya Barclays chini ya leseni ya Barclays Bank Plc.

215333601

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuujue umuhimu wa bahari yetu

MOJAWAPO ya rasilimali muhimu dunia kwa sasa ni bahari, ambayo Watanzania wengi waliamini kuwa bahari ni sehemu ya kuvua samaki na kwa ujumla wachache wanafahamu umuhimu wa kulinda na kutunza rasilimali bahari kwa manufaa yao na afya ya mazingira ya dunia.

Ukweli ni kwamba bahari leo ni muhimu kama ilivyo ardhi kwani ni chanzo cha shughuli za kibiashara zenye uhusiano na nishati ya maji kwani inaweza kutumiwa kufua umeme wa maji.

Pia zama hizi ni chanzo cha nishati kama gesi, mathalani kiasi kikubwa cha gesi inayopatikana na kuzalisha umeme nchini inatoka baharini na pia utafiti unaendelea kufanywa ili kupata mafuta na madini, yote haya ni mambo yanayotokana na bahari.

Aidha, kuwapo kwa chakula kama samaki, mimea mfano mwani unaozalishwa huko Zanzibar na pia kuwa barabara inayofanikisha na kuwezesha usafirishaji kutoka bara moja kwenda jingine ni sehemu ya mambo makubwa yanayofanywa na bahari.

Kwa hiyo tunaona kuwa bahari ni eneo muhimu na la kipekee ambalo linaweza kuitwa hazina ya rasilimali zinazoweza kukuza uchumi, kuzalisha nishati na kuchangia maendeleo na ukuzaji wa maendeleo ya taifa.

Leo hii bahari inaonekana kama sehemu inayotishia uhai wa dunia kwa vile vimbunga kama Tsunami huanzia humo, hivyo ni muhimu kulinda eneo hilo linalotishiwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Tunazungumzia ulinzi wa bahari kwa kuwa zama hizi kumekuwa na mijadala mingi inayozungumzia mabadiliko ya tabia nchi. Mojawapo za athari za mabadiliko hayo ni ongezeko la joto duniani.

Wiki hii kumekuwa na upepo mkali unaovuma kutoka baharini na hata kutishia kuezua nyumba na kuangusha miti.

Yote hayo ni mambo yanayoanzia baharini, ndiyo maana tunaona kuwa kuna umuhimu wa kulinda bahari kutokana na vitisho kama upepo mkali.

Njia mojawapo ni kupanda mikoko na kuitunza ili kudhibiti upepo na majanga mengine kama Tsunami.

Katika zama hizi taasisi za mazingira duniani zinakumbusha kwamba kulinda na kutunza kwa ubora mazingira ya bahari ni muhimu kwani bila kuwa na utawala wa sheria na usimamizi bora wa eneo hilo athari za mabadiliko ya tabia nchi zinaweza kuwa kubwa.

Miaka hiyo bahari ilitumiwa kama chanzo cha kutupa uchafu yakiwamo mabaki ya sumu viwandani, kemikali za sumu na hata kumwaga mafuta kwenye bandari mbalimbali.

Ukweli ni kwamba shughuli za kibiashara zenye uhusiano na maji kama uvuvi wa bahari kuu, kilimo cha mwani, kuchimba gesi na vyanzo vingine vya nishati vinaifanya habari kuwa moja ya vyanzo vikuu vya uchumi pengine kama ilivyo ardhi, hivyo ni lazima kuitunza na kuilinda kwa nguvu zote.

Watanzania wajue kuwa leo si wakati wa kuitumia bahari kama eneo la kuchafua mazingira kwani wapo watu baadhi ya wakazi au wafanyabiashara wa maeneo ya ufukweni waliokuwa wanaitumia kama maliwato.


Waliitumia kama sehemu ya kujisaidia bila kujua kuwa bahari haiweza kukaa na uchafu itautapika na mojawapo ya kinachofanyika ni kurudisha vinyesi ufukweni. Vikirudishwa huenda vikaangukia mikononi mwa wavuvi, wachuuzi wa samaki na hata wanaopata burudani ufukweni.

Miongoni mwa masuala muhimu yanayokubaliwa na jumuiya ya kimataifa ni kuwa na mikataba ya kulinda na kutunza matumizi ya bahari na viumbe vilivyomo.

Kwa hiyo ni muhimu Watanzania wakazingatia matumizi bora ya bahari kama eneo la kutunzwa na kulindwa kwa maendeleo ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Serikali isiridhie programu mzigo kwenye shule binafsi

Na Salome Kitomari

**WIKI** kadhaa zilizopita wamiliki wa shule binafsi walilalamika kuanzishwa kwa programu zinazowalazimu kuzilipia, na kuitaka Serikali kuzichunguza na hatimaye kuchukua hatua ili kupunguza usumbufu na gharama.

Malalamiko hayo yalitokana na barua waliyoandikiwa na Wizara ya Elimu kuwa imekubali taasisi ya Anti-Poverty and Environment Care (Apec), kutoa mafunzo kwa madereva wa mabasi ya wanafunzi katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam.

Katika barua ya Taasisi hiyo, imependekezwa kwamba madereva wapewe vyeti vya Apec, baada ya mafunzo.

Aidha, wanataka maofisa elimu kata kuendesha ukaguzi na kuchukua hatua kwa madereva ambao hawatakuwa na vyeti vya taasisi hiyo.

Katika malalamiko yao wamiliki wa shule hizo walibainishwa kwamba si mara ya kwanza kwa wizara kuridhia watu na taasisi mbalimbali kuwapelekea programu ambazo huwaingiza kwenye gharama kubwa.

Gharama ambazo wakati mwingine hufikia hadi kiasi cha Sh. 300,000 kwa mtumishi mmoja.

Walikwenda mbali zaidi na kutoa mfano wa programu za madereva zilizoletwa mwaka jana, ambapo shule zilitakiwa kugharimia Sh. 300,000 kwa kila dereva wake kwa mafunzo yalifanyika kwa wiki moja.

Mbaya zaidi wakabainisha kwamba pamoja na gharama hizo hawajawahi kuona mitaala ya vyuo au taasisi hizo.

Kwa kawaida vyeti vya udereva hutolewa na vyuo vilivyosajiliwa na Serikali, vikiwamo vya Veta na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

Lakini ni ajabu taasisi binafsi inapofikia hatua ya kuwa na nguvu ya kutoa maelekezo ya kukamatwa madereva iwapo hawataonyesha vyeti vilivyotolewa na taasisi hiyo, na walengwa wakiwa shule binafsi pekee.

Wachambuzi wa elimu wanahoji iweje suala hili lielekezwe kwa madereva wa shule binafsi, huku wa umma ambao ndio husafirisha wanafunzi wengi wakiachwa?

Kwa nini kuwe na makundi mawili ya wanafunzi kwamba wale wa shule binafsi waendeshwe na madereva waliofunzwa vyema na wengine wabaki na vyeti vilivyowawezesha kupata leseni tu?

Usafiri wa umma unategemewa na wanafunzi wengi zaidi na huko ndiko kuna utitiri wa mabaya kama vile matumizi ya lugha chafu kwa wanafunzi bila kujali umri wao.

Hivyo, Muungwana anaona kwamba kama lengo ni kufanya maboresho ili kuwa na maadili, ni vyema mafunzo haya yakawa kwa madereva wote bila ya kubagua.

Vilevile, hili la wamiliki wa shule binafsi kulundikiwa programu nyingi za kulipia kwa ajili ya watumishi wao ni vyema likaangaliwa pia, kwani linaathiri utendaji wa shule hizo.

Kwamba kutakuwa na ongezeko la michango na hivyo wazazi ndio watakaotwishwa mzigo wa kutozwa ada zaidi na wamiliki wa shule.

Na hiyo ni katikati ya kilio cha muda mrefu cha wazazi juu ya ada kubwa inayotozwa na shule binafsi nchini na mara kadhaa Serikali imeahidi kulitazama suala hilo lakini utekelezaji wake umekuwa ni mgumu.

Muungwana haoni umuhimu wa kuongeza mzigo huu kwa wazazi kupitia mafunzo ambayo wamiliki wa shule hawajaridhika nayo.

Kama kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa madereva, uwekwe utaratibu iwe ni sehemu ya elimu wanapokwenda vyuoni.

Mzazi ambaye ni mwajiriwa anatozwa kodi kwenye mshahara wake, anaponunua bidhaa, kama anamiliki gari anatozwa kodi kwenye mafuta, anapolinunua gari anatozwa kodi.


Aidha, anatakiwa kuwa na stika ya nenda kwa usalama, anakata bima kwenye gari yake, anapotumia simu kupiga, kupokea, kutuma fedha nako anakatwa kodi.

Mzazi huyo huyo ambaye anasomesha mwanaye katika shule binafsi kuliko na mazingira mazuri zaidi ya utoaji elimu, nako anakutana na ongezeko la ada linalochangiwa na michango mingi ikiwamo inayoridhiwa na Serikali kupitia taasisi mbalimbali.

Muungwana akiwa ni mzazi, mdau wa elimu na mwanahabari anaona kabisa kwamba jambo hili si sahihi, zaidi ya kuwaumiza wazazi.

Hivyo ni vyema Serikali ikaliangalia kwa umakini mkubwa.

## MJADALA




# Jamii ipiganie mavazi ya staha ulimwengu huu wa utandawazi

**Na Raphael Kibiriti**

MAVAZI ni moja ya vitambulisho vya taifa lolote lile, jamii, kabila na hata makundi mbalimbali katika jamii.

Na ndiyo maana ya maneno kama vazi la taifa, vazi la michezo, sare za mahitaji mbalimbali na hata kuna baadhi ya watu hujiwekea utambulisho binafsi kupitia mavazi.

Uzuri au ubaya wa kitu, ni tafsiri mbalimbali ambazo zinafanya nafsi ya mtu kujieleza, mara nyingi mavazi katika namna ya kipekee yana nafasi kubwa zaidi ya kuwasilisha ujumbe.

Pamoja na uzuri wa kitu au mambo, unaopatikana kupitia mavazi, katika sura ya pili matumizi mabaya au upotoshaji wa namna yoyote katika matumizi yake, yamezua matatizo makubwa katika jamii, hata kufarakanisha wanafamilia.

Sasa malalamiko yametawala, kiasi cha kwamba hata kwenye nyumba za ibada, ambako kunaheshimiwa kwa namna ya kipekee, matumizi mabaya ya mavazi moja kwa moja huwasilisha ujumbe wa kutoheshimu sehemu hizo.

Kimsingi, tafsiri ya mavazi ya heshima hutegemea imani, mila na desturi ya jamii husika.

Hivyo, mavazi ya heshima ni yale yanayozingatia mila na desturi za jamii katika hatua mbalimbali zilizoko, hadi ngazi ya taifa.

Vazi linaloendana na mahitaji ya jamii na miongozo ya ngazi hizo husika, yana maana kubwa sana.

Mathalani, katika sehemu nyingi staha ya mwanadamu ni kuvaa nguo inayohifadhi baadhi ya sehemu za maungo ya miili yao, ambayo kwa mujibu wa imani na desturi, si mahali pa kuachwa wazi.

Kwa kutumia kigezo hicho hicho, ndiyo inazaa marufuku kwa baadhi ya mavazi, ama yasivaliwe kabisa au hayapaswi kuvaliwa katika baadhi ya mazingira na maeneo mbalimbali, mfano hai ukiwa ni kutoruhusu mavazi ya michezo kuvaliwa na wafanyakazi katika sehemu wanakotumikia.

Tafsiri hiyo inaenda mbali zaidi kwa kina mama kuambiwa mavazi yanayobana, mafupi yanayoacha magoti na sehemu za mwili wazi, hali kadhalika kitovu na kifua.

Mwaka 1971, chama cha TANU ambacho kilikuwa kimeshika hatamu za uongozi wa nchi wakati huo, kilitoa waraka maalumu wenye mwongozo kuhusu mavazi.

Madhumuni ya waraka huo, yalikuwa kuimarisha heshima ya taifa, kwa mujibu wa imani ya jamii yake, ikilenga kuhakikisha kuwa watumishi katika sehemu za kazi wanadumisha staha ya heshima wawapo kazini.

Tukichukua kinachojiri leo mbele ya umma kuhusu mavazi na kilichoagizwa kwenye waraka huo wa Tanu, tofauti ni ya kutisha.

Mitindo ya mavazi hivi sasa inaporomosha thamani ya jinsia zote mbili katika jamii. Kwa kifupi hali ni tete.

Pengine hali ingekuwa ni mbaya zaidi, lakini tunapaswa kuzishukuru asasi za kidini, sehemu ambako imani ya umma imeshikiliwa.

Kwa watoto wa kike, imekuwa sehemu ya maisha yao kuvaa nguo fupi zinazoonyesha umbile la miili yao.

Kwa tafsiri yao, wanajihisi wanakuwa warembo zaidi na wanakubalika katika jamii yao ya Kitanzania, kwa kukumbatia utashi huo wenye mzizi kwenye utandawazi.

Ni jambo linalowagharimu wengi katika jamii, baadhi wakifukuzwa au kuzuiwa kuingia kwenye ofisi na nyumba za ibada au hata kutokukubalika katika makazi binafsi.

Jumuiya ambayo msingi wake ni mkusanyiko wa watu kwa lengo maalumu ina tafsiri pana, pia huendana na haja ya mtu mmoja mmoja au kikundi kutaka kukubalika nayo.

Inaweza kuwa kwenye kituo cha basi, sokoni, hospitali, nyumba za ibada, shuleni au vyuoni.

Moja ya tiketi muhimu katika kujumuika nayo ni vazi linalokubalika, kama nguo ndefu kwa kinamama ambayo ina kawaida ya kumbandika alama ya kimantiki kuwa mvaaji ni mstaarabu.

Katika mavazi kuna neno kujisitiri ambalo maana yake ni kuficha kitu mahali ili kisionekane.

Lakini kwa karne ya sasa wanaume kwa wanawake, wamekuwa wakivaa mavazi yasiyo na staha kwenye jamii.

Mjadala una rai kwa jamii ya sasa kujirekebisha kimavazi kwa kuvaa nguo zenye staha, na kujikita kwenye maadili kama jinsi mababu zetu walivyokuwa wakiishi, kwa kufuata mila na desturi za taifa letu.


**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERMRNT AUTHORITY.**
**TARIME DISTRICT COUNCIL**

**INVITATION FOR BIDS (IFB)**

**Date: 24th July, 2019**

1. Tarime District Council has set aside funds for **Conducting Hydro Geophysical Survey and Drilling of Two (2) Boreholes, Supply and Install Two (2) Hand Pumps at Kiterere Village and Construction of Six (6) Dams at Matamankwe, Surubu, Rosana, Kwisarara, Nyabirongo-Kwihancha and Msege Village in Tarime District Council** during the financial year **2019/2020.** It is intended that, part of the proceeds of the funds will be used to cover eligible payment under this invitation for bids.

2. The **Tarime District Council,** now invites sealed tenders from eligible qualified Contractor's registered with the Contractors Registration Board (CRB) to carry out

| TENDER NO. | SCOPE OF WORK | ELIGIBLE CONTRACTOR |
|---|---|---|
| LGA/067/2019/2020/W/01-LOT 1 | Construction of Six (6) Dams at Matamankwe, Surubu, Rosana, Kwisarara, Nyabirongo-Kwihancha and Msege Village in Tarime District Council | Civil Contractor Class Six and Above. |
| LGA/067/2019/2020/W/01-LOT 2 | Conducting Hydro Geophysical Survey and Drilling of Two (2) Boreholes, Supply and Install Two (2) Hand Pumps at Kiterere Village. | Specialist Contractor (Drilling) |

3. Bidding will be conducted through the **National Competitive Bidding procedures specified in the Public Procurement (Goods, Works, Consultancy Services, Non - Consultancy Services and Disposal of Public Assets by Tender)** Regulations, **2013** – Government Notice **No.446** and are open to all Bidders as defined in the Regulations.

4. Interested eligible Bidders may obtain further information and inspect the Bidding Documents at **Tarime District Council, Procurement Management Unit, P.O Box 16, Tarime** from Monday to Friday except on Public holidays.

5. A complete set of Bidding Document (s) in English may be purchased by interested Bidders on the submission of a written application to the address given under paragraph 4 above and upon payment of a non-refundable fee of **Tanzania Shillings One Hundred thousand only (Tshs.100,000/=)** Payment should be through bank **NMB DED-TARIME A/C. No.30410001496.**

6. All bids in **One Original** plus **Two Copies,** properly filled in, accompanied with **Bid Securing Declaration** and enclosed in separate plain inner envelope marked **'Original'** and **'Copy'** as appropriate, sealed in one plain outer envelope must be delivered to the undersigned before the deadline date to **Tender Board Secretary, Tarime District Council, P.O Box 16, Tarime.**

7. The deadline for the submission of bids is **10:00 Am** local time on **Tuesday, 06/08/2019** Bid will be opened immediately thereafter in public and in the presence of Bidder's representative who choose to attend.

8. Late bids, portion of bids, electronic bids, and bids not received, bids not opened and not read out in public at the bid opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstance.

**SYLVANUS GWIBOHA**
**Ag. DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR**
**TARIME DISTRICT COUNCIL**

215337402

# Vigingi 10 vinavyomkabili Simbachawene

INATOKA UK 3

malalamiko ya kulipa kodi mara mbili kwa watu wanaoununua bidhaa Zanzibar na kuzipeleka Bara.

**BAJETI FINYU**

Suala la kutengewa bajeti kidogo kwa wizara hiyo ni changamoto kubwa atakayokabiliana nayo Simbachawene. Hatua hiyo husababisha baadhi ya miradi ya maendeleo kutokamilika au kutotekelezwa kabisa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mohamed Mchengerwa, alinukuliwa akisema hadi Machi 26, mwaka jana, haikuwa imepokea hata senti moja kati ya Sh. bilioni moja zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi miwili ya maendeleo kwa mwaka 2017/18.

Miradi hiyo ni ya ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (Zanzibar) na ujenzi na ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II (Dar es Salaam).

Pia hadi Machi 8, mwaka jana, hakuna hata senti moja ya fedha za ndani zilizokuwa zimetolewa kati ya Sh. bilioni mbili zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mfuko wa Mazingira.

Mwaka 2016/17, Bunge liliidhinisha Sh. bilioni 10.973 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wizara hiyo lakini hadi Machi 15, 2017, ni Sh. bilioni 1.238 (asilimia 11.3) zilizokuwa zimepokewa.

Mtiririko huu usioridhisha wa utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni kigingi kingine kwa Simbachawene katika majukumu yake ili kufikia malengo yanayotakiwa.

Katika mwaka 2019/20, Makamba alieleza bunge kuwa ameomba fedha hizo kwa miradi ya maendeleo ambayo ni kuratibu vikao vya pamoja vya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia masuala ya Muungano na ufuatiliaji wa maelekezo na maagizo yaliyotolewa na vikao.

**SERA YA MAZINGIRA**

Jambo jingine ambalo atapaswa kuhakikisha linafanikiwa ni kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na mkakati wake wa utekelezaji na kuendesha Tuzo za Rais ya Hifadhi ya Mazingira.

Yote hayo yamo kwenye makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2019/20 ambayo yaliwasilishwa Bungeni Aprili, mwaka huu na aliyekuwa waziri wa wizara hiyo, Makamba.

**RIPOTI YA MAZINGIRA**

Katika kipindi cha uongozi wake, Simbachawene atatakiwa kuchapisha ripoti za nakala ya ripoti ya tatu ya hali ya mazingira ya mwaka 2018, kuelimisha na kuhamasisha umma ili kuhakikisha kuwa na mkaa mbadala.

**MABADILIKO YA TABIA NCHI**

Moja ya changamoto kubwa zinazoikabili dunia ni mabadiliko ya tabia nchi, ambayo athari zake zimeshaonekana kwenye nchi mbalimbali, Tanzania ikiwamo.

Kupungua kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro, mabadiliko ya vipindi vya mvua, ukame wa muda mrefu, mafuriko, kazi kubwa ni kuwaelimisha wananchi kupanda miti, kutunza mazingira na kuepuka kujenga kwenye vyanzo vya maji au kando ya mito.

**MRADI UMEME RUFIJI**

Kumekuwa na pingamizi kwa wadau wa mazingira wa ndani na nje ya nchi, vikiwamo baadhi ya vyama vya upinzani ambavyo vinadai kuwa kutakuwa na uharibifu wa mazingira kwenye Pori la Akiba la Selous kutokana na utekelezaji wa mradi wa umeme wa maji katika Bonde la Mto Rufiji.

Mradi huo unaojengwa kwa fedha za serikali, utagharimu Sh. trilioni 7.6 na utazalisha Megawati 2,100, ambao baada ya kukamilika kwa matayarisho ya awali utazinduliwa Julai 26, mwaka huu.

Wanaopinga suala hilo pamoja na kuho-



fia usalama wa mazingira ya eneo hilo ambalo ni urithi wa dunia, wanapendekeza matumizi ya nishati itokanayo na gesi kuliko kutegemea umeme wa maji pekee.

Katika hilo, Simbachawene ana changamoto ya kutetea utekelezaji wake na pia kuhakikisha suala la mazingira linapewa kipaumbele cha kipekee ili athari zinazozungumzwa na wanaharakati na wadau wengine zisitokee.

**MIFUKO YA PLASTIKI**

Kampeni ya kufuta mifuko ya plastiki nchini imefanikiwa tangu Juni Mosi, mwaka huu na sasa kuna mifuko mbadala. Hata hivyo, katika eneo hili kuna changamoto ya mifuko ya vifungashio ambayo bado ni ya plastiki.

Aidha, bado kuna viatu na vyombo vya plastiki vinazalishwa na kuuzwa nchini, ambavyo vinatajwa kuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira kutokana na kuishi kwa miaka mingi kwenye ardhi bila kuoza.

**UVAMIZI VYANZO VYA MAJI**

Kumekuwa na ongezeko la uvamizi wa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za binadamu kama makazi na kilimo, kiasi cha kushindwa kutekelezwa matakwa ya kisheria ya shughuli hizo kufanyika umbali wa mita 60.

Mathalani, jiji la Dar es Salaam shughuli hizo zinafanyika kwenye Mto Msimbazi kwa kuwa wananchi wamejenga hadi kando ya vyanzo vya maji na mafuriko yanapokuja huzoa au maji kujaa kwenye nyumba zao na kukosa pa kuishi.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc), lililo chini ya wizara hiyo, liliainisha nyumba zinazotakiwa kubomolewa lakini utekelezaji ulishindikana na hadi sasa kuna nyumba hazijabomolewa licha ya kutambulika.

**TATHMINI YA MAZINGIRA**

Moja ya changamoto kubwa ni uendeshaji wa tathmini ya matumizi ya mazingira kwa wawekezaji ambao huchelewa kupata vibali na hivyo kuchelewesha shughuli za uwekezaji kufanyika.

Waziri huyo alipewa agizo na Rais John Magufuli, baada ya kumwapisha kwa kumwambia atatue changamoto ya ucheleweshaji wa vibali kwa wawekezaji inayolikabili Nemc.

"Vibali kwa mfano vya Nemc, pasiwe na ucheleweshaji utoaji vibali kwa viwanda vyetu, tunataka kuwa na viwanda vya kutosha na wawekezaji wasiwekewe vipingamizi kwa visingizio vya Nemc, vibali hivi vitoke kwa wakati," alisema.

Licha ya ucheleweshaji wa vibali hivyo, baadhi ya waombaji wamekuwa wakilalamika kuwa Nemc imekuwa ikiwataka kulipia gharama za vikao ikiwamo posho kwa wajumbe wakati wa mchakato huo.

**USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

Aidha, katika moja ya agizo alilopewa na Rais ni kusimamia mazingira na changamoto zake.

Hili nalo ni jambo ambalo litahitaji usimamizi wa karibu hasa kwa nyakati ambazo bado wananchi wanatumia nishati ya mkaa kwa ajili ya kupika, wakitegemea kama ajira ya kujipatia kipato kutokana na kukata mkaa na kuvuna mbao.

# Bashiru ajitosa sakata la Kinana, Makamba

INATOKA UK 2

"Wana CCM jifunzeni kutoka kwa kiongozi wetu ambaye wakati wote hana muda wa malumbano, wakati wote amevumilia wanaomtusi, wengine wana umri wa watoto wake, amewavumilia na yupo tayari kuwasamehe lakini kwa kufanya hivyo siyo uoga, kazi ya kujenga chama ni ya kufa na kupona.

"Kuna watu watataka kuchukulia upuuzi unaoendelea kama wao ni makada kuliko wengine, kutafuta kiki ya kisiasa, wale wanaoleta 'clip' wanauza kwangu, utafukuzwa kwa kuwa tunazo taratibu zetu, kanuni na katiba.

"Ole wake mwanaCCM yeyote atakayetaka kutumia fursa ya wapumbavu wa mwaka, kutafuta kiki ya kisiasa ili achaguliwe uchaguzi wa serikali za mitaa, hapana tusifanye hivyo," Bashiru alionya.

Aliongeza kuwa Mwalimu Nyerere alisisitiza kujisahihisha na kukosoana kwa adabu na nidhamu, hivyo wanaCCM aliowalenga wanapaswa kuacha utoto.

"Hiki chama ni cha siasa za ukombozi na si za kipuuzi, haya ni majira ya uchaguzi na mtu wa kuchokozwa namba moja ni mkurugenzi wa uchaguzi ambaye ni mimi, sichokozeki na chini yangu kuna wakurugenzi wananisaidia, wasichokozeke," alisema.

"Bila CCM madhubuti nchi yetu itayumba, wapo watu wana uchuro, washindwe na walegee, wana uchuro eti CCM kimenuka vichwa vya habari vinatabiri kifo cha CCM, mpasuko wa CCM, kutumbulika kwa CCM, wapumbavu hao.

Alisema mtu yeyote mwenye akili timamu ambaye hajalewa kilevi chochote, iwe cha pombe au madaraka, hawezi kusema kwa namna yoyote ile CCM kimenuka.

"Msomi yeyote, mchambuzi, mwanasiasa makini, Mtanzania makini, hawezi akathubutu wala kuota kwamba chama hiki kwa historia yake, kwa itikadi na safu yake ya uongozi eti kinameguka, ndiyo maana natumia neno jepesi ni wapumbavu," alisema.

"Watu wanapoteza muda mitandaoni kumtukana Rais bila hata ubinadamu, mama yake yupo chini ya uangalizi maalum hasemi wala ali na wanajua kabisa, utu wetu umeenda wapi? Sisi watu wenye ndoa ambao tumefundishwa siri za ndoa, mkigombana mtu akibisha hodi mnatafuta tabasamu la kulazimisha.

"Ni mambo ya ndani sembuse mambo ya nchi, ukisikia mtu anasema mume wangu kikojozi ni dharau maana umesahau kiapo kwa padri ulisema utakuwa naye kwa mema na mabaya. Sasa bora angekuwa kikojozi lakini una mwongopea."

PINDA ANENA

Naye Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, alisema amefanya kazi na Rais Magufuli kwa muda mrefu, akisisitiza kuwa kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza.

"Huyu bwana ni chema kinachojiuza, ndani ya miaka mitatu ukitazama sifa kubwa imeenda kwa huyu jemedari, kwanini tumung'unye maneno? Ukweli ndio huo," alisema. Pinda alisema hayo maneno yanayosemwa ya mwaka 2020 kuwa kuna mtu atajitokeza, yasiwaumize kichwa wanaCCM kwa kuwa Rais Magufuli ana miaka mitano na ana miaka mingine mitano.

"Mimi nimefanya kazi na Baba wa Taifa miaka minane, (Ali Hassan) Mwinyi miaka 10, (Benjamin) Mkapa miaka 10 na nikapata nafasi ya kufanya kazi na (Jakaya) Kikwete miaka 10.

"Na mimi nimo nikisema anamaliza miaka yake 10, na wala sitashangaa akimaliza miaka yake 10 mkaanza kusema angeendelea, amefanya mambo makubwa kwa uaminifu mkubwa," alisema.

**MAKADA ARUSHA WAIBUKA**

Makada wa CCM mkoani Arusha, wamewataka Watanzania kujitokeza kumtia moyo na nguvu Rais John Magufuli ili asikatishwe tamaa na baadhi ya viongozi wa sasa na wastaafu.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM), Anna Msuya, alisema wamebaini kuna kikundi cha watu wachache ambacho kimejitokeza kwa lengo la kumkwamisha Rais Magufuli asiweze kutimiza malengo yake ya kuwatumikia Watanzania.

Alisema kuwa wanawake wa CCM mkoa wa Arusha wameandaa kongamano kubwa la kumpongeza Rais Magufuli litakalofanyika katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid Jumamosi ijayo.

"Rais Magufuli ameweza kuupatia mkoa wetu miradi mikubwa ukiwamo wa maji wenye kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 520 ambao utakapokamilika utakuwa umeweka historia kubwa na utatimiza kwa vitendo kaulimbiu ya kumtua mwanamke ndoo ya maji," aliongeza.

Kada wa chama hicho wilayani Arumeru, Ezekiel Mollel, alisema kuwa vijana wa chama hicho wilayani humo wapo tayari kusimama na Rais Magufuli kwa kila hatua na uamuzi atakaochukua ndani na nje ya chama hicho.

Mollel alikitaka chama hicho kuwachukulia hatua wanachama wake ambao alidai wameanza mikakati ya kukihujumu chama hicho.

Naye aliyewahi kuwa mgombea wa ubunge wa chama hicho katika Jimbo la Arusha Mjini, Dk. Godfrey Mollel, alisema wakati umefika kwa kila Mtanzania kunyanyuka na kumtetea Rais Magufuli kwa kazi kubwa anayofanya ya kusimamia maendeleo na kudhibiti uzembe serikalini.

HABARI KITAIFA

# Serikali yawakumbuka makandarasi wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itawajengea uwezo makandarasi wadogo wanaotumia teknolojia ya nguvukazi (Labor Based Technology) katika ujenzi na matengenezo ya barabara, madaraja na majengo.

Lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kuwa wanapata fursa zaidi za kushiriki na kushindana katika kazi zilizotengwa mahsusi kwa ajili makandarasi hao.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayeshughulikia Sekta ya Ujenzi, Elius Mwakalinga, alisema hayo jana kwenye kongamano la uhamasishaji na uanzishwaji wa umoja wa makandarasi na vikundi vinavyotumia teknolojia stahiki ya nguvu kazi katika ujenzi, ukarabati wa matengenezo ya barabara.

Mkutano huo uliofanyika katika Chuo cha Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi (ATTI) mjini hapa, ulihudhuriwa na zaidi ya makandarasi wadogo 150.

Mwakalinga alisema wizara kupitia taasisi zake zinazotekeleza miradi ya ujenzi, itaendelea kutumia sheria na kanuni zilizowekwa ili kuhakikisha kazi zilizoainishwa kwenye miradi ya ujenzi, ikiwamo ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na majengo zinafanywa na makandarasi hao.

**Mbali na kuongeza ajira na kuimarisha usafiri hususan maeneo ya vijijini, serikali inaelewa fika mnachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi kwa kodi mnayolipa kupitia kazi mnazozifanya.**

"Wizara imeteua timu ya wataalamu kupitia nyaraka mbalimbali za miradi ya ujenzi ili kuhakikisha asilimia 30 ya fedha zinazolipwa kwenye mikataba mbalimbali ya ujenzi zinaelekezwa kwa makandarasi wanaotumia teknolojia ya nguvu kazi," alisema Mwakalinga.

Aliongeza kuwa upitiaji utafanyika kwa haraka chini ya wataalamu hao na anaamini watafanya kazi hiyo vizuri ili kubainisha vigezo ambavyo makandarasi hao wamekuwa wakivilalamikia kila siku katika utekelezaji wa kazi zao ili vifanyiwe kazi.

Pia Mwakalinga alibainisha kuwa serikali inatambua makandarasi hao ni chachu kubwa katika kutatua tatizo la ajira kwa wananchi hususani maeneo ya vijijini kwa kuwa mara nyingi makandarasi hao hutumia vifaa na vibarua wanaopatikana katika eneo la mradi.

"Mbali na kuongeza ajira na kuimarisha usafiri hususan maeneo ya vijijini, serikali inaelewa fika mnachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi kwa kodi mnayolipa kupitia kazi mnazozifanya," alisisitiza Mwakalinga.

Alisema ni jukumu la makandarasi hao kushirikiana na kufanya kazi kwa pamoja na kuwa na sauti moja katika kufuatilia fursa mbalimbali na maslahi yao na kupata ufumbuzi wa pamoja wa changamoto zinazowakabili.

Akimkaribisha Katibu Mkuu huyo, Mkurugenzi wa Barabara, Mhandisi Rogatius Mativila, alisema madhumuni ya kikao kazi hicho ni kujadili kwa pamoja masuala muhimu katika sekta ya ujenzi ili kuendeleza na kuimarisha matumizi ya teknolojia ya nguvukazi katika kutekeleza matengenezo ya barabara, madaraja na majengo bila kusahau sekta nyingine nchini.

Akizungumza kwa niaba ya makandarasi hao, Aurelia Mtui, alitoa shukrani za dhati kwa serikali kwa kuwa amekuwa kwenye taaluma hiyo kwa miaka 18 na kwa mara ya kwanza wamekutana na Katibu Mkuu wa Sekta ya Ujenzi kuzungumzia changamoto zao na kuomba maazimio waliyokubaliana katika kikao hicho yafanyiwe kazi.

Serikali ilianzisha mpango wa kuendeleza matumizi ya teknolojia ya nguvukazi tangu mwaka 2004 na kulingana na takwimu zilizopo hadi Juni, mwaka huu, makandarasi 267 walikuwa wamesajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) katika madaraja ya kutumia teknolojia ya nguvukazi.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC) wa pili kushoto akiwa ameambatana na viongozi kadhaa wakikagua bwawa la tope sumu pamoja na Kaimu Meneja wa Mgodi wa Acacia North Mara, Ruben Ngusaro (wa kwanza kushoto), katika eneo la mgodi wa Acacia Nyamongo wilayani Tarime mkoani Mara. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Elimu kuhusu taa za kuongoza magari yatakiwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI, imesema kutokana na mji wa Kahama kuwa na taa za kuongoza magari barabarani, wananchi hawanabudi kubadilika na kufuata sheria na taratibu za usalama barabarani kama taa zinavyoowaongoza.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamringi Macha, aliyasema wakati akikagua taa za kuongeza magari na kuwasihi wananchi hasa madereva wa vyombo vya moto kufuata sheria ili kuepuka ajali.

Alisema Mji wa Kahama ni moja ya miji ambayo inakua kwa kasi kimaendeleo nchini, na kuongeza kuwa kuwapo kwa taa hizo kunaonyesha ni kiasi gani mji huo umekuwa na madereva wanatakiwa kubadilika.

Aidha, aliliagiza Jeshi la Polisi wilayani hapa kutoa elimu ya usalama barabarani, na matumizi sahihi ya taa za kuongoza magari, huku akisema hivi sasa ni sehemu mbili kati ya sehemu tano ambazo zitakuwa na taa hizo hivi karibuni.

Macha alisema magari yanaposimama, watembea kwa miguu wanatakiwa kupita, lakini imekuwa kinyume kwa kuwa watembea kwa miguu wanapita hata pale magari yanaporuhusiwa, hali ambayo ni hatari.

Pia, alisema askari wa usalama barabarani wanatakiwa kuchukua siku mbili hadi tatu kukaa katika alama hizo kutoa maelekezo kwa wananchi jinsi ya kusimama na kuvuka barabara ili waweze kufika upande wa pili salama.

Macha alisema, wananchi wamekuwa wakivuka kushoto na kulia bila kuangalia ni sehemu gani magari yanatokea, ingawa kuna taa za barabarani, hivyo kufanya usalama wao kuwa mdogo.

Pia aliwataka madereva wa vyomba vya moto kutunza miundombinu ya taa za barabarani na kuepuka kuzivunja kwa kuzigonga kwa uzembe, na kuongeza kuwa serikali imetuma fedha nyingi na kama zitaharibika mji utaendelea kama ilivyokuwa awali.

# DED akerwa kujirudia hoja Mdhibiti Mkaguzi Serikali

**Na Gurian Adolf,** NKASI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, imetakiwa kumiliki mali zake ili kuondokana na suala la kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambazo zimekuwa zikijirudia rudia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Missana Kwangula, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Baraza la Madiwani lililofanyika mjini hapa kwa ajili ya kuzipitia hoja za CAG.

Alisema halmashauri hiyo inamiliki mali mbalimbali yakiwamo majengo ya shule za msingi, sekondari na vituo vya afya yapatayo 200 lakini kati ya majengo hayo, 15 tu ndiyo yana hatimiliki.

Kwangula alisema hiyo imekuwa miongoni mwa hoja zinazotokea mara kwa mara pindi wanapotokea ripoti ya CAG, hivyo imefika wakati ni lazima hoja hiyo imalizwe.

Alisema haiwezekani baadhi ya hoja ziwe zinajirudia mara kwa mara, hivyo ni lazima zimalizwe kwa kuwa kitendo hicho kinaonekana kuna uzembe katika kushughulikia hoja hizo. Kutokana na hali hiyo, alisema lazima watendaji wabadilike na kuhakikisha wanazimaliza hoja hizo ili ziache kujirudia.

Kwa upande wake, Ofisa wa Serikali za Mitaa mkoani Rukwa, Albinus Mgonya, alisema ripoti ya CAG imetoa hoja 496 ambazo zinatakiwa kujibiwa, hivyo ni wajibu wao kuzitafutia majibu haraka.

# Madalali, wanunuzi wa madini wabanwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI mkoani Shinyanga imepiga marufuku madalali na wanunuzi wa madini ya dhahabu na almasi kuacha kufanyabiashara zao katika maeneo ambayo sio rasmi badala yake waende kwenye masoko yaliyotengwa na serikali.

Kwa wanunuzi wa madini ya dhahabu walioko Kahama na madalali wao wametakiwa kuhamia katika jengo rasmi lililotengwa na serikali kwa ajili ya kufanya biashara hizo kwani ofisini hizo ziko katika hatua za mwisho za ukamilishwaji.

Mhandisi Joseph Kumbulu, Ofisa Madini Mkoa wa Shinyanga, ndiye aliyetangaza marufuku hiyo wakati akizungumza na madalali na wanunuzi ambao wananunua dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo, na kusema jumla ya wanunuzi 10 wameshahamia kwenye soko lililotengwa na serikali.

**Nilikuwa niende Kakola tangu juzi kwani huko kuna mifuko zaidi ya 1,000 imekamatwa kwa watu wakitaka kuzitorosha, na kwa sasa nimeweka ulinzi wa Polisi kuhakikisha kuwa wanailinda mpaka nitakapofika na kujiridhisha uhalali wake.**

Alisema kwa Wilaya ya Kahama ofisi zimeshajengwa na kilichobaki ni Halmashauri ya Mji wa Kahama kuingia mikataba na wapangaji wake ambao ni wanunuzi wa madini kutoka kwa wachimbaji wadogo na madalali wa madini.

Aidha, Kumbuli aliwataka madalali wa madini kutokaa mjini na badala yake wanatakiwa kwenda kwenye maeneo ambayo yametengwa na serikali kulingana na mauzo ya dhahabu yaliyopo katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

Pia alisema ofisi ya madini haitawajibika kwa dalali yeyote ambaye atataka leseni katika eneo ambalo haliko rasmi na halitambuliki na serikali, huku akisisitiza kuwa zoezi la leseni litatolewa kulingana na makubaliano ya pande zote mbili.

Mhandisi Kumbulu alisema kwa mnunuzi atakayebainika kuuza madini nje ya soko la dhahabu linalotambulika kisheria, atalazimika kulipa faini ya gharama ya mzigo, kulipa kodi ya serikali pamoja na kutaifishwa mali zake.

"Kwa sasa serikali imesema kuwa atakayebainika kuuza madini hayo katika masoko ambayo sio rasmi atalipa gharama zote na faini za mgizo aliokamatwa nao na kutaifishwa mali zake zote atakazokuwa nazo," alisema Kumbulu.

Kumbulu aliongeza: "Nilikuwa niende Kakola tangu juzi kwani huko kuna mifuko zaidi ya 1,000 imekamatwa kwa watu wakitaka kuzitorosha, na kwa sasa nimeweka ulinzi wa Polisi kuhakikisha kuwa wanailinda mpaka nitakapofika na kujiridhisha uhalali wake."

Hivi karibuni, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, akishirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kahama pamoja na Ofisa Madini wa Mkoa wa Shinyanga, walifanya msako katika Kijiji cha Kakola na kubaini wanunuzi wengi wa dhahabu wakifanya biashara kwenye masoko ambayo hayako kisheria.



Wananchi wakiangalia ajali ya gari aina ya Toyota Rav 4, lililomshinda dereva wake na kuingia kwenye mtaro wa maji ya mvua katika Barabara ya Sam Nujoma, eneo la Mlimani City, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Wataka Magufuli aombewe

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

VIONGOZI wa dini wilayani Kalambo mkoani Rukwa, wamewaomba wananchi kumwombea Rais John Magufuli pamoja na serikali yake ili kuzikabili changamoto mbalimbali anazokutana nazo katika utekelezaji wa majukumu yake.

Ombi hilo walilitoa juzi katika Kata ya Lyowa wakati serikali ikitoa misaada kwa kaya 120 zilizobomolewa makazi yao wakati wa msimu wa mvua uliopita na kuwaacha katika wakati mgumu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti viongozi hao kutoka dini mbalimbali walisema wanaona na kutambua vema changamoto anazokutana nazo Rais Magufuli katika utekelezaji wa majukumu yake, ndiyo maana wanawaomba waumini wa dini zote kuzidisha maombi kwa Mwenyezi Mungu ili ampe nguvu ya kuzishinda changamoto hizo.

Mmoja wa wachungaji hao, Peter Sikale wa Kanisa la Tanzania Assembles of God (TAG), alisema kuwa Rais ana kazi kubwa ya kuiongoza Tanzania, ambayo ni moja ya nchi kubwa barani Afrika, hivyo anahitaji nguvu za Mungu na njia ya kuzipata hizo nguvu ni maombi ya wananchi.

Alisema hivi sasa serikali ya awamu ya tano imajitahidi sana kukabiliana na mambo yanayomchukiza Mungu kama vile ufisadi, wizi ulanguzi na mambo mbalimbali yaliyokuwa yakifanyika siku za nyuma, lakini kwa jitihada za Rais Magufuli mambo hayo yamepungua.

Sikale alisema anajua Rais Magufuli peke yake bila kumshirikisha Mungu hawezi kwani anaopambana nao ni kundi kubwa na baadhi yao waliwahi kushika nyadhifa kubwa.

Mmoja wa wananchi waliohudhuria shughuli hiyo, Monica Nakazwe, alisema Rais Magufuli asijihisi yuko peke yake kwani wananchi walio wengi wanamwombea kwa kuwa wanaona mambo yalivyobadilika hivi sasa.

Alisema wanafahamu kuwa anapigwa vita serikalini na katika chama, lakini asikate tamaa kwani atashinda na atambue kuwa hayo ni majaribu tu katika kutekeleza majukumu yake.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Julieth Binyura, aliwaasa wakazi wa kata hiyo kuhakikisha wanapanda miti kwani hakuna miti ya kutosha, ndiyo maana karibu kila masika mvua zinasababisha uharibifu wa makazi yao.

# Azania Benki yapiga jeki mkutano wa Alat mil. 40/-

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

BENKI ya Azania imekabidhi hundi ya Sh. milioni 40 kwa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (Alat) kwa ajili ya kufanikisha mkutano wa 35 wa jumuiya hiyo wa siku tatu ulioanza jana jijini Mwanza.

Akikabidhi hundi hiyo juzi Mkurugenzi Mtendaji wa Azania, Charles Itembe, alisema benki hiyo imeamua kuendeleza mapambano ya kusaidia upungufu wa fedha katika halmashauri ambazo zitatumika kupitia katika maendeleo ya jumuiya hiyo.

"Azania imeamua kufadhili mkutano huo wa Alat kwa kuwa wajumbe, viongozi na wanachama wake wapo chini ya Tamisemi, hivyo imani yetu fedha hizo zitakwenda kufanikisha malengo ya kutatua changamoto zilizopo kwa kila halmashauri nchini," alisema Itembe.

Itembe alisema benki ya Azania imewekeza katika sekta ya mikopo ya muda mfupi na mrefu kwa wateja wadogo na wa kati pamoja na kusaidia sekta za afya na elimu katika halmashauri mbalimbali nchini kwa kushirikiana na Alat na kutumia mfumo wa Tehama katika makusanyo ya mapato kwenye matawi yake.

Alisema ajenda kubwa kwa sasa katika taasisi mbalimbali nchini ni uchumi wa viwanda ili kuleta tija katika uwekezaji kwenye viwanda vidogo na wa kati, kuongeza uzalishaji wa uchumi, na kwamba benki hiyo pia imejikita katika uwekezaji kwenye sekta ya kilimo, mazao ya miwa, korosho, pamba na tumbaku.

Akipokea hundi hiyo, Mwenyekiti wa Taifa wa Alat, Gulamhafeez Mukadam, aliipongeza benki hiyo kwa kutoa mchango huo, na kuiomba mwaka ujao kuongeza na kufikia Sh. milioni 200 ili kutatua changamoto walizonazo wananchi na halmashauri zao kwa ujumla.

# DC Muro afagilia Chuo cha Uhasibu

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amefurahishwa na kazi zinazofanywa na Chuo cha Uhasibu Arusha na kukiomba kiendelee kuwaandaa vijana kitaaluma na kivitendo katika kuwawezesha kupambana na changamoto za soko la ajira.

Muro aliyasema hayo jana wakati akifunga maonyesho ya nadharia na vitendo ya kitaaluma, yaliyoshirikisha shule 18 za sekondari mkoani humo.

Alisema anakipongeza chuo hicho kwa kutoa elimu ambayo inasaidia vijana huku akiwataka kusoma kwa bidii na kuwa na ufaulu mzuri wa kuwawezesha kusonga mbele.

Kwa mujibu wa Muro, chuo hicho kimefanya ubunifu mkubwa wa kushirikisha vijana wa sekondari za mkoa wa Arusha, kuona kazi mbalimbali zinazofanywa na chuo hicho, kwa kuwa kufanya hivyo wanawaandaa vijana hao kwa ajili ya kujiunga na elimu ya vyuo vikuu kwa baadaye.

"Hapa kuna wanasayansi, uchumi, watu wa mapambo na upishi wa keki, hii yote ni lengo la chuo kuwawezesha vijana ili wakimaliza masomo wasitoke na elimu ya darasani tu, bali waende kuwa wajasiriamali na wamudu kuendesha maisha yao," alisema Muro.

Kwa upande wake, Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema chuo hicho kitaendelea kutoa elimu bora, ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na ujuzi wa kuendesha maisha yao baada ya masomo.

"Kila kozi anayosoma mwanafunzi anapewa kazi mbalimbali ili ajue kwa vitendo, kwani lengo letu ni kutoa wajasiriamali pia huko waendako wakaweze kupata ajira na kujiajiri, kwani soko la ajira kwa sasa ni changamoto kubwa," alisema Prof. Sedoyeka.

"Chuo chetu pia tunatoa ushauri wa masomo gani mwanafunzi achukue, ili aendane na soko la ajira, iwe anataka kuajiriwa au anataka kujiajiri, hivyo wazazi walete watoto wao wapatiwe ushauri mzuri," alifafanua Prof. Sedoyeka.

Mmoja ya mwanafunzi aliyeshiriki maonyesho hayo, Bundalla Bachia, alishukuru kwa kuweka maonyesho hayo, kwani yatawasaidia kuwapa fursa ya kujifunza kivitendo masomo wanayofundishwa darasani.

Alisema maonyesho hayo yamewatengenezea uzoefu na ujuzi, kwani wamekutana na wanachuo wanaosoma fani mbalimbali, hivyo wanatarajia kujiunga nazo mara baada ya kidato cha nne na hiyo imewapa hamasa ya kufikia elimu ya juu.



# Serikali yaridhishwa na utekelezaji mradi umeme

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KAMISHNA wa Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga, amesema ameridhishwa na utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa kituo cha kupooza umeme na njia ya kusafirishia umeme mkubwa wa msongo wa kilovoti (Kv) 400, kutoka mkoani Singida kuelekea Namanga, Arusha.

Akizungumza jana wakati wa kutembelea mradi huo mkoani hapa, Luoga alisema kazi inayofanywa na makandarasi hao inaridhisha kwa kuwa wanakwenda na mkataba.

Alisema hadi sasa utekelezaji umefikia asilimia 51 na kwamba mradi unatakiwa kukamilika na kukabidhiwa serikalini Aprili, 2020.

**Hadi sasa utekelezaji umefikia asilimia 51 na kwamba mradi unatakiwa kukamilika na kukabidhiwa serikalini Aprili, 2020.**

Aidha, alisema mradi huo ni wa kimkakati na kwamba umeanzia mkoani Arusha hadi nchini Kenya na utaunganisha nchi za Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika.

"Nchi ambazo zitapitiwa na mradi huu wa kimkakati ni Tanzania, Kenya, Ethiopia, Sudani, Misri, Zambia, Zimbabwe, Angola, Namibia, na Kongo. Ukikamilika utasaidia ongezeko la umeme hadi kufikia Kv 100,000 na kuimarisha upatikanaji wa huduma, kuongeza kipato kwa wananchi na serikali itaweza kuuza umeme nje ya nchi," alisema.

"Mwanzo tulikuwa tunazalisha umeme Kv 200, na baada ya kuongezeka kwa vyanzo vya umeme huduma ikaongezeka kufikia Kv 320, na mradi huu ukikamilika tutafikia kiwango cha Kv 400 ya uzalishaji wa umeme nchini," alisema Luoga.

Aidha, alisema mahitaji ya umeme ni 1,200 na kuna ziada ya Megavolts (Mv) 100-200, kwa siku kutokana na kukamilika kwa baadhi ya vyanzo vya upatikanaji wa huduma ya umeme.

Mratibu wa Mradi wa Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (Tanesco), Mhandisi Piter Kigadye, alisema wananchi zaidi ya vijiji 20, waliopitiwa na umeme wanatanufaika na huduma hiyo, kwa gharama nafuu ya Sh. 27,000.

Alisema mradi huo umepokelewa vizuri na wananchi kutokana na jitihada waliyofanya ya kutoa elimu ya umuhimu wa mradi huo kwa wananchi.

Naye, Kaimu Meneja wa Tanesco Mkoa wa Arusha, Mhandisi Donasiano Shamba, alisema mradi huo unatekelezwa kwa ubora na kwa wakati na kwamba wananchi watarajie huduma bora.

Kwa mujibu wa meneja huyo, mkoa wa Arusha ulikuwa unakabiliwa na ukosefu wa umeme na kwamba kukamilika kwa mradi kutapunguza na kufungua milango kwa wawekezaji kujenga viwanda kwa wingi.



Mkurugenzi wa Asasi ya Mirerani Mining Tourism, mkoani Manyara, Charles Mnyalu, akizungumza kwenye mafunzo ya wajasiriamali yaliyofanyika katika Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mil.100/- kugharamia miradi ya maendeleo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAASISI ya Chemchem Association imepanga kutumia zaidi ya Sh. milioni 100 mwaka huu, ili kuchangia miradi ya maendeleo katika eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori (Juhibu).

Juhibu ilianzishwa mwaka 2003 inaundwa na vijiji vya Sangawe, Mwada, Ngoley, Vilimavitatu, Minjingu, Kakoi, Olasiti, Manyara, Magala, na Maweni.

Ofisa Maendeleo ya Jamii ya Taasisi ya Chemchem Association, Walter Palangyo, alisema inachangia miradi hiyo kama sehemu ya wajibu wake kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii, mbali ya kodi na tozo nyingine zinazolipwa na Chemchem iliyowekeza shughuli za utalii katika hifadhi hiyo.

Alisema taasisi hiyo imekamilisha ukarabati wa majengo ya Shule ya Msingi Vilima Vitatu, ofisi mbili za walimu na sasa mradi wa ujenzi wa vyoo.

"Katika shule hii tumetumia kiasi cha Sh. milioni 50 ili kuhakikisha wanafunzi katika shule hii wanapata elimu bora katika mazingira mazuri, kwani tayari tumewapatia madawati 100 kwa ajili ya kumaliza tatizo katika shule hii," alisema.

Alisema taasisi hiyo pia imetoa Sh. milioni 5 ili kusaidia Vikoba katika baadhi ya vijiji katika eneo hilo, ikiwapo vikundi vya jamii ya Wabarbeig ili kuweza kuwa na miradi ya maendeleo.

"Kuna kikundi cha Wicheda na Datoga vya jamii ya Kibarbeig ambavyo tumewapatia kiasi cha Sh. milioni 2.5 ili kukuza mitaji yao. Pia kumeanzishwa mradi wa maboma ya asili, ambayo watalii wataweza kuwatembelea," alisema na kuongeza.

"Mwaka huu pia tunaendelea na mradi wa kusomesha watoto katika jamii hii, katika Chuo cha Wanyamapori cha Mweka na Chuo cha Ufundi (VETA) na wengine tumewalipia ada za shule ya sekondari," alisema.

Alisema pia kuna miradi ya maji, michezo na afya katika vijiji hivyo, hasa kutokana na fedha ambazo zinatokana na utalii.





# Mjane arejeshewa mali alizopokwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MJANE Renalda Maleo, mkazi wa Kata ya Kiomu katika Wilaya ya Moshi ambaye alikuwa amedhulumiwa shamba lenye ukubwa wa ekari 10 na ndugu wa familia ya mumewe, ameshinda kesi ya rufani iliyofunguliwa dhidi yake katika Baraza la Ardhi la Wilaya na kukabidhiwa mali yake.

Baraza la Ardhi la Wilaya ya Moshi ambalo lilisikiliza rufani hiyo chini ya Mwenyekiti wake, James Silas, limempa ushindi mjane huyo, baada ya kujiridhisha kwamba uamuzi wa awali uliotolewa na Baraza la Ardhi la Kata ya Kiomu ulikuwa sahihi.

Jana, Silas alithibitisha kuwa mlalamikaji huyo ameshinda kesi hiyo na kwa mujibu wa sheria, ndiye mmiliki halali wa shamba hilo.

Renalda aliachiwa shamba hilo na mume wake, Elinami Maleo, baada ya kufariki dunia, lakini mjomba wa mumuwe, Kennedy Anaseli, alimpokonya na kumtolea vitisho na kuanza kulimiliki kinyume cha utaratibu.

Baada ya ushindi huo, Renalda alisema ujasiri wa kufuatilia haki yake na kisha kumilikishwa kisheria, aliupata baada ya kukutanishwa na msaidizi wa kisheria Getrude Terry, ambaye alimshauri kuambatana naye na kufungua shauri hilo katika ngazi ya kata na akapata ushindi na baadaye akashinda tena katika Baraza la Ardhi la Wilaya.

**Nashukuru sana kwa kazi nzuri ya ushauri wa wasaidizi wa kisheria na ninaomba niwaambie kwamba nimeanza mchakato wa kutafuta hatimiliki na limeshapimwa.**

"Getrude alijitambulisha kwangu kuwa yeye ni msaidizi wa kisheria aliyepata mafunzo katika Shirika la Kwieco (Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organization). Baada ya hapo tulikwenda kufungua shauri na baada ya kusikilizwa pande zote, baraza liliona nina haki ya kumiliki shamba hii kwani ni mrithi halali wa mali ya marehemu mume wangu Elinami Maleo," alisema.

Kutokana na ushindi niliopata Baraza la Ardhi la Kata ya Kiomu, mlalamikiwa Kennedy hakuridhika na alikata rufani Baraza la Ardhi la Wilaya, tuliendelea na kesi hatimaye nilishinda tena.

"Nashukuru sana kwa kazi nzuri ya ushauri wa wasaidizi wa kisheria na ninaomba niwaambie kwamba nimeanza mchakato wa kutafuta hatimiliki na limeshapimwa. Kwa kifupi wameanza kwa kunipa hati ya kimila, hivyo sasa mimi ni mmiliki halali wa shamba hilo la ekari 10,"alisema.

Akizungumzia ushindi huo, Getrude Terry alisema halikuwa jambo rahisi kupambana kutetea haki ya mjane huyo lakini kwa kuwa anajielewa anapaswa kufanya nini kwa mujibu wa mipaka ya kisheria, Mungu alisimama katikati ya haki na dhuluma.

Kanuni ya 22 ya Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2018 na Sheria Namba 1 ya Mwaka 2017, ni wajibu wa mtoa huduma ya msaada wa kisheria kutoa huduma ya sheria kadri itakavyohitajika kwa mtu asiyekuwa na uwezo kama kumshauri mtu asiye na uwezo juu ya hatua zinazofaa na zitazochukuliwa kulingana na mazingira ya jambo husika.

Pia msaidizi huyo wa kisheria anapaswa kumwelekeza mtu asiye na uwezo juu ya mchakato na utaratibu wa kufikia haki, kumjulisha mtu asiyekuwa na uwezo juu ya hatua zinazoendelea katika kesi yake, kutoa ufafanuzi kwa mtu asiye na uwezo juu ya masuala ya kisheria na maamuzi yaliyofikiwa juu ya suala husika na kumtaarifu mtu asiye na uwezo juu ya utekelezaji wa hukumu.



Diwani wa Kata ya Kunduchi wilayani Kinondoni, jijini Dar es Salaam, Michael Urio (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kukagua mifereji ya maji ya mvua iliyojengwa na Kanisa la Mungu Baba Tegeta, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wazee wajitosa sakata la kina Makamba

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KUNDI la wazee wakiwamo baadhi ya viongozi wa mila wa mkoa wa Kilimanjaro, limejitosa katika sakata la makatibu wakuu wastaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na watu wengine mashuhuri kudaiwa kuandika waraka unaolenga kukivuruga chama hicho au kumkwamisha Rais John Magufuli.

Katika tamko lao lililotolewa jana na mwenyekiti wa wazee hao, Michael Mcha, wazee hao wanadai kuwa wanaoendesha harakati hizo wanafanya hayo wakitaka kulirejesha taifa mahali lilikotoka.

"Tunahuzunika kuona majaribio mapya ya kuturejesha tulikotoka yameanza. Kazi inayofanywa na Rais kwa Watanzania inaonekana ni dhahiri. Hatukutegemea wale walitufikisha hapa washangilie ila sisi tunataka wautumie uzee wao kulinda amani na utulivu wa nchi, hatutakubali kugawanywa kwa tamaa binafsi za watu," alisema Mcha.

Alisema jambo pekee wanalopaswa kufanya watu hao ni kumuacha Rais aendelee kuitibu nchi na kuwapigania wasiokuwa na sauti.

Miongoni mwa wazee walioeleza masikitiko yao ni Neema Kassa, mwasisi wa CCM ambaye alisema hao watu wanaompiga vita ni wale waroho wa madaraka, waliozoea kula kula, kunyonya na kwa kuwa sasa wanaona Rais Magufuli kafanya mambo mengi mazuri wanaona bora wampige vita, lakini wajue Mungu atawapiga wao vita mara 70.

"Labda kwa upeo wangu au labda kwa uzee wangu, niseme tu kwamba sisi wazee wa mkoa wa Kilimanjaro, tutapiga goti usiku na mchana, tutamwombea Magufuli, hao watu wanaompiga vita, watuachie Rais wa wanyonge, sisi tunampenda Magufuli kufa na kupona na tutaendelea kumwombea, misikitini tutaenda kumwomba huyu Mungu, makanisani tutaenda kumwita huyu Mungu, kumlinda Magufuli pande zote za dunia."

Naye Gabriel Mollel ambaye ni kiongozi wa mila (Legwanani) wa jamii ya wafugaji wa Kimasai kutoka Kata ya Kia, Wilaya ya Hai, alisema wanamuunga mkono Rais Magufuli kwa mambo mengi anayoyafanya na wanahakikishia Watanzania kuwa watamuunga mkono.

Kapteni mstaafu Haron Swai alisema tangu alipokuwa kijana wa Tanu Youth League, wakati wa Uhuru, anaweza kusema Rais Magufuli ameonyesha njia katika mambo mengi ya kupeleka taifa katika uchumi wa kati.

# Wachangishana mil.23.7/- kulipa deni la wazabuni

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

WANANCHI wa vijiji vya Katangara na Mrere katika Wilaya ya Rombo, wameridhia kuchangishana fedha zaidi ya Sh. milioni 23. 7 kwa ajili ya kulipa deni la wazabuni waliokopesha vifaa vya ujenzi wa maabara ya kisasa ya baiolojia na fizikia katika Shule ya Sekondari Mashati.

Kwa mujibu wa taarifa ya serikali iliyowekwa katika tovuti ya halmashauri hiyo, wananchi hao wamefikia uamuzi huo, baada ya wataalamu kutoka ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo kukutana na wananchi na kujadiliana namna ya kumaliza deni hilo ambalo limezua mgogoro kwa muda mrefu na kusababisha halmashauri hiyo kuburuzwa mahakamani.

Watumishi waliokwenda kukutana na wananchi hao ni Ofisa Mipango, Mkaguzi wa Ndani, Mwanasheria na Ofisa Elimu Sekondari na Bodi ya Shule ya Mashati.

Baada ya wananchi kusomewa taarifa kamili ya mradi huo pamoja na madeni ambayo mradi unadaiwa, waliridhia kulipa deni hilo kwa awamu, huku kila kaya ikipangiwa kuchangia Sh. 30,000.

Katika mkutano huo iliamuliwa kuwa, wataanza na zile kaya ambazo hazijachanga kabisa kwa uwiano wa Sh. 15,780,000 kwa wananchi wa kijiji cha Mrere na Sh. 8,000,000 kwa Kijiji cha Katangara ili kulipa deni lote ambalo mradi huo unadaiwa.

Mradi wa maabara ya Sekondari ya Mashati ni mradi ambao ulikataliwa kuzinduliwa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge mwaka jana kutokana na mzabuni kutokulipwa deni lake na kuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rombo kuhakikisha anamlipa mzabuni aliyetoa vifaa vya ujenzi huo.

Mzabuni huyo anadai kiasi cha Sh. milioni 22.744 ambapo kiasi cha Sh. milioni 10 kililipwa na halmashauri na kiasi kilichobaki kilitakiwa kulipwa kutokana na michango ya wananchi.

Hata hivyo, baada ya Ofisi ya Mkurugenzi kulipa kiasi kilichotakiwa kulipwa, bado upande wa wananchi hakuna malipo yoyote yaliyofanyika kitu ambacho kilisababisha mdai kurudi mahakamani ili kukazia hukumu amaliziwe deni lake lote.

Ukurasa 18



**Waziri mkimbizi wa Msumbiji kufia katika nchi ya Marekani?**

## UCHAMBUZI:

CUF ziarani kuhubiri sera yao mpya 'Furaha Haki kwa Wote'




Ukurasa 19

## Kimataifa



**Ruto, kinara Kenya 'anayeutesa' Urais**

Ukurasa 14


# siasa

JUMATANO JULAI 24, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




**Mwendesha mashtaka asulubiwa, kisa Rais Ramaphosa Afrika Kusini**

Ukurasa 17

## BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-6

PIUS Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia, Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mizizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa na leo hii tunaendelea kutokea tulipoishia wiki iliyopita. Endelea na sehemu hii ya sita ya kitabu hicho inayoanzia na Changamoto ya Kifedha.

**5.2.2 Changamoto ya Kifedha**

(a) Kukataa kwa Serikali ya Zanzibar kuunganisha Fedha zake za Kigeni na Tanzania Bara Wakati wa kuandaa bajeti ya mwaka wa fedha 1965/66, ambao ulikuwa ni wa kwanza baada ya Muungano, Waziri wa Fedha Amir Jamal alipata wazo la kwenda Zanzibar kumshauri Rais Karume akubali kuhifadhi fedha za kigeni za Zanzibar katika mfuko wa Serikali ya Muungano, ili kuongeza nguvu

Endelea 16



Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

**Bunge Marekani lachoshwa uswahiba wa Trump na mtawala wa Saudia**

Ukurasa 20

# Ruto, kinara Kenya 'anayeutesa' Urais

**Na Mashaka Mgeta**

ZINAPOTAJWA harakati za kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu wa Kenya, moja ya mataifa yaliyo wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), si rahisi kuliacha jina la William Samoei arap Ruto.

Ruto ambaye kwa sasa ni Makamu wa Rais katika Serikali inayoongozwa na Rais Uhuru Kenyatta, amekuwa katika siasa tangu utawala wa Rais Daniel Toroitich arap Moi, akitumikia zaidi katika jumuiya ya vijana ya kilichokuwa chama tawala cha Kenya African National Union (KANU).

Chama hicho kiliondoka madarakani baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2002 pale muungano wa National Alliance Rainbow Coalition (NARC) uliposhinda na mgombea urais wake, Mwai Kibaki kuibuka mshindi.

Katika uchaguzi huo, Kibaki alikuwa akishindana kwa karibu na aliyekuwa mgombea kupitia KANU, Uhuru Kenyatta ambaye Rais wa wakati huo, Moi, alimtaja kuwa chaguo lake pekee katika 'kumrithi.

Kama walivyo wanasiasa wengi wa Kenya, Ruto hajakulia kisiasa katika chama kimoja. Amekuwa akihama kutoka upande mmoja kwenda mwingine, ili mradi kumuunga mkono mmoja wa wagombea urais.

Lakini ushiriki wake mpana zaidi ulijitokeza katika Uchaguzi Mkuu wa 2007 alipokuwa katika muungano wa Orange for Democratic Movement (ODM) ulioongozwa na kinara wa siasa za upinzani wa Kenya, Raila Odinga.

Ruto alikuwa na jukumu kubwa la kuhakikisha ODM inapata kura nyingi katika ukanda wa bonde la ufa, wakati huo akiwa Mbunge wa Eldoret Kaskazini.

Katika uchaguzi huo, matokeo tata ya kura za urais yalitangazwa na mshindi akatangazwa kuwa ni Rais aliyekuwa anamaliza muhula wake wa kwanza, Kibaki.


Hata hivyo, upinzani na jumuiya za kimataifa zilipinga kutangazwa kwa Kibaki, hali iliyoibua machafuko yaliyosababisha vifo vya watu zaidi ya 1000, uharibifu wa mali na wengine kadhaa kuwa wakimbizi wa ndani ama nje ya nchi hiyo.

Hali hiyo haikumkosa Ruto ambaye alishukiwa kuwaunga mkono watu wa jamii zinazoishi ukanda wa bonde la ufa hususani Wakelenjing anapotokea, waliowajeruhi na kuwaua raia wengine hasa kutoka jamii ya Wakikuyu anapotoka Kibaki.

Katika mwendelezo wa 'siasa za kuhama-hama', wakati vurugu hizo zikitokea, Kenyatta aliyeshindana na Kibaki mwaka 2002, alikuwa akimuunga mkono (Kibaki) katika uchaguzi uliokosolewa na kuibua machafuko nchini humo.

Kama ilivyokuwa kwa Ruto, Kenyatta naye alishukiwa kuwaunga mkono watu wa jamii za ukanda wa kati na eneo la mlima Kenya hasa Wakikuyu, kuwajeruhi na kuwaua raia wengine hasa wanaotoka ukanda wa bonde wa ufa wakiwamo Wakalenjing.

Wote wawili, wakajikuta wanatajwa katika mashitaka yaliyofunguliwa kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Makosa Uhalifu dhidi ya Ubinadamu (ICC) iliyopo Uholanzi.



Naibu Rais wa Kenya, William Samoei arap Ruto.**PICHA: MTANDAO**

**UTAYARI WAKE**

Ruto ameshatamka kwamba yupo tayari kushiriki kinyang'anyiro cha urais mwaka 2022, ikiwa ni pamoja na uhakika wa kutumia rasilimali zote zinazohitajika.

"Shughuli za kesho zinapangwa leo," amekuwa akisema Ruto akisisitiza namna alivyojiandaa kwa ajili ya uchaguzi huo.

Nia ya Ruto kutaka kuwania urais iliibua hisia za kutoelewana kati yake na Rais Kenyatta ambaye ushindi wake katika awamu mbili ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na ushiriki wa Ruto anasadikiwa kuungwa mkono na jamii pana ya ukanda wa bonde la ufa na Magharibi mwa Kenya.

**KENYATTA NA ODINGA**

Kitendo cha kushikana mkono kwa Rais Kenyatta na Odinga Machi 9, mwaka jana, kililenga kupunguza joto la siasa za chuki kati ya watawala na upinzani, lakini kikajenga tafsiri ya kiongozi wa Kenya kumtosa Makamu wake, Ruto na kumuunga mkono kinara wa upinzani (Odinga).

Licha ya hali hiyo, kushikana mkono huko kulikigawa chama tawala cha Jubilee, kundi moja likitambulika kama Kieleweke na jingine Tanga Tanga.

**MISUKUSUKO**

Ruto amepitia misukosuko mingi ya kisiasa, kwa sehemu kubwa ikihusishwa na kashfa kadhaa.

Hata hivyo mashinikizo mengi yametokana na ushiriki wa washirika wake kadhaa kutajwa ama kushukiwa kushiriki vitendo vinavyohujumu uchumi wa taifa hilo ama kukiuka maadili ya utumishi wa umma.

Hivi sasa kuna shinikizo la kumtaka ajiuzulu nafasi yake kwa kile kinachoelezwa kuwa ni kuhusishwa katika kashfa iliyosababisha kukamatwa kwa maofisa wa Hazina kwa matumizi mabaya ya fedha za miradi ya mabwawa ya Arror na Kimwarer.

Baadhi ya wanasiasa akiwamo Mbunge wa Suba Kusini, John Mbadi, wamemtaka Ruto na Kiongozi Maseneta walio wengi, Kipchumba Murkomen kujizulu nyadhifa zao kutokana na kashfa hiyo iliyosababisha upotevu wa mabilioni ya fedha za walipa kodi.

> Hata hivyo, upinzani na jumuiya za kimataifa zilipinga kutangazwa kwa Kibaki, hali iliyoibua machafuko yaliyosababisha vifo vya watu zaidi ya 1000, uharibifu wa mali na wengine kadhaa kuwa wakimbizi wa ndani ama nje ya nchi hiyo.

**MABADILIKO YA KATIBA**

Wakati joto la Uchaguzi Mkuu wa 2022 likizidi kupanda, hoja ya mabadiliko ya Katiba nayo inaendelea nchini humo na kuzidi kuibua hisia tofauti na mgawanyiko.

Kwa upande wake, Ruto anaamini kwamba Kenya haihitaji mabadiliko ya Katiba kuzishinda changamoto zinazoikabili Serikali yake.

Badala yake, anasema Wakenya wanapaswa kulitumia Bunge kuanzisha ofisi za kambi rasmi ya upinzani ili itekeleze wajibu wake ipasavyo.

"Tunahitaji upinzani imara kuliko kitu chochote katika Kenya kwa sasa. Viongozi wa upinzani 'wapo wapo' kwa sababu hawakuingia bungeni ama kwenye ofisi yoyote ya umma," anasema Ruto.

Anasema wanaotaka kuwapo mabadiliko ya Katiba wanapaswa kujitokeza kwa Wakenya na kuwaelezea mapendekezo yao.

"Nikiwa Makamu wa Rais, nipo 'bize' kumsaidia Rais kusukuma mbele ajenda za maendeleo," anasema Ruto akisisitiza kutotambua umuhimu wa mabadiliko ya Katiba ili kuzikabili changamoto mbalimbali nchini humo.

**UHUSIANO WAKE NA KENYATTA**

Licha ya kuwapo ishara nyingi za kuyumba kwa uhusiano wake na Rais Kenyatta, Ruto anakanusha kwamba hali hiyo haipo.

"Tunashirikiana vizuri sana mimi na Rais Kenyata. Uhusiano wetu upo kwa muda mrefu sana. Tuna dira moja ya umoja, We share a vision of unity, mafanikio na mambo mema kwa Wakenya wote," anasema wakati akihojiwa na kituo cha runinga cha K24 cha nchini humo.

**HISTORIA YAKE**

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa Ruto amewahi kushika nyadhifa tofauti zikiwamo Waziri wa Kilimo (2008) na Makamu wa Rais tangu mwaka 2013.

Alizaliwa Desemba 21, 1966 huko Kamagut. Ameona mke mmoja,

Rachel Ruto mwenye watoto, Nick Ruto na Abby Cherop Ruto.

Kwa namna iwayo yote, historia ya Ruto katika kushiriki kampeni za urais umesaidia kwa kiasi kikubwa kuwaingiza madarakani marais karibu wa awamu zote, isipokuwa marehemu Jomo Kenyatta.

Kwa hali hiyo, Wakenya na maeneo ya dunia wanatarajia kumuona Ruto katika Uchaguzi Mkuu ujao akiwania urais badala ya kuwa 'msindikizaji' wa wagombea urais.

Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi wake anapatikana kupitia simu namba +255754691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.

UCHAMBUZI



Rais John Magufuli (katikati waliokaa) akiwa na viongozi wengine wa mihimili ya dola, Spika Job Ndugai (wa pili kulia) na Jaji Mkuu wa Tanzania Prof. Ibrahim Juma (wa tatu kushoto). Wengine ni Makamu wa Rais, Samia Suluhu (wa tatu kulia) na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ( wa pili kushoto). **PICHA: MTANDAO**

# Utashi wa kisiasa unavyoleta matokeo vita dhidi ya rushwa

**Na Reubeni Lumbagala**

RUSHWA ni tatizo linalokabili nchi nyingi duniani na kuleta athari hasi katika nyanja zote za maisha yaani kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mikakati na mipango mbalimbali inawekwa na nchi mbalimbali katika kuhakikisha tatizo la rushwa linapungua kama si kulimalizika kabisa ili kuleta tija na ustawi wa maendeleo.

Tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, vita na mapambano dhidi ya rushwa imeonyesha mafanikio makubwa kutokana na ukweli kuwa mafanikio ya mapambano ya rushwa yanahitaji sana utashi wa kisiasa.

Hili ni jambo linalodhihirishwa pasi na shaka na utendaji kazi wa Rais wa John Pombe Magufuli na Serikali yake.

Rais Magufuli amekuwa kinara wa kupiga vita rushwa kutokana na namna jitihada za kimaendeleo zinavyoweza kuathiriwa na rushwa kama ikiachwa itamalaki pasipo kudhibitiwa haraka iwezekanavyo.

Jitihada za Serikali za kukusanya kodi kwa maendeleo, kuwekeza fedha katika utekelezaji wa miradi mikubwa na midogo ya kimaendeleo, uboreshaji wa huduma bora za kijamii kwa wananchi, suala la utoaji ajira kwa vijana; haya na mengine mengi hayawezi kufanikiwa bila kudhibiti rushwa nchini.

Na kwa kutambua hilo, ndiyo maana Rais Magufuli na Serikali yake kwa ujumla imejizatiti katika kuhakikisha inakomesha vitendo vya rushwa ili kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo iweze kufanikiwa.

Utashi wa kisiasa katika mapambano ya rushwa umeonyeshwa na viongozi wa Awamu ya Tano.

Kutokana na nia ya dhati ya viongozi katika kukomesha rushwa, mafanikio yameonekana, ambapo kwa nchi sita za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Tanzania inashika nafasi ya pili ikitanguliwa na Rwanda katika mafanikio ya mapambano dhidi ya rushwa.

Juhudi zaidi zinaendelea kufanywa kupitia elimu kwa umma inayotolewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), taasisi nyingine za Serikali na asasi za kiraia katika kutokomeza rushwa ili Tanzania ishike nafasi ya kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla kwa mafanikio ya mapambano dhidi ya rushwa.

Taasisi ya Transparency International (TI) imeitaja Tanzania kuwa miongoni mwa nchi ambazo zinafanya vizuri katika mapambano ya kupinga rushwa kubwa na ndogo ambazo ni adui wa uhujumu uchumi na kuathiri ustawi wa maisha bora ya wananchi.

**RIPOTI**

Kwa mujibu wa ripoti ya Taasisi hiyo, Ofisi ya Rais na Waziri Mkuu, rushwa imepungua kutoka asilimia 15 hadi nne, na kwa wabunge kutoka asilimia 21 hadi nane.

Mafanikio haya ni zao la utashi wa kisiasa katika kuhakikisha rushwa inakwisha kabisa nchini, kwani Tanzania bila rushwa inawezekana.

Sambamba na hilo, Serikali imefanya kazi kubwa ya kuminya mianya ya rushwa kwa kuweka mazingira ya uwazi katika uendeshaji wa shughuli zake.

Uwazi umedhibiti njia za panya ambazo zilikuwa zikitumiwa katika kufanya vitendo vya rushwa.

Pia kumekuwa na kasi kubwa ya kuwashughulikia wala rushwa wanaofikishwa katika vyombo vya sheria na hivyo kuwatia hofu wapenda rushwa kuachana na vitendo hivyo mara moja.

Mashauri ya watoa na wapokea rushwa yamekuwa yakifanyiwa kazi kwa haraka na kufikia utoaji wa hukumu wa mashauri hayo.

Aidha, uanzishaji wa Mahakama ya Mafisadi na Wahujumu Uchumi imekuwa chachu ya kuchagiza vita ya rushwa ambapo kwa sasa; si dagaa (mtoa rushwa ndogo) wala papa (mtoa rushwa kubwa), wote wanashughulikiwa kikamilifu kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mkazo wa mapambano dhidi ya rushwa utafanikisha juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika ujenzi wa viwanda ili kufikia uchumi wa kati mwaka 2025.

> Tanzania tuna nafasi nzuri ya kuendelea kufanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa kwa nchi za Afrika na hata kimataifa kwani tayari utashi wa kisiasa upo nchini katika kukomesha rushwa.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa, paliposhamiri rushwa, hata ukuaji wa uchumi hukwama.

Julai 11, 2019, katika ufunguzi wa Siku Maalum ya Mapambano dhidi ya Rushwa kwa nchi za Umoja wa Afrika, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro alisema zaidi ya Dola Trilioni 1.4 zinapotea kila mwaka kwa njia ya rushwa barani Afrika.

Hizi ni fedha nyingi ambazo nchi za Afrika zinapoteza, kwani zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo.

Wananchi waendelee kuwa mabalozi wa kupinga vitendo vya rushwa kwani ni adui wa haki na maendeleo.

Na pale wananchi wanapotakiwa kutoa ushirikiano katika kesi za rushwa watoe ushirikiano ili wahusika wa vitendo hivyo kuchukuliwe hatua za kisheria.

Tanzania tuna nafasi nzuri ya kuendelea kufanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa kwa nchi za Afrika na hata kimataifa kwani tayari utashi wa kisiasa upo nchini katika kukomesha rushwa.

Nitamatishe makala haya kwa kuwasihi wananchi kuwa mwezi Oktoba mwaka huu, upo uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ambapo wananchi watapaswa kutumia haki yao ya kisheria na kikatiba kuchagua viongozi watakaowaongoza kwa miaka mitano.

Wananchi wawakatae wagombea wote watakaotoa rushwa, kwani rushwa ni adui wa kupata viongozi na utawala bora. Tafakari.

Mwandishi wa Makala hii ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa na Mlezi wa Klabu ya Kupinga Rushwa katika shule hiyo.
**Maoni: (+255) 764 666349.**

UCHAMBUZI

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-6

Inatoka Uk. 13

ya mfuko huo. Kwa mujibu wa maelezo yake mwenyewe Waziri Jamal, siyo tu kwamba Rais Karume aliukataa ushauri huo, bali pia ulimkasirisha sana. Kwani aliuona kuwa ni njama ya Serikali ya Muungano ya kutaka kupora akiba ya Fedha za Kigeni za Zanzibar.

(b) Serikali ya Zanzibar kutokuchangia fedha za kuendesha Muungano Katika jitihada zake za kujaribu kutatua kero za Muungano, mnamo mwaka 1991 Seri kali ya Muungano iliunda 'Tume ya Shellukindo', ambayo ilipewa jukumu la kuchambua kero hizo na kutoa mapendekezo ya utatuzi wake. Katika Ripoti yake iliyotolewa mwaka 1992, Tume ya Shellukindo ilianisha kuwapo kwa tatizo la Zanzibar kutochangia fedha za kuendesha shughuli za Muungano toka ulipoasisiwa mwaka 1964. Ripoti hiyo ililitaja jambo hili kuwa ni kero kwa upande wa Tanzania Bara, kutokana na kubebeshwa mzigo huo peke yake.

(c) Kutokuwapo kwa uwazi wa Mapato na Matumizi ya fedha za Serikali ya Muungano Ripoti huyo ya Tume ya Shellukindo pia ilitaja madai ya Serikali ya Zanzibar ya kutoku wapo uwazi wa kuonesha mapato na matumizi halisi ya shughuli za Muungano, na Kwamba, hii ndiyo ilikuwa sababu ya kuifanya Serikali ya Zanzibar isiweze kuchangia fedha kwa shughuli za Muungano. Lakini, Ripoti ya Shellukindo ilianisha mambo mengi mengine ambayo yalikuwa ni kero za Muungano. Miongoni mwa yale yaliyoorodheshwa ni pamoja na makubwa yafuatayo:

Suala la mamlaka ya nchi, yaani 'sovereignty'

"Kuwapo kwa serikali ya Zanzibar (SMZ) yenye mamlaka kamili juu ya mambo yasiyokuwa ya Muungano, lakini, bila kuwa na sovereignty yake kumeleta hisia kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kweli ni serikali ya Tanzania Bara iliyovaa 'sovereignty' ya Jamhuri ya Muungano"

Suala la Ulinzi na Usalama:

"Kuwapo kwa utata wa mamlaka ya kuunda majeshi."

Suala la Uraia

"Kuwapo kwa sheria ya Mzanzibari (n. 5 ya 1985 inaleta utatanishi unaoifanya Tanzania ionekane kuwa ina raia wa aina mbili, yaani, Watanzania na Wazanzibari"

Mikopo na Biashara za Nje

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano inalalamika kwamba imekuwa ikidhamini mikopo ya Nje ya Serikali ya Mapinduzi na kulazimika kuihudumia bila kuhusisha fedha za kigeni za Zanzibar; na kwamba, serikali ya Zanzibar huwa hairejeshi madeni yake kwa wakati na hivyo kusababisha serikali ya Jamhuri ya Muungano kulazimika kulipa madeni hayo pamoja na riba; wakati

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalalamikia suala la mikopo kuwa ni la Muungano, kwani linainyima Zanzibar uhuru wa kukopa kutoka nchi za nje na hivyo kushindwa kuendeleza miradi yake na kukimu mahitaji ya wananchi wa Zanzibar."

> "Serikali ya Jamhuri ya Muungano inalalamika kwamba imekuwa ikidhamini mikopo ya Nje ya Serikali ya Mapinduzi na kulazimika kuihudumia bila kuhusisha fedha za kigeni za Zanzibar; na kwamba, serikali ya Zanzibar huwa hairejeshi madeni yake kwa wakati na hivyo kusababisha serikali ya Jamhuri ya Muungano kulazimika kulipa madeni hayo pamoja na riba




Mwalimu Julius Nyerere (katikati) akichanganya mchango wa Tanganyika na Zanzibar, kuashiria Muungano wa nchi hizo mbili na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**5.2.3 Changamoto za maadui wa Muungano**

Masimulizi ya Sheikh Thabit Kombo

Kitabu kinachoitwa Masimulizi ya Sheikh Thabit Kombo ( Dar es Salaam University Press, 1996), kinaeleza kisa kimoja cha uzushi na uwongo kilichosukwa na viongozi fulani wa Zanzibar, ambacho kilitishia kuvunjika Muungano wetu.

Kitabu hicho kinasimulia jinsi mnamo mwaka 1965, viongozi fulani wa Zanzibar waliwafukuza watumishi wa umma waliokuwa wamehamishiwa huko kufanya kazi za Muungano. Watumishi hao walielezwa kwamba, hawatakiwi kuwapo Zanzibar kwa kuwa Muungano wenyewe pia, hautakiwi. Watumishi hao walikimbia kurudi Dar es Salaam, ambapo walikwenda kutoa taarifa ya kufukuzwa kwao kwa Waziri Oscar Kambona wa Mambo ya Nje, na kwa Abdallah Kassim Hanga, Waziri wa Mambo ya Muungano.

Mawaziri hao wawili walifikisha taarifa hiyo haraka kwa Rais Nyerere, wakaipamba kwamba, Rais Karume amefukuza watumishi waliotoka Bara, eti kwa sababu hapendi Muungano. Kwa mshangao uliochanganyika na hasira, Rais Nyerere aliitisha kikao cha dharura cha Baraza la Mawaziri kwa nia ya kuliarifu kwamba, amepata ushahidi wa kuaminika unaothibitisha kuwa, Rais Karume hapendi Muungano. Baada ya kuwaarifu Mawaziri kuhusu taarifa alizokuwa amepewa na Kambona na Hanga, alimalizia kwa kutoa kauli kwamba, kwa kuwa, huu ni Muungano wa hiari, hawezi kumlazimisha Karume kubaki ndani yake. Kwa hiyo, akawaarifu Mawaziri hao kwamba, wajiandae kusikia tangazo la kuvunjika kwa Muungano muda wowote kuanzia hapo.

Bahati njema, baadhi ya Mawaziri hawakuamini kuwa Rais Karume angeweza kweli kufanya hivyo, kwa hiyo, wakashauri upelekwe ujumbe kwa Rais Karume mwenyewe ili kupata uhakika wa jambo hilo. Papohapo ujumbe wa viongozi wawili, Rashid Kawawa na Thabit Kombo, ulipelekwa Zanzibar kwa madhumuni hayo. Ujumbe huo uliporejea ulitoa taarifa kwamba, Rais Karume alikuwa amesingiziwa, na wala hakuwa na habari ya kufukuzwa kwa watumishi hao! Majibu hayo yalimpa faraja kubwa Rais Nyerere, kwani yalimfanya atambue kwamba, kumbe hizo zilikuwa njama tu zilizotengenezwa na maadui wa Muungano. Kwa hiyo, akaachana na lile wazo lililokuwa limeamujia la kutangaza kuvunjika kwa Muungano.

**5.2.4 Changamoto za Kikatiba**

Madai ya Zanzibar kwamba, 'Tanganyika imevaa koti la Muungano,' tumekwishaona kuwa, Tume ya Warioba imelitaja jambo hili, na kueleza kuwa ndilo limeshika nafasi kubwa miongoni mwa kero zinazotolewa na upande wa Zanzibar.

Lalamiko lenyewe ni kwamba, Serikali ya Tanganyika ilijigeuza kuwa ndiyo Serikali ya Muungano, kwahiyo, imekuwa inafaidi peke yake misaada na fursa nyingine zote zinazotolewa kwa nchi nzima kwa jina la Muungano.

(a)....Uchambuzi

Uchambuzi wangu kuhusu suala hili unaonesha kwamba, kwa sehemu kubwa, madai haya yanatokana na tofauti ya uelewa juu ya dhana ile aliyoeleza Mwalimu Nyerere ambayo nimeinukuu hapo juu, kwamba, katika hali ya kawaida, "nchi inayoingia katika Muungano hujivua madaraka yake yote na kuyakabidhi kwa Serikali ya Muungano." Tafsiri sahihi ya maneno hayo ni kwamba, wakati Tanganyika ilipoingia kwenye Muungano huu, ilijivua madaraka yake yote na kuyakabidhi kwa Serikali ya Muungano. Zanzibar haikukabidhi madaraka yake yote kwa Serikali ya Muungano, kutokana na sababu alizozieleza za hofu ya kuonekana kuwa Zanzibar imemezwa na Tanganyika.

Kwa kuzingatia dhana hiyo, Hoja ya "Tanganyika kuvaa koti la Muungano" itakuwa imetokana na uelewa tofauti, unaosababisha kuwapo kwa tafsiri ambayo pia, ni tofauti, ya kwamba maneno hayo 'Tanganyika kujivua madaraka yake yote na kuyakabidhi kwa Serikali ya Muungano,' maana yake ni 'Tanganyika kuvaa koti la Muungano!'

(b)...Tanganyika ilijivua madaraka yake yote kwa kutumia sheria

Ni kweli kabisa kwamba, Tanganyika ilijivua madaraka yake yote, tena kwa kutumia sheria, na kuyakabidhi kwa Serikali ya Muungano. Hayo yalifanyika kwa mujibu wa sheria zifuatazo:

The Transitional Provisions Decree, 1964, ya tarehe 1 Mei 1964, na

The Transitional Provisions (No. 2) Decree, 1964, ya tarehe 15 Juni, 1964.

Sheria hizo mbili zilitungwa mahsusi kwa madhumuni ya kuifuta rasmi Serikali ya Tanganyika, na kukabidhi madaraka yake yote kwa Serikali ya Muungano; ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa dhana hiyo.

(c)...Changamoto za utata wa tafsiri ya sheria hizo

Sheria hizo zinaweza kutafsiriwa kwa namna mbili tofauti. Tafsiri moja ni kwamba, Serikali ya Tanganyika ilijivua madaraka yake yote ya kisheria na kuyakabidhi kwa Serikali ya Muungano. Ndiyo sababu serikali ya Tanganyika ilitoweka. Hiyo ndiyo tafsiri iliyotolewa na Mwalimu Nyerere. Lakini, tafsiri nyingine ni kwamba, sheria hizo ziliifanya Tanganyika ikawa ndiyo Jamhuri ya Muungano. Hiyo ndiyo tafsiri inayotolewa na baadhi ya Wazanzibari, ambao wanasema kwamba, 'Tanganyika ilivaa koti la Muungano.'

Kwahiyo, inategemea uamuzi wa mtu kuhusu tafsiri ipi anayoitumia katika kujenga hoja.

Maudhui ya sheria hizo ni kama ifuatavyo:

The Transitional Provisions Decree, 1964. Published on 1st May, 1964

Sheria hii ilibadilisha watu wote ambao walikuwa ni watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Tanganyika, wakawa moja kwa moja ni watumishi wa Serikali ya Muungano. Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Tanganyika ilibadilishwa kuwa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano. Nembo (public seal) ya Jamhuri ya Tanganyika ilibadilishwa kuwa ndiyo nembo ya Jamhuri ya Muungano.

The Transitional Provisions (no 2) Decree. Published on 15th June, 1964.

Sheria hii iliagiza kama ifuatavyo:

Kwamba, mahali popote katika sheria zilizopo ambapo neno 'Tanganyika' linaonekana, neno hilo lifutwe, na badala yake liwekwe neno 'Jamhuri ya Muungano.'

Kwamba, mahali popote katika sheria zilizopo ambapo maneno 'Serikali ya Tanganyika' yanaonekana, au ambapo kuna kitu chochote kinachotajwa kuwa ni mali yake au kinahusiana kwa namna yoyote na Serikali ya Tanganyika, basi, ichukuliwe kwamba mali hiyo au kitu hicho ni mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**ITAENDELEA WIKI IJAYO**



Mwendesha Mashitaka nchini Afrika Kusini, Busisiwe Mkhwebane. **PICHA: MTANDAO**

## Mwendesha mashtaka asulubiwa, kisa Rais Ramaphosa Afrika Kusini

MAHAKAMA ya Katiba nchini Afrika Kusini, imetoa uamuzi wake kwamba Mwendesha Mashitaka aliyemtuhumu Rais Cyril Ramaphosa kwa kuwa na uongozi mbaya, alichukua hatua hiyo akiwa na nia mbaya dhidi ya rais huyo.

Uamuzi huo unaweza kutilia mashaka uaminifu wa Mwendesha Mashitaka Busisiwe Mkhwebane, aliyekuwa akichunguza kisa cha kuchochea uchumi kilichofanyika wakati wa enzi za ubaguzi wa rangi.

Kwa sasa Mkwebane anajitayarisha kwenda mahakamani dhidi ya Rais Ramaphosa na Waziri wa Biashara Pravin Gordhan, ambaye ni mshirika muhimu wa rais.

Mahakama ya Katiba imesema Mkhwebane hakuwa muwazi kuhusu shughuli zake wakati wa uchunguzi.

Mahakama hiyo sasa imethibitisha adhabu dhidi ya Mkhwebane iliyotolewa na Mahakama ya Juu mwaka jana kwa kutumia njia zisizo sawa katika uchunguzi alioufanya mwaka 2017.

Benki ya Akiba ya Afrika Kusini ilipinga mapendekezo aliyoyatoa Mkhwebane katika kesi hiyo, na kutaka madaraka yake yabadilishwe kama hatua za mara moja zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake na pia alitakiwa kulipia gharama za kisheria.

Hata hivyo, Mwendesha Mashitaka huyo amesema ni lazima auangalie uamuzi kwa makini kabla ya kuzungumza chochote.

ASHUTUMIWA KUUNGANA NA ZUMA

Kabla ya uamuzi huo wa Mahakama, Rais Ramaphosa alisema atamfikisha mahakamani Mkwebane kupinga matokeo ya uchunguzi wake dhidi yake, kwamba alilipotosha Bunge kuhusu mchango wake katika kampeni za urais za mwaka 2017 alipokuwa anawania uongozi wa chama tawala Afrika Kusini, ANC.

Wakati huo huo, wafuasi wa Rais Ramaphosa wanamshutumu Mkhwebane kwa kujiunga na vita vya chini kwa chini vya wale wanaomuunga mkono rais wa zamani, Jacob Zuma, madai ambayo anayakanusha vikali.

Uchunguzi mwingine wa hivi karibuni uliofanywa na Mkhwebane uligundua kuwa Waziri wa Biashara Pravin Gordhan alikiuka katiba kwa kuongeza madaraka yake wakati alipokuwa kamishna wa ushuru.

Gordhan, aliyewahi pia kuwa waziri wa fedha, anayakana matokeo ya uchunguzi huo.

Kwa sasa anasimamia juhudi za kufufua kampuni kadhaa za Serikali kama shirika kubwa la umeme nchini Afrika Kusini, Eskom, na kampuni ya kutengeneza silaha ya Denel. **DW**

# Waziri mkimbizi wa Msumbiji kufia katika nchi ya Marekani?

**Na Ani Jozeni**



Aliyekuwa Waziri wa zamani wa Fedha wa Msumbiji, Manuel Chang (aliyekaa) akiwa kizimbani nchini Afrika Kusini. **PICHA: MTANDAO**

MAHAKAMA nchini Afrika Kusini imebadili upepo kwa aliyekuwa Waziri wa Fedha wa Msumbiji, Manuel Chang ambaye anatakiwa nchini Marekani kujibu mashtaka ya rushwa na ubadhirifu ya kutumia misaada kutoka nje.

Inafuatia Mahakama moja kufikia uamuzi elekezi kuwa waziri huyo wa zamani arudishwe Msumbiji baada ya serikali ya nchi hiyo kutoa ombi hilo, wakati awali haikuwa imefanya lolote kuhusu mtuhumiwa huyo kwa miaka kadhaa tangu aondolewe katika wadhifa huo na kuanza kuishi nje.

Wanaharakati wana shauku kubwa kuwa waziri huyo ahamishiwe Marekani ambako atashtakiwa, na si Msumbiji.

Waziri mpya wa Sheria nchini humo, Ronald Lamola amesifiwa kwa kuonyesha kujali utawala wa sheria badala ya kuendelea kujali mshikamano kati vya vyama vya ukombozi Kusini mwa Afrika kama ambavyo wengi wamezoea.

Chang sasa anakabiliwa na uwezekano mkubwa wa kuhamishiwa Marekani ambako anatakiwa kujibu mashtaka kuhusu rushwa katika mradi wa mkopo wa euro bilioni mbili kuunda meli za uvuvi na doria kutumiwa na serikali ya Msumbiji.

Inasemekana kuwa alipokea milingula ya mamilioni ya dola (za Marekani) katika mradi huo ambako wawekezaji kadhaa wa kimataifa pia walipoteza fedha zao.

Chang alikamatwa Desemba 29 mwaka jana akiwa katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Oliver Tambo jijini Johannesburg, nchini Afrika ya Kusini kwa kibali cha Interpol kufuatia ombi la Marekani.

Kilichothibitishwa na Mahakama moja jijini hapo. Mwezi Januari ombi likatolewa na Marekani kuwa waziri huyo wa zamani ahamishiwe Marekani kujibu mashtaka, pamoja na maofisa wengine wa kampuni za meli na benki wanaotuhumiwa pia katika kesi hiyo.

Ndiyo hapo Serikali ya Msumbiji ikatayarisha ombi kwa waziri mkimbizi huyo kurudishwa nyumbani eti ili afunguliwe mashtaka, wanaharakati Afrika Kusini wakipinga mwelekeo huo.

Mwezi Aprili Mahakama moja eneo la Kempton jijini humo ikafikia hukumu elekezi kuwa Chang anaweza kisheria kuhamishiwa Msumbiji au Marekani, halafu mwezi Mei waziri Michael Masutha aliyemtangulia Lamola akaamua kumhamishia Chang nchini Msumbiji kwa msingi kuwa makosa yanayomhusu yalifanyika nchini humo na hivyo ndiyo mahali ambako mashtaka yanahitaji kufunguliwa.

Kundi la wanaharakati nchini Msumbiji, Forum de Monitoria do Orcamento (FMO) likawakilisha ombi mahakamani kupangua uamuzi wa waziri huyo, kwa msingi kuwa hapakuwa na uhakika wowote kuwa Chang atashtakiwa.

Siku moja kabla ya Masutha kufanya uamuzi huo, wakili na profesa wa sheria za kimataifa wa Chuo Kikuu cha Afrika Kusini huko Pretoria, akaandika katika jarida moja mtandaoni kuwa Mamlaka ya Mashtaka (NPA) ya Afrika Kusini ilikuwa imekubali kwa kuelewana maelezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Msumbiji kuwa kinga ya kutoshtakiwa ya Chang ilikuwa imeondolewa.

Kwa maana hiyo akirudishwa Msumbiji angeshtakiwa, maelezo ambayo yalikubaliwa na hakimu mkazi Mahakama ya Kempton kuwa Chang ahamishiwe Msumbiji.

Hata hivyo, taarifa zinasema kuwa Bunge la Msumbiji liliondoa kutokamatwa na kuhojiwa na polisi kwa waziri huyo mkimbizi, na siyo kinga ya kukamatwa na kushtakiwa kuondolewa.

Mamlaka zinadai uchunguzi unaendelea, miaka mitano.

Jambo la kushangaza ni kuwa katika uamuzi wake kufuta msimamo wa mtangulizi wake, Lamola hakutumia vielelezo vya mikataba ya kimataifa au kupelekeana watuhumiwa kati ya Afrika Kusini na Marekani, n.k.

Julai 13, ofisi ya waziri huyo ilitoa tangazo kuwa imesimamisha mpango wa kumrudisha Chang nchini Msumbiji, inapinga ombi la waziri huyo mkimbizi la kupelekwa Msumbiji, na haitapinga ombi la wanaharakati wa Msumbiji kuwa asirudishwe nchini humo.

Taarifa hiyo ilisema kumhamishia Msumbiji kungekuwa kinyume cha katiba (ya Afrika Kusini) na kinyume cha sheria ya uhamishaji watuhumiwa ambayo pia inatambuliwa na nchi za ukanda wa SADC. Siyo sheria za Marekani.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa vipengele vya sheria na mikataba hiyo iliyokubaliwa na nchi za Kusini mwa Afrika, vinaruhusu mtuhumiwa kuhamishiwa nchi fulani kama hana kinga ya kushtakiwa kwa tuhuma zinazomkabili, na kama tayari mashtaka yalishafunguliwa kwa tuhuma husika.

Ina maana kuwa mikataba hiyo inapendelea kuwa mtuhumiwa ahamishiwe pale ambapo kuna uwezekano halisi wa kushtakiwa, wakati Msumbiji ilikuwa inatoa matamshi tata kuhusu waziri huyo mkimbizi kufunguliwa mashtaka.

Cha msingi ni kuwa miaka mitano baada ya matukio hayo vyombo vya sheria vya Msumbiji vilikuwa vinaendelea na kazi ya kuchunguza, hivyo siyo leo au kesho ambako mashtaka halisi yangefunguliwa.

Vuta nikuvute ya kisheria ilirindima nchini Afrika Kusini kuhusu suala hilo, na hakuna uhakika lilichangia kiasi gani kwa Rais Cyril Ramaphosa kubadilisha mshika kitengo hicho cha Sheria na Katiba, kama suala hilo lilichangia au imetokea tu kuwa mwelekeo umebadilika baada ya waziri mwingine kuingia ofisi hiyo.

Ila kwa sababu Rais Ramaphosa pia ana kampeni ngumu dhidi ya rushwa hasa katika utawala uliopita wa Jacob Zuma, kumwachia mtuhumiwa mkubwa kama Chang anayetafutwa kwa kesi ya kimataifa ingekuwa dosari ya kimkakati, kuwa ni mtu wa mapinduzi, si utawala wa sheria. Alichelea picha hiyo.

Isitoshe suala hilo lilidakwa kuwa la uchambuzi halisi wa sheria za kimataifa na jinsi Afrika Kusini inavyozisimamia, hali iliyotoa nafasi kwa nchi hiyo kubadili taswira iliyojitokeza wakati serikali ya Afrika Kusini ilipokataa kumkamata aliyekuwa kiongozi wa Sudan, Jenerali Omar el Bashir baada ya mkutano wa Umoja wa Afrika nchini humo.

Kundi la wanaharakati nchini Msumbiji, Forum de Monitoria do Orcamento (FMO) likawakilisha ombi mahakamani kupangua uamuzi wa waziri huyo, kwa msingi kuwa hapakuwa na uhakika wowote kuwa Chang atashtakiwa.

Kulikuwa na ombi la Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (The Hague) ikimtaka kiongozi huyo kujibu mashtaka ya uhalifu wa kivita na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu jimbo la Darfur nchini Sudan.

Afrika Kusini ikiwa ndiyo mwenyeji wa mkutano na hasa mhakikishaji wa usalama wa wageni wake, ikasita na kukataa kukamatwa kwake kana kwamba alipita hapo tu.

Kilichofurahisha wanaharakati katika kuamuliwa suala la uhamishaji wa Chang ni hati ya maelezo ya mkurugenzi mkuu wa Wizara ya Sheria ya Afrika Kusini, Vusi Madonsela.

Kwanza alinukuu kwa kirefu maelezo ya Profesa Thomashausen katika jarida hilo kuwa Mamlaka ya Mashtaka ilipotezea tu kutokuona upana wa sheria ya Msumbiji kuhusu kutoshtakiwa, na hivyo kumpotosha hakimu mkazi wa Kempton bila kutazamia.

Wakati profesa alikuwa akitoa tuhuma laini kuhusu kilichopelekea uamuzi wa Mahakama hiyo, hati ya mkurugenzi ilimtuhumu waziri aliyetangulia kupuuzia ushahidi huo.

Masutha alipokea taarifa ya mshauri wa wizara wa sheria za kimataifa, kilio cha wanaharakati na ubalozi wa Marekani kuwa Chang hatashtakiwa Msumbiji na kinga yake haikuwa imeondolewa. Akapuuza.

Wachunguzi wa habari wanasema kuwa Masutha ni sehemu ya mabaki ya utawala wa Zuma katika Serikali ya ANC, hivyo alijali zaidi mshikamano na chama tawala ndugu cha Msumbiji, FRELIMO.

Ndiyo sababu inayoonekana inaingia akilini kwanini waziri huyo alipuuzia ushahidi na ushauri kuwa Chang akirudishwa Msumbiji anakwenda kula bata na siyo kujibu tuhuma zozote kisheria.

Waziri wa wakati huo wa Mambo ya Nje, Lindiwe Sisulu, alishasema kabla ya uamuzi wa Mahakama ya hakimu mkazi Kempton kuwa waziri Chang atarudishwa Msumbiji.

Baba yake ni Walter Sisulu, mmoja kati ya vigogo wa kihistoria wa ANC waliokuwa katika jela za utawala wa kibaguzi hadi mwaka 1990 na mshikamano kati ya vyama vya ukombozi ni kila kitu kwao.

Chang hashikiki Msumbiji kwani hata familia ya aliyekuwa rais, Armando Guebuza ilishatajwa mara kadhaa kuhusiana na kashfa hiyo.

Ni Marekani tu ambayo ina shauku na kesi hiyo na inaimudu, siyo Msumbiji au Afrika Kusini, swahiba wake.

UCHAMBUZI

# CUF ziarani kuhubiri sera yao mpya 'Furaha Haki kwa Wote'

**Na Sabato Kasika**

VIONGOZI wa Chama cha Wananchi (CUF) ngazi ya taifa, wakiongozwa na mwenyekiti wao Prof. Ibrahim Lipumba, wamekuwa katika ziara mkoani Dar es Salaam kutambulisha sera yao mpya ya 'Furaha Haki kwa Wote.'

Mbali na kutambulisha sera hiyo, viongozi hao pia wamekuwa na kazi ya kuimarisha chama kwa kufungua mashina mapya na kuhamasisha wananchi ili washiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Mahusiano ya Umma, Abdul Kambaya, ziara hiyo ilianza Julai 7 mwaka huu wilayani Kinondoni kisha ikahamia wilaya ya Ubungo, Ilala, Temeke na sasa ipo Kigamboni.

Mkurugenzi huyo anasema ziara hiyo, ambayo bado inaendelea wilayani Kigamboni, inatarajia kuhitimishwa leo Julai 24, kisha watajipanga kwa ajili ya kwenda mikoani ili kuendelea kutambulisha sera hiyo mpya.

Kambaya anasema ziara hiyo imeonyesha kwamba bado Chama cha CUF kina nguvu kubwa na kinaendelea kurejea kwenye hadhi yake, ambayo anadai ilivurugwa na mgogoro wa uongozi ndani ya chama hicho.

"Hapa nina maana kwamba kila tulikopita tulipokea wanachama wapya wengi tu, ambao wamejiunga na chama chetu, hivyo hizi ni dalili mojawapo kuwa CUF itarudi kwenye hadhi yake ya zamani," anasema.

Anasema mgogoro wa uongozi uliokuwapo katika chama hicho ulitaka kukidhoofisha, lakini sasa kimejipanga upya na ndio maana viongozi wa kitaifa wamefanya ziara hiyo, ambayo imeanzia Dar es Salaam.

Anasema, mwitikio wanaliopata na hasa wa wanachama wapya kujiunga na CUF hawakuutarajia na kwamba inawezekana wanafurahishwa na sera mpya ya 'Haki Sawa na Furaha kwa Wote.'




Prof. Ibrahim Lipumba (kushoto) akimpa kadi mmoja wa wanachama wapya, kwenye ziara ya viongozi wa CUF, wilayani Ilala. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**WANACHAMA WAPYA**

Kambaya anasema tangu ziara hiyo ianze hadi kufikia wiki hii, tayari CUF imeshapata wanachama wapya zaidi ya 2,000 na ana uhakika itaendelea kuvuna wengine zaidi katika wilaya za Temeke na Kigamboni.

"Kule Kinondoni ambako ziara yetu ilianzia, tulipata wanachama wapya 463 na kisha tukaenda Ubungo tukapata wanachama wapya 374, tumepata wanachama 495 na Temeke wanachama 866," anasema.

Anabainisha kwamba sera yao imejikita katika masuala ya afya, elimu, ajira, miundombinu na Tehama, na kwamba wanawachambulia wananchi na wanaielewa, ndio maana wanawaunga mkono.

"Kimsingi ni kwamba sera hii imejikita katika maisha halisi ya Mtanzania na inalenga kuhakikisha wajawazito wanapata lishe bora na kujifungua salama, elimu bora itakayowasaidia watoto kuwa na ujuzi wa kutosha," anasema.

Anaongeza kuwa sera hiyo pia inagusa mazingira ya sekta binafsi kutoa ajira kwa wingi, ujenzi wa miundombinu, pensheni kwa wazee na matumizi ya Tehama katika kuwezesha vijana kuendelea kujifunza.

Mkurugenzi huyo anasema, mambo yaliyomo katika sera hiyo yanawezekana, kwa vile kwa miaka 45 Prof. Lipumba amekuwa akifanya utafiti na kujifunza masuala mbalimbali ya uchumi na anaelewa anachotaka kufanya.

"Kila anayekubaliana na sera hii aendelee kutuunga mkono, kwani lengo letu ni kutaka tutumie utaalamu na ujuzi tulionao kwa ajili ya kujenga Tanzania, ambayo wananchi wake watakuwa na furaha wakati wote," anasema.



Baadhi ya wanachama wa CUF wa tawi la Haki Sawa na Furaha kwa Wote, Ilala, wakimsubiri Mwenyekiti wa chama hicho Prof. Lipumba na msafara wake.

**UCHAGUZI WA MITAA**

Kambaya anasema katika ziara hiyo pia wanatoa fomu maalum kwa wanachama wao ambazo wanaorodhesha majina kwa ajili ya kupata wale ambao watawakilisha chama katika uchaguzi huo.

"Tunaacha fomu hizo katika ofisi zetu za matawi ili kugawiwa kwa wanachama na zinalenga kuwatambua wale wenye sifa za kuwania uongozi, kwa sababu wasifu wao unajazwa humo," anasema.

Anafafanua kuwa baada ya hapo zitapelekwa kwenye ofisi za kata kwa ajili ya kuchambua majina hayo na hatimaye kupata wagombea wenye sifa za kuwakilisha vyema chama hicho katika uchaguzi huo. Aidha, anasema CUF kama taasisi, ina wajibu wa kuhamasisha wananchi ili hatimaye wajitokeze kwa wingi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika miezi michache ijayo.

"Maana ya Serikali za Mitaa na dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi, pia Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania inafafanua kuwa Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi vilivyo katika ngazi ya msingi ya Serikali," anasema.

Anasema Serikali za Mitaa huundwa, huendeshwa, husimamiwa na kuwajibika kwa wananchi wenyewe, hivyo kwa kutambua hilo, CUF inahamasisha wananchi ili hatimaye wajitokeze kwa wingi katika uchaguzi wa mitaa.

Anasema, Serikali za Mitaa zimeundwa kwa mantiki ya kuwawezesha wananchi wote kushiriki katika masuala ya siasa, uchumi, upatikanaji wa huduma na utawala katika maeneo yao na katika nchi yao.

"Muundo huu unawawezesha wananchi kuwa na udhibiti wa maamuzi ya wawakilishi wao, hivyo Serikali za Mitaa ni fursa kwa wanajamii kukuza demokrasia na ushiriki wao katika maendeleo ya maeneo yao," anasema.

Kambaya anabainisha kwamba wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali, inapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwao na kwamba ndio maana ya kupeleka madaraka kwa wananchi.

"Nikujulishe tu kwamba katika Uchaguzi Mkuu wa 2020, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) yatakuwa sehemu ya sera na ilani ya uchaguzi ya chama ya chetu," anabainisha.

Na Nimi Mweta

# Bunge Marekani lachoshwa uswahiba wa Trump na mtawala wa Saudia

•Ni kuhusu mauzo ya silaha



Rais Donald Trump wa Marekani (kushoto), akiwa na mwanamfalme wa Saudi Arabia Mohammed bin Salman. **PICHA: MTANDAO**

BARAZA la Senate nchini Marekani limeonyesha kutoridhika kwa kina na sera za Marekani kuhusu eneo la Ghuba, hasa mauzo makubwa ya silaha kwa Saudia kwani silaha hizo zinatumika katika vita chafu ya Yemen.

Ni nchi ambayo inasikitisha katika macho ya dunia kwa jinsi inavyoharibiwa, watu wengi kuuawa au kukimbia makazi hata kama hawavuki mipaka ya nchi, na miundombinu ya elimu na afya, majisafi, n.k, kuharibiwa kabisa.

Wengi kati ya wapigakura wa Marekani hawaoni furaha au sifa kuwa Marekani inachangia hali hiyo, kuwa adui ni Iran, n.k.

Wajumbe wa Baraza la Senate nchini humo wamepiga kura hivi karibuni kutaka kuzuia mauzo mapya ya silaha ambayo Rais Donald Trump aliyatangaza kwa bashasha mwezi uliopita, lakini juhudi hizo haziwezi kumzuia Trump kufanikisha azma yake.

Ili kumzuia rais kisheria asiweze kuuza silaha kwa nchi fulani, inabidi kuwe na wingi wa kura usio na mashaka, kwa mfano theluthi mbili ya kura za Senate ambako maswahiba wake wa Republican ndiyo wengi zaidi.

Ni wajumbe wachache wa baraza hilo wa Republican waliounga mkono muswada huo, uliopata kura 53 dhidi ya 45 uliposomwa na kupigiwa kura mara ya kwanza na ile ya pili, halafu 51-45 katika kura ya mwisho, hali inayoonyesha Rais Trump anaweza kutumia kura ya turufu, aziuze.

Azimio kuhusu suala hilo lililopitishwa na Senate lilikuwa na hatua 22 za kuchukuliwa kuzuia mipango ya Ikulu ya nchi hiyo kuuza silaha zenye thamani ya dola bilioni 8.1 kwa Saudi Arabia na Falme za Ghuba.

Mkazo wa Trump katika suala hilo ni umuhimu wa Saudia katika kuzuia wimbi la Iran kujitanua katika eneo hilo, wakati wabunge wa Marekani wanataka nchi hiyo iwe kioo na kielelezo cha kujali demokrasia na haki za binadamu si kuangalia 'salio' tu kuuza silaha.

Ikulu ya Trump ilitoa angalizo kabla ya kura hiyo kupigwa kuwa muswada huo usipopita basi rais atatumia kura ya 'veto' dhidi yake, akijua hautafikia viwango vinavyozuia 'veto' hiyo isitumike.

Upande mwingine wa taarifa ya Ikulu ulisisitiza kuwa kuzuiwa kuuzwa silaha hizo kungeathiri baadhi ya nchi washirika wa Marekani kama Korea Kusini, India, Jordan na nyinginezo ambazo zina leseni ya kutengeneza sehemu za silaha hizo katika mtiririko wa kimataifa wa ongezeko la thamani.

Ilisema pia kuwa sehemu kubwa ya mfumo wa viwanda vya silaha vya nchi za NATO hutegemea kwa kiwango kikubwa vifaa muhimu vinavyotengenezwa Marekani na hatimiliki ya uundwaji wake, hivyo kuwezesha utumiaji wa vifaa hivyo kushabihiana na NATO kuimarika kama mfumo wa ushirikiano wa utafiti na uundwaji wa silaha.

Ni utetezi wa ulinzi wa NATO kama mfumo na u-magharibi kwa jumla, kuwa haiwezekani kuingiza vikwazo ndani ya mfumo huo.

Silaha zinazoleta ugomvi ni za hali ya juu, ikiwa ni pamoja na makombora au mabomu yenye uwezo wa kutafuta kinacholengwa, injini mpya za ndege za siku nyingi za kivita za F-15, na michanganyiko tofauti ya silaha kadhaa za maroketi, makombora na injini za ndege za teknolojia ya juu sana zilizopangwa kuuzwa Saudia, Falme za Ghuba na Jordan.

Ugomvi na Bunge, hasa kwa upande wa wajumbe wa Democrat hauko katika mifumo ya NATO inavyofanya kazi, ila kama mauzo ya silaha nchi za nje yanalenga maslahi ya Marekani na maadili yake muhimu pia.

Wajumbe mabaraza yote mawili, Uwakilishi na Senate, wanachukia vita ya anga juu ya Yemen.

Pia kuna wasiwasi kuhusu ushirikiano na Saudia bila kujali haki za binadamu nchini humo na kuwajibika mtawala halisi wa Saudia, mwanamfalme Mohammed bin Salman katika mauaji ya mwandishi nguli Jamal Khashoggi ubalozi mdogo wa Saudia nchini Uturuki.

Utawala wa Trump umetumia mbinu ya kutangaza tishio la Iran katika eneo hilo kuwa ni hali ya hatari, kwa maana hiyo kutumia haki ya kisheria ya Ikulu (utawala wa jumla) kuweka kando uchunguzi wa Bunge kuhusu kufaa au kutofaa kwa uuzaji huo wa silaha.

Pia hatua hiyo ya kutangaza hali ya hatari hivyo silaha ziuzwe inakiuka kawaida ya kusitisha mauzo kama hayo pale Bunge likiyapinga.

Hata hivyo wako wajumbe wa Senate kwa upande wa Republican ambao licha ya kuainisha mapungufu ya kina katika uswahiba wa Marekani na Saudia hasa kwa upande wa viongozi wakuu wa Ufalme wa Saudia, bado waliona kuzuia mauzo ya silaha siyo jawabu la tatizo hilo.

Wajumbe hao, hasa wenyeviti wa kamati za Senate zinazohusika na mambo ya nje, masuala ya kijeshi na kamati ya uongozi wa kundi la Republican katika baraza hilo kimsingi walipinga hatua ya Marekani 'kujitenga' na washirika wake kutokana na mapungufu ya tawala za nchi hizo.

Hasa ikichukulia umuhimu wa kuhakikisha uwezo wa nchi hizo kujilinda na hali hatarishi kuhusu Iran.

Wachunguzi wa habari waliona maeneo mawili ya ushindani katika hisia za wajumbe Baraza la Senate kuhusu nini kitanguliwe na kuwa mhimili wa sera za Marekani kuhusu Saudia na Ghuba kwa jumla. Moja ni umuhimu wa kulinda mahusiano kati ya nchi hizo na Marekani hasa baada ya Marekani kujiondoa katika mkataba wa kimataifa wa udhibiti wa urutubishaji madini ya urani nchini Iran.

Hivyo hapatakuwapo njia nyingine ila kujitayarisha kwa misukosuko miongoni mwa washirika wa Marekani katika eneo hilo kwani Iran itachelea kupambana na nchi za Marekani, Uingereza moja kwa moja. Zina meli za kivita mpenyo wa Hormuz - kuzuia Iran isiuze mafuta.

Hisia ya pili ni mwenendo wa utawala wa Saudia hivi sasa, kwa mfano kuhusiana na ubaya wa vita ya Yemen ambayo ni mbaya zaidi kuliko ile ya Syria hivyo kufanya mauzo ya silaha za Marekani kuwa ni kuridhia uhalifu huo dhidi ya utu wa binadamu uendelee.

Hisia hii iko zaidi miongoni mwa wajumbe wa Democratic licha ya kuwa hata Republican wanachukia vita ya Yemen, lakini miongoni mwa Republican ni ushiriki na uwajibikaji wa moja kwa moja wa mwanamfalme Mohamed bin Salman kulikobadili kabisa sura ya Saudia miongoni mwa wabunge wa Marekani.

Katika nchi kama Marekani ambako hata rais anawajibika kwa yale aliyofanya endapo Mahakama na Bunge vinathibitisha dhamira ya kutenda jinai, iweje hatua ya MBS ya kuelekeza mauaji ya mwandishi nguli Kashoggi ipite bila kuhojiwa, ili silaha ziuzwe?

Mmoja wa wajumbe wa Senate walio karibu na Rais Trump, Lindsay Graham, alisema alipiga kura kuunga mkono kuzuiwa mauzo ya silaha ili kupeleka ishara kwa Saudia kuwa kama itaendelea kutenda inayotenda sasa, hakuna nafasi ya uhusiano wa kimkakati, maalum kati yake na Marekani.

Alisema kuendeleza uhusiano huo ndani ya mazingira ya kuuawa Kashoggi na vita ya Yemen ni jambo linalomfedhehesha Trump, kwani haihitaji uthibitisho wa Umoja wa Mataifa au mashirika ya ujasusi ya Marekani kuwa MBS aliagiza kuuawa kwa Kashoggi.

Ni jambo linaloingia akilini; hapakuwa na njia nyingine ya mauaji hayo kufanyika, nje ya maagizo ya mtawala huyo.

Ni ishara kuwa uhusiano kati ya Marekani na Saudia uko mbioni kubadilika, na kinachoulinda hivi sasa ni kuwa Marekani ina mzozo mkubwa na Iran hivyo inabidi kujisitiri kidiplomasia na hata tayari kwa vita.

Nje ya hali ya Iran ingekuwa vigumu kwa Rais Trump kutetea uhusiano maalum na Saudia. Anaungwa mkono kiasi na Baraza la Senate, na kupingwa kabisa Wawakilishi.

Ni wajumbe wachache wa baraza hilo wa Republican waliounga mkono muswada huo, uliopata kura 53 dhidi ya 45 uliposomwa na kupigiwa kura mara ya kwanza na ile ya pili, halafu 51-45 katika kura ya mwisho, hali inayoonyesha Rais Trump anaweza kutumia kura ya turufu, aziuze.



## Waomba uratibu misimu ya mvua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakulima mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwa na utaratibu wa kufuatilia na kuratibu misimu ya mvua katika kila eneo linalojishughulisha na kilimo ili inapoagiza pembejeo iwe inaendana na misimu ya kilimo maeneo yote.

Baadhi ya wakulima wa mahindi wa Kata za Ilembo na Santilya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, walisema wamekuwa wakishindwa kutumia mbolea kwenye baadhi ya maeneo kutokana na bidhaa hiyo kuchelewa kuwafikia.

Mmoja wa wakulima hao, Emmanuel Sosten, alisema katika ukanda huo msimu wa kilimo unaanza Agosti, lakini mbolea zinaanza kuingia Novemba, hali inayowafanya washindwe kutumia mbole hiyo kwa ajili ya kupandia.

Alisema wanashauriwa na wataalamu kuwa wanatakiwa watumie mbolea kupandia mahindi pamoja na kukuzia, lakini pembejeo hizo zinachelewa kuwafikia, hivyo wanashindwa kuzitumia kama wanavyoelekezwa.

"Wataalamu wanatoa elimu nzuri sana, lakini tunashindwa kuitumia kwa sababu ya mifumo ya uagizaji wa mbolea, mahindi yetu tunaanza kupanda Agosti, lakini mbolea zinaingia Novemba wakati mahindi yanahitaji kukuziwa," alisema Sosten.

Alisema serikali inatakiwa kubadilisha mfumo wa uagizaji wa mbolea hizo kwa kuzingatia misimu ya mvua kwa kila eneo ili kila eneo ambalo wananchi wanajishughulisha na kilimo waendane na msimu.

Samwel Mwaigaga, alisema baadhi ya maeneo yao mvua zikianza kunyesha barabara huwa hazipitiki kirahisi, hivyo kulazimika kutumia gharama kubwa kusafirisha na hivyo gharama kuongezeka, hali inayowafanya baadhi washindwe kumudu.

Alisema kama mbolea hizo zingekuwa zinawafikia kabla ya mvua kuanza ingekuwa rahisi kwa wao kuzihifadhi na kuzitumia msimu unapokuwa umefika ili waepuke gharama kuongezeka.

# Mazao yazalishwa kukabili tabianchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Mazao (Tari) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, kimejinasibu kuwa kimeanza kuzalisha mbegu za mazao mbalimbali zenye uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameanza kuathiri sekta ya kilimo katika baadhi ya maeneo nchini.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa anazungumza kuhusu maandalizi ya maonyesho ya wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo yanatarajiwa kuanza Agosti Mosi, mwaka huu.

Alisema mabadiliko ya tabianchi yameanza kuathiri kilimo katika baadhi ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini hasa katika Mkoa wa Iringa ambako baadhi ya wilaya zake mazao yalikauka kwa kukosa mvua ya kutosha.

Alisema taasisi hiyo imeanza kuzalisha mbegu za mazao ambazo zinakomaa haraka kwa ajili ya maeneo yenye mvua kidogo na mbegu zinazochukua muda mrefu kukomaa kwa ajili ya maeneo yenye mvua nyingi.

**Baadhi ya mbegu zinahitaji mvua kidogo, lakini mavuno yake ni makubwa na baadhi zinahitaji mvua nyingi ili kupata mavuno mengi.**

"Hapa tumeandaa mashamba darasa kwa ajili ya kufundishia wakulima wakati wa maonyesho ya Nanenane, tuna aina mbalimbali za mazao, yapo mahindi, maharage, ngano, soya pamoja na viazi lishe, wakati wa maonyesho tutakuwa na darasa maalumu ili wakulima wetu wabadilike na wazalishe kisasa," alisema Dk. Bucheyeki.

Vilevile, alisema taasisi hiyo imeanza kutumia mbinu ya mseleleko kufikisha teknolojia na utafiti kwa wananchi mbinu ambayo alisema ni yenye kasi zaidi ili kuhakikisha wananchi wanapata teknolojia hizo katika muda mfupi.


Mratibu wa Utafiti wa mazao kutoka katika taasisi hiyo, Dk. Ndabhimeye Mlengela, alisema mbali na aina mbalimbali za mbegu wanazowashauri wakulima wazitumie kulingana na hali ya hewa, pia wanatakiwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA).

Alisema taarifa hizo ni muhimu kwa wakulima kwa kuwa zinawasaidia kujua mwenendo wa hali ya hewa ikiwamo mgawanyiko wa mvua ili wanapopanda mazao yao wawe na uchaguzi sahihi wa mbegu.

Dk. Mlengela alisema baadhi ya mbegu zinahitaji mvua kidogo, lakini mavuno yake ni makubwa na baadhi zinahitaji mvua nyingi ili kupata mavuno mengi.

Mtafiti wa mazao kutoka katika taasisi hiyo, Catherine Kabungo alisema wanatumia mbinu mbalimbali kuhakikisha teknolojia wanazobuni zinawafikia wakulima ikiwamo maonyesho mbalimbali ya kilimo. Alisema mwaka huu wametumia mbinu ya maonyesho ya Kilimo Biashara na wanatarajia kutumia pia maonyesho ya Nanenane kuonyesha teknolojia kwa wakulima.

Alisisitiza wanafuatilia kwa wakulima ili kujiridhisha kama wanatumia teknolojia wanazofundishwa pamoja na kuwarekebisha wanapokosea.



Baadhi ya waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya na Maofisa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa), wakiwa ndani ya pango, lililoko ndani ya Hifadhi ya Mpanga Kipengele juzi, ambalo linadaiwa kuwa lilikuwa linatumiwa na Chifu Mkwawa na Chifu Melele kupanga mikakati ya kupambana na askari wa Wajerumani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Fursa lukuki za Hifadhi ya Mpanga-Kipengele zatajwa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

HIFADHI ya Wanyamapori ya Mpanga- Kipengele imetajwa kuwa miongoni mwa hifadhi zenye vivutio vingi na vya kipekee ambavyo vikitumika vizuri vinaweza kuinua sekta ya utalii katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini.

Hayo yalisemwa na ofisa utalii wa hifadhi hiyo ambayo inaigusa mikoa ya Mbeya na Njombe, Emmanuel Silayo, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya ambao walifanya ziara ya siku mbili katika hifadhi hiyo na kutembelea baadhi ya vivutio.

Alisema Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Tawa) inafanya jitihada mbalimbali za kuimarisha utalii katika hifadhi hiyo ikiwamo kuvitangaza vivutio vilivyomo na kuhakikisha vinafikika kirahisi.

Silayo alivitaja baadhi ya vivutio ni maporomoko ya maji ambayo ni ya kipekee, mapango ya asili likiwamo lililokuwa linatumika na Chifu Mkwawa wa kabila la Wahehe na mwenzake Chifu Melele wa Wasangu kujadili mbinu za kupambana na askari wa Wajerumani.

Vilevile, alisema ndani ya hifadhi hiyo kuna baadhi ya wanyama wenye kuvutia wakiwamo tandala wakubwa ambao wanapatikana katika uwanda wa chini, fisi maji, ndege wa aina mbalimbali pamoja na maua ya kuvutia hasa katika safu za Mlima Kipengele.

"Tuna maporomoko makubwa matano ndani ya hifadhi yetu ambayo ni Lyamakunohila, Ikovo, Kipengele, Kimani na Nyaugenge ambayo yote yanapatikana kwenye Mto Kimani, kwa sasa tunachokifanya ni kuhakikisha tunatengeneza miundombinu ya kuwezesha vivutio vyote kufikika na sasa tumeanza kutengeneza barabara," alisema Silayo.

Vilevile, alisema nje ya hifadhi hiyo vimebainika baadhi ya vivutio ikiwamo alama za unyao wa binadamu wa kale ambazo zipo kwenye mawe na kwamba wanaendelea na utafiti wa kubaini kama zimo hata ndani ya hifadhi.

Mratibu wa Klabu za Malihai (MCT) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Humphrey Ntuku, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo pamoja na zingine ili kuhakikisha wanakuwa sehemu ya kulinda maliasili zilizomo.

Alisema wanatoa zaidi elimu na kuunda klabu za Malihai katika maeneo ya shule za msingi na sekondari, lakini elimu inatolewa pia kwa wananchi wa kawaida kupitia mikutano ya hadhara.

Ntuku alisema Tawa pia inawezesha wanachama kulinda mazingira kwa kupanda miti katika maeneo yao na kuwawezesha wanachama kufanya ziara kwenye hifadhi mbalimbali pamoja na mapori ya akiba yanayosimamiwa na serikali.





# Ofisa Nida akamatwa kwa wizi wa kamera 12

Na Renatha Msungu, DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linamshikilia Ofisa Usajili wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa(NIDA), Ezekiel Subugo(24) kwa wizi wa kamera 12 za mamlaka hiyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Gilles Muroto, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa katika msako uliofanywa na jeshi hilo juzi.

Alisema mbinu aliyotumia ni kutumia nafasi yake kuiba ofisini vifaa hivyo na kuuzia watu mitaani.

"Uhalifu huu ni mbaya hasa unapohusisha mtumishi, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani," alisema.

Pia, Jeshi hilo limemkamata mkazi wa Area A jijini Dodoma, Rajabu Kambi (32), ambaye kwa muda mrefu amekuwa akitapeli watu kwa kujifanya askari polisi na kuwatishia kwa silaha bandia.

**Uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa kijana huyu aliwahi kuhudhuria mafunzo ya JKT na kufukuzwa kwa utovu wa nidhamu.**

Muroto alisema kijana huyo alikamatwa akiwa na sare ya polisi, bastola ya bandia, picha na sare ya JWTZ.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa kijana huyu aliwahi kuhudhuria mafunzo ya JKT na kufukuzwa kwa utovu wa nidhamu," alisema.

Alisema kumekuwa na taarifa za watu kutapeliwa kirahisi hasa wengi wakitumbukizwa katika tamaa ya kupata fedha nyingi kwa muda mfupi na mwisho wake wanajikuta wametapeliwa.

"Nitoe wito wangu kwa wananchi kutokukubali kuibiwa au kutapeliwa na wadanganyifu na hakuna fedha zinazopatikana pasipo kufanya kazi halali, kila mtu afanye kazi halali kwa bidii," alisema.

Katika hatua nyingine, mkazi wa Hazina, Mussa Pungu, amekamatwa na madawa ya kulevya aina ya heroini kete 132 zikiwa zimefungashwa kwenye nailoni.

"Mtuhumiwa Mussa kwa muda mrefu ameharibu vijana wengi kwa madawa ya kulevya katika mtaa wa Hazina katika Jiji la Dodoma, mtuhumiwa na wenzake wanne watafikishwa mahakamani," alisema.

Wakati huo huo, Kampuni ya Innomax imekabidhi pikipiki mbili mpya kwa jeshi la polisi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na doria katika mji wa Dodoma.

Aliishukuru kampuni hiyo kwa uzalendo wao wa kulileta taifa maendeleo na kuwaomba watu wengine waige mfano huo.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, akitoa ufafanuzi jijini humo juzi, wakati wa kikoa cha kutoa tamko la kulaani waraka wa makatibu wakuu wastaafu wa chama hicho, Yusufu Makamba na Abdulrahamani Kinana, walioutoa kwenye vyombo vya habari. Kulia ni Katibu wa CCM wa mkoa huo, Jamila Yusufu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CCM walaani waraka wa Kinana, Makamba

Na Augusta Njoji, DODOMA

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Dodoma kimewataka viongozi wastaafu kufuata taratibu za kisheria na kikatiba kuwasilisha malalamiko yao katika vyombo husika.

Imewataka viongozi hao kumpa nafasi Mwenyekiti wa CCM, Rais John Magufuli nafasi ya kuwatumikia Watanzania na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa CCM 2015/2020 bila kumbugudhi.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu Mwenezi wa CCM mkoa, Henry Msunga, alipokuwa akitoa tamko la kikao cha halmashauri hiyo jijini hapa.

Alisema halmashauri hiyo inalaani vikali waraka wa Makatibu Wakuu wastaafu wa CCM, Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba, walioutoa kwenye vyombo vya habari bila kufuata utaratibu wa chama kwa kupitia kanuni na taratibu walizojiwekea.

"Halmashauri Kuu imesema kitendo hicho cha kumhusisha mwanaharakati Cyprian Musiba na CCM ni ukiukwaji mkubwa wa maadili na miiko ya chama, hasa ikizingatiwa kwamba matamko yaliyotolewa na Musiba ni ya binafsi walipaswa viongozi hawa kushughulika na mtu na sio taasisi hii kubwa,"alisema.

Msunga alisema viongozi hao walipaswa kuwasilisha malalamiko yao kama ambavyo imeshauriwa na Katibu wa Baraza la Wazee, Pius Msekwa. Alitaka hatua kali zichukuliwe dhidi ya viongozi hao wastaafu kwa kuwa wameonyesha dhahiri kuwa na nia ovu katika safari ya kuiletea nchi maendeleo wakati Rais amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha nchi hiyo inastawi.

Vile vile, alisema kikao hicho kinaipongeza serikali inayoongozwa na Rais Magufuli kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa katika kutekeleza ilani ya uchaguzi na kuwaondolea kero Watanzania.

Naye, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, alisema katika kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu, Dodoma itaendelea kuwa ngome ya CCM.

Alisema Rais amefanya kazi kubwa Dodoma kwa uamuzi wake wa kuhamishia Makao Makuu ya nchi, na kwamba kuna kila sababu ya kujitokeza kukemea mambo yanayoharibu mstakabali wa nchi.

# Utaratibu mpya usajili wa NGO waanza

Na Renatha Msungu, DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na mamlaka zingine za serikali, imefungua kituo cha pamoja cha kusajili mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (Ngo's) kwenye mikoa ya kanda ya kati ili kutekeleza mabadiliko ya sheria namba tatu ya mwaka 2019 inayosimamia mashirika hayo.

Kituo hicho kinaratibiwa na wizara hiyo kwa ushirikiano na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Wizara ya Mambo ya Ndani ni utekelezaji wa matakwa la sheria hiyo ambayo pamoja na mambo mengine inaweka bayana usajili na utendaji kazi wa mashirika hayo kulingana na shughuli na huduma wanazotoa nchini.

Hayo yalisemwa na Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali wa wizara hiyo Vickness Mayao, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sheria hiyo kwa mashirika hayo.

Alifafanua kuwa huduma hiyo ya usajili itadumu kwa muda wa siku tano na kuwataka wadau ambao wapo katika maeneo mengine waweze kufika kupata usajili kwa kuwa zoezi hilo sasa limerahisishwa ili kukidhi mahitaji ya wadau husika wanaofika kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni taasisi hizo kuzingatia muda uliowekwa ili wapate usajili kulingana na sheria iliowekwa ili waweze kutekeleza majukumu yao kiufasaha zaidi.

"Hii sheria inayataka mashirika hayo kujisajili katika Sheria ya Ngo's kwa kipindi cha miezi miwili hivyo huu ni wakati wa mashirika kujitathmini yako wapi ili yaweze kufanya uamuzi sahihi kabla ya kipindi kilichotolewa cha kufikia ukingoni," alisema Mayao.

Mwakilishi wa Msajili wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Thomas Hanila, alisema marekebisho ya sheria hiyo kwa kiasi kikubwa yataondoa vitendo vya uhalifu na ukiukwaji wa maadili mila na tamaduni kwa kutumia mwamvuli wa Ngo's kinyume na sheria.

Alisema kituo hicho kitahudumia mikoa ya Dodoma Singida, Tabora na Kigoma.

Alipongeza utaratibu huo kwa kuwa umeondoa ukiritimba.

Alisema usajili huo kwa kanda ya kati utakamilika Julai 26 na baadae kuhamia kwenye kanda nyingine. Naye, Khadija Omari kutoka Taasisi ya Tuvuke Wote, iliyoko jijini Dodoma alisema mashirika yanapaswa kujitokeza kwa wingi huku akipongeza taratibu za usajili zilizowekwa kuwa ni za haraka tofauti na jamii inavyofikiria.



# Watakiwa kutumia fursa za maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIJANA wametakiwa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali ili kufikia malengo ya kujikwamua na tatizo la umaskini katika maeneo yao.

Hayo yalisema jana na Katibu wa Baraza la Sanaa, Sensa na Filamu Zanzibar, Dk. Omar Abdallah Adam, alipokuwa akifungua mafunzo kwa Baraza la Vijana Shehia ya Pangawe, katika Shule ya Msingi Kijitoupele, Wilaya ya Magharibi B.

Alisema serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuwasaidia vijana kufikia malengo ya kujikwamua na tatizo la umaskini ikiwamo kuanzisha mfuko maalum wa Khalifa Fund.

Adam alisema ni vyema vijana wakaandaa miradi itakayokubalika na kupatiwa mitaji ya kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Pia aliwataka vijana hao kufuata misingi na taratibu za nchi zilizowekwa ili kujua wajibu wao katika kutetea, kulinda na kujenga nchi yao.

Vilevile, aliwataka kutii maelekezo wanayopewa na viongozi wao ili kuepuka kutumiwa vibaya na baadhi ya watu wasiopenda maendeleo.

Aliwataka vijana hao kuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania katika kudumisha amani na utulivu nchini.

Sambamba na hayo, aliwaomba wanasiasa kutumia nafasi zao katika kuielimisha wafuasi wao kuacha kushabikia masuala yasio na mwelekeo katika maisha yao kama vile kutumia dawa za kulevya.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Shehia ya Pangawe, Mtumwa Suleiman Mnoga, alisema lengo la kuandaa mafunzo hayo ni kuwajenga vijana kuwa wazalendo wa nchi yao katika kuilinda kuitumikia na kuwaomba kushirikiana ili kufikia malengo yaliopangwa na serikali.

**serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuwasaidia vijana kufikia malengo ya kujikwamua na tatizo la umaskini ikiwamo kuanzisha mfuko maalum wa Khalifa Fund.**

# Wasaidia kifaa cha uchunguzi saratani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Watu wenye Ulemavu wa Uoni Tanzania kimeikabidhi Wizara ya Afya kifaa tiba cha uchunguzi wa kansa ya ngozi kwa watu wenye ualbino na watu wengine Zanzibar.

Akizungumza jana katika hafla ya makabidhiano hayo yaliyofanyika makao makuu ya Wizara ya Afya, Mwenyekiti wa Jumiya ya Watu wenye Ualbino Zanzibar, Raya Mselem, alisema kupatikana kwa kifaa hicho kutapunguza gharama za kufuata matibabu Tanzania Bara kwa albino wenye saratani ya ngozi.

Alisema awali Zanzibar hakukuwa na kifaa tiba cha uchunguzi wa saratani ya ngozi, hivyo watu wenye ualbino walikuwa wakipata usumbufu mkubwa kufuata huduma hiyo.

Kutokana na hali hiyo, alisema watu wenye ualbino wanaathirika sana ngozi kutokana na mionzi ya jua na husababisha kupata saratani ya ngozi.

**Saratani ya ngozi inasababishwa na mionzi mikali ya jua na watu 10 wenye ualbino wanaofika katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dar es Salaam, watu watatu hugundulika na saratani na wengi wao hufariki dunia.**

"Saratani ya ngozi inasababishwa na mionzi mikali ya jua na watu 10 wenye ualbino wanaofika katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dar es Salaam, watu watatu hugundulika na saratani na wengi wao hufariki dunia," alisema.

Aidha, alisema katika kazi wanazofanya za kutafuta kipato hufanyia juani ikiwamo kilimo na kazi zingine, hivyo mionzi ya jua huwaathiri sana.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Tanzania, Agaodson Molle, aliyeomba Wizara ya Afya Zanzibar kuhakikisha katika hospitali za wilaya kunakuwa na kliniki ya ngozi ili kuwawezesha watu wenye ualbino kupata huduma.

Alisema wengi wao hali zao za kipato ni duni, hivyo inawawia vigumu kufuata huduma hiyo katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja au kwenda nje ya Zanzibar ambako kunahitaji gharama za kifedha.

Molle aliipongeza serikali ya Tanzania na ya Zanzibar kwa kupiga vita na kutokomeza mauaji ya wenye ualbino.

Naibu Waziri wa Afya, Harous Said Suleiman, alisema vifaa hivyo tiba vya kuchunguza saratani ya ngozi kutaimarisha utoaji wa huduma katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

Suleiman alikipongeza chama hicho kwa msaada huo na kukitaka kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuacha kuwanyanyapaa watu wenye ualbino.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kuacha kuwaficha watu wenye ualbino na badala yake kuwapeleka shuleni ili kupata elimu ambayo itawasaidia katika maisha yao ya baadaye.

"Pia niwaombe wazazi kuhakikisha wanawavisha nguo zenye kufunika mwili wao watoto wenye ualbino ili wasiathiriwe na mionzi ya jua," alisema.



Ofisa Utawala wa Chuo Kikuu cha Zanzibar, Hassan Haji (kushoto) na Sultan Said Omar Mhadhiri Msaidizi wakiwa kwenye banda lao kwenye maonyesho ya vyuo vikuu yaliyokwisha hivi karibuni katika Viwanja vya Mnazi Mmoja. jijini Dar e sa Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama yatishia kufuta kesi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAHAKAMA Kuu ya Zanzibar imesema inakusudia kuzifuta kesi ambazo ziko mahakamani kwa muda mrefu na bado upelelezi wake haujakamilika.

Mahakama hiyo imesema kufanya hivyo kutasaidia kupunguza idadi ya mahabusi waliokaa gerezani kwa muda mrefu. Hatua hiyo imekuja baada ya Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, kufanya ziara katika magereza mbalimbali kwa ajili ya kuangalia hali halisi iliyomo magerezani na utendaji wa kazi katika mahakama visiwani Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mrajis wa Mahakama Kuu Zanzibar, Muhammed Ali Muhammed, alisema mambo ambayo yanasababisha mrundikano wa mahabusi katika magereza ya Zanzibar ni kutokuwapo dhamana na masharti ya dhamana kuwa magumu.

"Hivi sasa kuna mrundikano mkubwa wa mahabusi katika magereza yetu ambao wanakabiliwa na kesi mbalimbali ikiwamo za ubakaji," alisema.

Aidha, alisema kutokana na ziara hiyo ya Jaji Mkuu alitoa maelekezo kwa Mahakimu kuhakikisha kuwa suala la dhamana linapatiwa ufumbuzi kwa makosa yote ambayo ni madogo kwa mujibu wa sheria ili kuondosha usumbufu unaojitokeza.

Hata hivyo alisema hali halisi ya magereza kwa Zanzibar ni nzuri kutokana na serikali kuboresha pamoja na kuwajengea watoto magereza yao ili kuondosha msongamano uliokuwapo hapo awali.

Wakizungumza wakati Jaji Mkuu alipofanya ziara katika Gereza la Zanzibar, baadhi ya watuhumiwa walioko mahabusu walilalamikia kitendo cha kunyimwa dhamana wakati wanafamilia zinawategemea.

HABARI KITAIFA

# Tembo wazua taharuki

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

HALI ya taharuki jana imewakumba wananchi wa kata za Nyasura na Sazira wilayani Bunda Mkoa wa Mara pamoja na taasisi kadhaa, baada ya tembo kutoka katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuvamia katika maeneo yao.

Maeneo mengine yaliyokumbwa na taharuki hiyo ni jumuiya ya Chuo cha Ualimu Bunda na Shule ya Msingi Mazoezi.

Baada ya uvamizi wa wanyama hao, baadhi ya wananchi wakiwamo wanafunzi walipatwa na taharuki na kuanza kukimbia huku na kule kwa ajili ya kuokoa maisha yao, huku wanafunzi wengine wakiwasogelea kwa karibu zaidi wanyama hao.

**Ni kweli tembo walikuwa watano na wamevamia katika maeneo haya na kuleta taharuki kwa wananchi kwani si kawaida wanyama hawa kufika katika maeneo haya.**

Tembo hao watano walivamia katika maeneo hayo jana majira ya asubuhi. Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nyasura, Kagoye Mwenge, alithibitisha wanyama hao kuvamia katika makazi ya watu.

"Ni kweli tembo walikuwa watano na wamevamia katika maeneo haya na kuleta taharuki kwa wananchi kwani si kawaida wanyama hawa kufika katika maeneo haya," alisema Mwenge.

Alisema baada ya tembo hao kuvamia katika maeneo hayo, wananchi walianza kuwafukuza kwa kupiga yowe, ambapo askari wa wanyamapori walifika katika maeneo hayo na kuwafukuza kwa ajili ya kuwarudisha hifadhini.

Alitoa angalizo kwa wananchi pindi wanapoona wanyama hao katika makazi yao wasipige kelele wala kuwakaribia kwa karibu kwa kuwa wanaweza kuwadhuru.

Baadhi ya walimu na wanafunzi walisema wanashangazwa na wanyama hao kufika katika makazi ya watu, na kuwaomba askari wa Maliasili kuwadhibiti wanyama hao.

Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Bunda, Marwa Kitende, alisema ameshawatuma askari wa wanyamapori ili wawarejeshe hifadhini.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa majengo ya ofisi za stedi mpya ya mabasi ya mikoani katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ujenzi wa daraja kukomboa wananchi

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

ADHA ya ukosefu wa daraja kwa zaidi ya miaka 50 katika Mto Miesi unaounganisha vijiji vitano vya Kata ya Lupaso kikiwamo kijiji cha Mbangara wilayani Masasi mkoani Mtwara, itakuwa historia baada ya serikali kuanza ujenzi wa daraja.

Imeelezwa kwamba daraja hilo ni la kisasa lenye thamani ya Sh. milioni 800, na kwamba kukamilika kwake kutasaidia kupunguza changamoto ya wajawazito kujifungulia njiani na majumbani, kutokana na wengi kushindwa kuvuka mto huo kipindi cha masika kutokana na kujaa maji.

Hayo yalibainishwa jana wilayani Masasi na wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Lupaso kwenye kikao cha kujadili shughuli za maendeleo ya kata hiyo kwa robo ya nne ya 2019/2020.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Lupaso, Heri Selemani, alisema ukosefu wa daraja kwenye mto huo ambao unaunganisha vijiji zaidi ya viwili vya Lupaso pamoja na Mbangara umekuwa adha ya muda mrefu kwa maendeleo ya vijiji hivyo kwa sababu ni vigumu kuvuka mto pindi unapofurika maji, hivyo hata kusafirisha mazao ya wakulima ni tatizo.

Alisema wananchi waishio kando ya mto huo wanategemea kupata huduma mbalimbali katika Kijiji cha Lupaso zikiwamo huduma za afya, hivyo wanalazimika kuvuka mto huo ili kufika Kijiji cha Lupaso.

Alisema lakini kutokana na mto huo kuwa mkubwa na kujaa maji, wananchi wanashindwa kuvuka, hivyo shughuli za kiuchumi kukwama na hata wajawazito kujifungulia majumbani.

Alisema Kata ya Lupaso ina uchumi mkubwa ambao ni tegemeo chanya kwa wilaya kwa ujumla, lakini kikwazo kikubwa ni daraja kwa sababu wananchi wanashindwa kuvuka na mazao yao kama korosho, ufuta, mbaazi na mahindi kwenda kuuza, lakini daraja hilo likikamilika adha hiyo haitakuwapo tena.

Antony Mrekoni, Mwenyekiti wa Kijiji cha Utimbe, alisema ushirikiano kati ya diwani, mtendaji kata na wenyeviti wa vijiji vyote vitano vya Kata ya Lupaso umekuwa na tija katika kuleta maendeleo ya kata hiyo, baada ya serikali kukubali kujenga daraja hilo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Lupaso ambaye pia ni Diwani wa kata hiyo, Douglas Mkapa, aliipongeza serikali kwa kuanza ujenzi wa daraja muhimu kwa wananchi wa vijiji vilivyozunguka kata, na kwamba kero ya wanawake kujifungulia majumbani kwa kuhofia kuvuka mto huo sasa itakwisha.

Aidha, Mkapa alisema miradi mingine ambayo inatekelezwa kwenye kata hiyo ni ujenzi wa nyumba nne za walimu wa shule ya sekondari ya Lupaso ambapo pia ilikuwa ni changamoto na kwamba mradi huo

ITV

KIPINDI MAALUMU: SAA 3:10 USIKU

FUATILIA KIPINDI HIKI IKIWA NI KUONYESHA MIPANGO NA MIKAKATI MBALIMBALI YA SHIRIKA KATIKA KUHAKIKISHA KILA MWANANCHI ANAPATA UMEME WA UHAKIKA NA KWA GHARAMA NAFUU KUPITIA MRADI WA REA NA MIRADI MINGINE YA SHIRIKA.

# Wakubaliana kukuza sekta ndogo ya maziwa

**Na Enock Charles**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Kampuni ya Heifer International wamekubaliana kuendeleza sekta ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ili kuongeza tija katika uzalishaji maziwa na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa.

Makubaliano hayo yametiwa saini jijini Dar es Salaam jana na Mkurugenzi wa Fedha wa TADB, Derick Lugemala na Meneja Mradi wa Heifer International Tanzania, Mark Tsoxo. Akizungumza na waandishi wa habari katika halfa hiyo, Lugemala alisema TADB iko tayari kushirikina na Heifer International kuendeleza sekta ya maziwa ambayo ni muhimu katika ustawi wa viwanda vya usindikaji maziwa nchini.

"Heifer International ina uzoefu mkubwa katika sekta ya maziwa. Hivyo TADB imeingia nao makubaliano ili kuwaingiza wafugaji katika utaratibu maalum ambao utawawezesha kupata mikopo ambayo itasaidia kuendelea sekta hiyo hapa nchini," alisema Lugemala.

Alisema TADB imekuwa ikitoa mikopo katika sekta ya kilimo ili kuchagiza maendeleo katika uzalishaji wa mazao yenye tija na kukubalika katika masoko; hivyo sekta ya maziwa ni sehemu ya majukumu ya benki katika kuendelea sekta mifugo.

"Lengo la kuwapo kwa Benki ya Kilimo ni kuchagiza maendeleo katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Hivyo tutaendelea kushirikiana na wadau ili sekta hizi ziweze kukua na kuchochea uanzishwaji wa viwanda mbalimbali na kupelekea nchi kupata maendeleo," alisema.

Aliongeza kuwa jambo muhimu ni wafugaji kupata elimu na mbinu bora za ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa ili waweze kuzalisha maziwa kwa wingi na uwepo wa upatikanaji wa uhakika wa maziwa kwa ajili ya viwanda vilivyopo vya kusindika maziwa kama vile Tanga Fresh na ASAS Dairies.Alisema sekta ya maziwa nayo imepewa kipaumbele ili itoe mchango kwa pato la taifa.

Naye Tsoxo alisema makubaliano hayo yataongeza kasi ya kuwaunganisha wafugaji katika vikundi nchini ili kupata elimu na mbinu za kisasa za ufugaji ili uzalishaji wa maziwa uongezeke nchini.

"Jukumu letu ni kuhakikisha wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa wananufaika kiuchumi kupitia sekta hii na kuwa sehemu ya kutekeleza azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda," amesema Tsoxo.

Makubaliano haya yatasaidia wakulima kupata huduma za kifedha kutoka TADB ili kukuza na kuendeleza sekta ya maziwa ambayo imekuwa mkombozi kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa katika mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya.

HABARI KIMATAIFA

## Waasi wa ADF waushambulia mji wa Beni

**KINSHASA,** Congo

WAASI wa kundi la ADF kutoka Uganda wamewaua raia zaidi ya 20 mjini, mauaji yaliyotokea baada ya Rais wa Congo, Félix Tshisekedi (pichani) kuahidi kuwatokomeza waasi hao.

Waasi hao pia wameua watu 10 kwa kuwakata na mapanga usiku wa kuamkia jana kaika kata ya Mabasele, katika mji mdogo wa Oicha.

Mwenyekiti wa mashirika ya kiraia katika mji wa Beni, Kizito Hangi alisema, kuwa haelewi hali ya kusuasua kwa operesheni za kijeshi dhidi ya waasi wa ADF katika eneo hilo.



Akizungumzia maeneo yaliyoshuhudia mauaji hayo, Kizito alimuomba Rais Tshisekedi kutekeleza ahadi yake kwa raia wa Beni, wakati wa ziara yake katika eneo hilo.

Mauaji yaliyotokea usiku wa kuamkia jana baada ya yale yaliyofanywa na waasi hao katika vitongoji vya Eringeti, Mayimoya, Mangboko na Malolu, yamezusha hofu mioyoni mwa wakazi, waliokuwa na matumaini kwamba amani ya kudumu imerejea katika eneo hilo.

Katika kuwashambulia waasi wa ADF, baada ya kuwaua raia, majeshi ya serikali yalifanikiwa kuwaua waasi wanne, na kuchukuwa silaha mbili kutoka kwa waasi hao.

"Hongera kwa majeshi ya serikali ya Kongo, kwa kazi walioifanya ya kuwaua waasi wanne na kuchukuwa silaha zao,"alisema Meya wa Beni, Bwanakawa Masumbuko Nyonyi.

Idadi ya waasi wa ADF waliouawa katika operesheni za kijeshi, imeongezeka na kufikia watano. **DW**

# Johnson ang'ara mbio za uwaziri mkuu Uingereza

**LONDON,** Uingereza

MBIO za kuwania kiti cha Waziri Mkuu Uingereza zinafikia tamati baada ya Boris Johnson kushinda kwa kishindo uchaguzi wa wananchama wa Conservative wa kumchagua kiongozi wao mpya.

Johnson ambaye ni Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje wa Uingereza alichaguliwa kuwa kiongozi wa chama tawala cha Conservatives nchini humo kwa kupata kura 92,153 dhidi ya mpinzani wake Jeremy Hunt aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje ambaye alipata kura 46,656.

Kwa matokeo hayo, inamaanisha kuwa Johnson atakuwa Waziri Mkuu mpya wa Uingereza baada ya May kutangaza kujiuzulu mwezi uliyopita.

Boris mwenye umri wa miaka 55 alimshinda mpinzani wake Jeremy Hunt kwa wingi wa kura katika uchaguzi wa wanachama wa chama cha conservatives jana.

Waziri huyo wa Mambo ya Nje wa zamani wa Uingereza anatarajiwa kuchukua rasmi nafasi hiyo ya Waziri Mkuu leo.

**Boris mwenye umri wa miaka 55 alimshinda mpinzani wake Jeremy Hunt kwa wingi wa kura katika uchaguzi wa wanachama wa chama cha conservatives jana.**

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema kungekuwa na mshituko mkubwa iwapo uongozi usingekwenda kwa Boris Johnson, ambaye pia aliwahi kuwa meya wa zamani wa Jiji la London.

Johnson amekua kivutio kikubwa kwa wanachama wa Conservative kwa kuahidi kufanikisha pale ambapo May alishindwa kuiongoza Uingereza kujitoa kutoka Umoja wa Ulaya (EU) katika tarehe iliyopangwa oktoba 31, mwaka huu.

Johnson alikuwa kiongozi wa kura ya maoni iliyotaka Uingereza kuondoka EU mwaka 2016.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Johnson ameahidi kuwa ataiwasilisha Brexit, kuiunganisha nchi na kumshinda Jeremy Corbyn.

Johnson alisema: "Tutaipa nchi nguvu.Tutaiwasilisha Brexit kufikia Oktoba 31 na kuchukua fursa zote zitakazotokana na muamko mpya wa inawezekana.Tutajiamini upya na tutainuka upya na kuondosha shaka na fikra za kutojiamini".

Takriban wanachama 160,000 wa Conservative walikuwa na fursa ya kupiga kura lakini waliojitokeza walikuwa ni asilimia 87.

Asilimia ya kura kwa Johnson ilikuwa ni asilimia 66.4 ikiwa ni pungufu ya aliyojishindia Waziri Mkuu wa zamani wa nchi hiyo, David Cameron mwaka 2005 aliyejinyakulia asilimia 67.6.

May alimpongeza Johnson, na kumuahidi ushirikiano wake kikamilifu.

Rais wa Marekani, Donald Trump pia alimtumia ujumbe katika mtandao wa kijamii wa Twitter akimpongeza Johnson kwa kueleza atakuwa kiongozi mzuri.

Jeremy Corbyn alituma ujumbe kwenye mtandao wa Twitter akisema: "Nimeshinda uungwaji mkono wanachama chini ya 100, 000 wasiowakilisha wa chama cha Conservative, lakini "hajashinda uungwaji mkono wa nchi yetu".

Boris alishinda uchaguzi uliofanyika jana katika chama cha Conservative kwa kupata kura 92,153 dhidi ya mpinzani wake Jeremy Hunt aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje ambaye alipata kura 46,656. **DW**




Boris Johnson akishangilia baada ya kutangazwa mshindi wa uchaguzi wa wananchama wa Conservative. **PICHA: AP**

# Kamati ya kupambana na ebola yaidhinishwa

**KINSHASA,** Congo

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) imeidhinisha kamati ya kuratibu muitikio wa serikali katika kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa wa ebola, mashariki mwa nchi hiyo.

Hatua hiyo imeidhinishwa saa chache baada ya mhusika aliyeongoza jitihada hizo kwa muda mrefu kujiuzulu.

Waziri wa Afya wa DRC, Oly Ilunga, alijiuzuru baada ya kulalamika namna ambavyo mlipuko huo wa Ebola unavyoshughulikia.

Baadhi ya viongozi wa kisiasa kutoka Ikulu wanaeleza kuwa Dk. Ilunga amejiuzulu kutokana na tuhuma kwamba alikataa kuwashirikisha watu wengine katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Katika barua yake ya kujiuzulu, Ilunga alishutumu uamuzi wa Rais Félix Tshisekedi kumteua mtu mwingine wa kikosi kinachokabiliana na ugonjwa wa ebola nchini humo.

Pia, alishutumu alichokitaja kuwa shinikizo la nje la kuidhinisha chanjo za majaribio kwa ugonjwa huo.

Mlipuko wa ugonjwa wa ebola umesababisha vifo vya zaidi ya watu 1,700 katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Wiki iliyopita Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza kwamba mlipuko wa ugonjwa huo kuwa dharura ya afya ya kimataifa. Janga la ugonjwa wa ebola liliathiri sehemu kadhaa za Afrika Magharibi kuanzia mwaka 2014 hadi 2016, na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 11,000.

Katika barua yake kwa Rais Tshisekedi, Ilunga alishutumu uamuzi wa yeye kuondolewa kama kiongozi wa kikosi kinachokabiliana na ebola nchini na badala yake kuchaguliwa kamati ilio chini ya usimamizi wa Rais.

Alisema wanakamati hao waliingilia kazi yake katika miezi ya hivi karibuni.

Pia Ilunga alishutumu shinikizo kubwa lililopo katika miezi ya hivi karibuni kutumia chanjo ya majaribio ya ugonjwa huo inayopigiwa upatu na mashirika ya misaada na wafadhili.

Alisema chanjo iliopo sasa ndiyo iliothibitishwa kufanyakazi pekee.

Mlipuko wa ugonjwa wa ebola nchini DRC uliotokea sasa ni wa pili kwa ukubwa, ulianza Agosti mwaka jana na umeathiri majimbo mawili nchini Congo , Kivu ya kaskazini na jimbo la Ituri.

Zaidi ya watu 2,500 wameathirika na ugonjwa huo huku theluthi mbili ya idadi hiyo wakiwa wamefariki. **BBC**

# Jela miaka mitatu kwa mauaji ya mke wake

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Kigoma, imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Mwamugongo Wilaya ya Kigoma, Kunduwenda Kiza (37), kutumikia kifungo cha miaka 3 jela kwa kosa la kumuua mkewe, Zubeda Haruna, bila kukusudia.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Ilivin Mugeta, baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa la kumuua Zubeda bila kukusudia.

Jaji Mugeta alisema mahakama inatoa adhabu kali dhidi ya mashtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wanaofanya vitendo vya kikatili.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Shabani Masanja, alidai mahakamani kuwa mshtakiwa majira ya mchana katika Kijiji cha Mwamungongo alifika nyumbani kwake na kuanza kumpiga mkewe wa fimbo sehemu mbalimbali za mwili na kusababisha bandama kupasuka na kufariki dunia wakati anapelekwa Hospitali ya Mkoa (Maweni) kwa matibabu.

Aliendelea kudai kuwa baada ya mwili wa Zubeda kufanyiwa uchunguzi, ilibainika kuwa alifariki dunia kwa kupigwa sehemu mbalimbali za mwili na kusababisha bandama kupasuka.

Masanja alidai baada ya Zubeda kupigwa alimpigia simu Siwema Masudi na kumweleza kuwa amepigwa vibaya na mumewe, na kwamba amevimba mwili mzima kwa sababu ya Sh. 200 ya alizopewa mtoto wake kwa ajili ya kununuliwa mandazi.

Mwendesha Mashtaka huyo akiieleza zaidi mahakama kuwa sababu za Zubeda kupigwa na mshtakiwa ni mtoto wake Haruna Amadu kupewa fedha hizo kwa ajili ya kununua mandazi, lakini hakurudi nyumbani.

Kwamba baada mtoto huyo kutorudi nyumbani, mshtakiwa alidai kuwa hataki kumuona tena nyumbani kwa sababu siyo mtoto wake.

Baada ya maelezo hayo kutoka kwa Mwendesha Mashtaka, Jaji Mugeta alimpa mshtakiwa nafasi ya kujitetea ambapo Wakili wake, Annania Ndayase, alidai mteja wake ana familia inayomtegemea.

Aidha Wakili huyo alidai hilo ni kosa lake la kwanza, na alitenda kosa bila kukusudia, hivyo kuiomba mahakama impunguzie adhabu.

Hata hivyo, Jaji Mugeta alitupilia mbali utetezi huo, na kusema mshtakiwa atakwenda gerezani miaka mitatu.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo ya huduma za kibenki kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Wateja Wadogo na Wakati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alipotembelea kwenye banda la benki hiyo, katika Mkutano wa ALAT, unaoendelea jijini Mwanza jana. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Serikali cha NMB, Vicky Bishubo (kushoto). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Sekta ya afya yamwaga ajira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya 550 ili kujaza nafasi kwenye Hospitali za wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati.

Kwa mujibu wa Tangazo lililotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Joseph Nyamhanga, Ofisi hiyo imepata kibali cha ajira mbadala Julai 12, mwaka huu kwa ajili ya kuajiri watumishi hao.

"Hivyo, Ofisi ya Rais, Tamisemi inapenda kuwatangazia wahitimu wote wa kada za afya nchini kuwasilisha maombi ya nafasi za kazi kuanzia Julai 22, mwaka huu,"

Nafasi zilizotangazwa ni Daktari Daraja la II, Tabibu Daraja la II, Tabibu Msaidizi, Afisa Muuguzi daraja la II, Afisa Muuguzi Msaidizi daraja la II, Muuguzi daraja II, Afisa Afya Mazingira daraja la II.

Pia Afisa afya mazingira Msaidizi daraja la II, Mteknolojia daraja la II, Mteknolojia msaidizi daraja II (Maabara), Mteknolojia msaidizi (maabara), Mteknolojia daraja la II (mionzi), Mteknolojia daraja la II(dawa), Mtoa tiba kwa vitendo daraja la II na Msaidizi wa Afya (Mhudumu wa Afya).

Katibu Mkuu huyo aliwataka wahitimu hao watume maombi yao kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa kielektroniki wa ajira. tamisemi.go.tz.

"Maombi yoyote yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kuletwa moja kwa moja ofisi hayatafanyiwa kazi, mwisho wa kupokea maombi nia Agosti 5, mwaka huu saa 9:30 alasiri,"alisisitiza.

# Sheria, sera zinazokwaza biashara kupitiwa

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amesema wamejipanga kuhakikisha sheria na sera zinazokwaza biashara na uendeshaji wa viwanda nchini zinapitiwa upya ili kufanyiwa marekebisho.

Amesema hatua hiyo itasaidia kufanikisha maono ya Rais John Magufuli ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Waziri Bashungwa aliyasema hayo jana, wakati akizungumzia kuhusu maandalizi ya maadhimisho na Maonyesho ya Awamu ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema wanapitia sheria na sera zinazohusiana na masuala ya biashara ili zitakazobainika kuwa na vikwazo, zitapelekwa bungeni Septemba kufanyiwa marekebisho.

Baadhi ya sera zinazotarajiwa kufanya marekebisho ni Sera ya Kuendeleza Wajasiriamali Wadogo na Wakati (SMEs) ya mwaka 2003 ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Sera Endelevu ya Maendeleo ya Viwanda ya mwaka 1996 ambayo mwisho wake ni 2020 na Sera ya Mazao ya Kilimo.

Bashungwa alisema marekebisho hayo yatasaidia kuongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini kwa kuwa itasaidia kuongeza wawekezaji, kuwezesha viwanda vingi kujengwa hivyo kazi itakuwa ni kushiriki kwenye ushindani wa masoko mbalimbali ikiwamo SADC.

Akizungumza kuhusu maonyesho hayo yatakayofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam Agosti 5-9, 2019, alisema yatafunguliwa na Rais John Magufuli.

Aidha, yanarajiwa kufungwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, Agosti 8.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni Mazingira Wezeshi ya Biashara kwa Maendeleo Jumuishi na Endelevu ya Viwanda.

Maonyesho yatawakutanisha wazalishaji na wadau mbalimbali wa bidhaa za viwandani na wafanyabiashara kutoka nchi 16 za SADC.

"Kupitia maonyesho hayo, washiriki watapata nafasi ya kufanya majadiliano ya kibiashara na kutangaza bidhaa hususan zile zinazotengenezwa katika nchi za SADC," alisema Bashungwa.

Alisema maadhimisho na maonyesho ya Wiki ya Viwanda ya SADC ni hatua mojawapo ya kuonyesha kwa vitendo utekelezaji wa mkakati wa viwanda wa SADC (2015- 2063). Mkakati huo unaolenga kuongeza kasi ya kuimarisha ushirikiano na ushindani wa kiuchumi kwa nchi wanachama wa SADC, umejikita katika maeneo makuu matatu ambayo ni uendelezaji viwanda; ushindaji na mtangamano wa kikanda.

Tanzania imetajwa kufanya vizuri katika ufanyaji wa biashara katika SADC kwa mfano, mauzo ya Tanzania kwenda nchi za SADC kwa mwaka 2018 yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 999.34 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 877.8 mwaka 2017.

Alisema hii ni sawa na ongezeko la asilimia 12.16. Wakati huo uingizaji wa bidhaa Tanzania kutoka SADC uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 600.64 mwaka 2017 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 604.32 mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 0.61

Baadhi ya bidhaa muhimu ambazo Tanzania inauza SADC ni madini kama vile tanzanite na dhahabu; bidhaa za kilimo kama chai na kahawa; bidhaa za viwandani kama plastiki; sigara, saruji, marumaru; dawa na vifaa tiba.

"Tunawahamasisha wananchi na wadau wote kwa ujumla kuchangamkia fursa hizo ambazo tunaamini kuwa zitaongeza chachu ya kufanya vizuri zaidi katika uendelezaji viwanda nchini na pia kuimarisha urari wa biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine wanachama SADC," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


## VYETI VIMEPOTEA



115337802

**CATHERINE DAVID** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0204-0038** kilichotolewa na JANGWANI GIRLS SECONDARY SCHOOL November, 1995. Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.137/1090** kilichotolewa na MKWAWA HIGH SCHOOL May, 1998. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/150884/2019.**

## CHETI KIMEPOTEA




115337202

**Lucy Daniel Shayo** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.372/43** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1988 katika shule ya Sekondari Kirua.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: IGU/RB/1397/2019**

## CHETI KIMEPOTEA



115336802

**AULATH AHMEDI SHAKIRU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.4493-0017** kilichotolewa na **RELINI SEKONDARI** mwaka 2016.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/MBA/RB/151342/2019.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya mwanzo: Hai Kati
Usimamizi wa mirathi namba 13 mwaka 2019, Ombi la Cuthbert E Urassa kuteuliwa msimamizi wa mirath marehemu Elias Stephano Urasa.

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhuthuria kesi wakitaka mnao tarehe 05-08-2019 kabla huyu mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Imwtokea leo tarehe 22-07-2019 mwaka 2019



115336602


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No; 152/2019.

Ombi la FARIDA SHABANI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SHABANI RAMADHANI CHISI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/08/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/07/2019.



115336902


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# LILLE YAMWEKA SOKONI PEPE




**PARIS,** Ufaransa

MCHEZAJI, Nicolas Pepe ambaye anawaniwa na Manchester United atauzwa haraka iwezekanavyo kwa mujibu wa Rais wa Lille, Gerard Lopez.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu za Liverpool na United kipindi hiki cha majira ya joto, huku mashetani wekundu wakiripotiwa kutoa ofa ya pauni milioni 70.

Winga huyo wa kimataifa wa Ivory Coast alifunga mabao 23 katika mechi 41 alizoichezea timu hiyo msimu uliopita wakati Lille ikimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Pepe, ambaye ameichezea timu yake ya taifa mechi 15, pia alikuwa kwenye kikosi cha msimu cha Ligi Kuu Ufaransa.

Mshambuliaji huyo amebakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake na Lille na hivyo ofa yoyote nzuri itamfanya mchezaji huyo aondoke klabuni hapo.

Katika mahojiano na gazeti la La Viox du NordLille la Ufaransa, raia wa Lille amethibitisha kwamba mchezaji huyo anatarajia kuondoka hapo kwenye dimba la Pierre Mauroy.

"Kuhusu kuondoka na kusajili, kama mchezaji akiondoka, tutakwenda sokoni na kuangalia nani tunamhitaji.

"Kwa Nico, ni kama uhamisho wake umeshakamilika, anaweza kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto.

"Ni kweli kwamba kuna ofa kubwa kutoka kwenye klabu kubwa, hivyo nafikiri ataondoka. Hata hivyo, lolote kwenye soka linaweza kutokea."

# Tammy ahakikishiwa namba

**TOKYO,** Japan

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amemhakikishia namba kinda, Tammy Abraham kuwa atakuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi cha kwanza msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 aliukosa mchezo wa Ijumaa wa kirafiki dhidi ya Kawasaki Frontale, lakini alitarajiwa kucheza jana Jumanne dhidi ya Barcelona hapa Japan, ukiwa ni mchezo wa maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu.

Abraham alifanya mazoezi na kikosi cha Chelsea pale Saitama Jumatatu kuelekea mchezo huo wa jana Jumanne dhidi ya klabu hiyo ya La Liga.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Lampard ameonyesha kuvutiwa mno na kiwango cha Abraham, ambaye anakuwa akiwania namba sambamba na Olivier Giroud na Michy Batshuayi.

Msimu uliopita wakati akicheza ligi daraja la kwanza, Abraham alifunga mabao 25 katika mechi 37 na aliisaidia Aston Villa kurudi kucheza Ligi Kuu.

Lampard amekuwa akitumia mfumo wa 4-2-3-1 na 4-4-2 kipindi hiki cha maandalizi ya msimu mpya, ikiwa na maana kwamba Abraham atacheza sambamba na Giroud au Batshuayi.

Baada ya kucheza na Barcelona, Chelsea ina mechi nyingine tatu za kirafiki kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

Watacheza dhidi ya Reading kwenye Uwanja wa Madejski Jumapili, kabla ya kuwavaa RB Salzburg na Borussia Monchengladbach.

Mchezo wa kwanza kwa Lampard kuiongoza Chelsea kwenye Ligi Kuu utakuwa dhidi ya Manchester United kwenye uwanja wa Old Trafford.



# Nabil Fekir akamilisha usajili Real Betis



**MADRID,** Hispania

NYOTA aliyekuwa akiwaniwa na Arsenal na Liverpool, Nabil Fekir amekamilisha usajili wa kujiunga na Real Betis kutoka Lyon kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 22.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 amesaini mkataba wa miaka minne kuichezea timu hiyo na Jumatatu alitua rasmi katika viunga vya timu hiyo tayari kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ambaye alikaribia kujiunga na Liverpool kipindi cha majira ya joto kilichopita kabla ya usajili wake kushindikana dakika za mwisho, pia alikuwa kwenye rada za Arsenal.

Kulikuwa na taarifa kwamba klabu nyingi Ulaya zinawania saini yake, lakini Betis wamekamilisha usajili wake haraka.

Ofisa Mtendaji wa Lyon, Jean-Michel Aulas, alidokeza mwanzoni mwa kipindi cha majira ya joto kwamba, Fekir ataruhusiwa kuondoka kipindi hiki.

Kocha Sylvinho alimpa ruhusa Fekir kuondoka klabuni hapo wakati timu ikiwa kwenye mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya na alisafiri kwenda Hispania kwa ajili ya kukamilisha mapatano ya maslahi binafsi.

Fekir aliweka wazi kwamba hakuwa na mpango wa kusajili mkataba mpya, na mkataba wake na miamba hao wa Ligue 1 ulikuwa unamalizika Juni 2020.

# Sarri ataka Juventus imsajili Danny

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri ameitaka klabu yake kumsajili nyota wa klabu ya Tottenham Hotspurs, Danny Rose.

Sarri amewaambia waajiri wake hao wapya kuhakikisha wanamsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, kwani alikuwa akimfuatilia hata wakati akiinoa Chelsea.

Spurs ipo tayari kumuuza beki huyo wa pembeni kipindi hiki cha majira ya joto baada ya kumuuza, Kieran Trippier aliyetua Atletico Madrid kwa pauni milioni 20.

Usajili wa Trippier ulikamilika kabla ya Spurs kupaa kwenda nchini Singapore na Rose aliachwa kwenye kikosi hicho cha kocha Mauricio Pochettino wakati akisubiria hatima yake.

Sarri anahisi kwamba ana nafasi kwenye kikosi chake kwa beki wa kushoto, huku mchezaji Luca Pellegrini aliyesajiliwa hivi karibuni akitarajiwa kupelekwa kwa mkopo kule Cagliari.

Na sasa Sarri anataka kuhakikisha kwamba klabu yake inafanya jitihada za kumsajili Rose ambaye pia amekuwa akiwaniwa na Klabu ya Paris Saint-Germain na miamba wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Schalke.

Spurs inapanga kumsajili nyota wa Fulham, Ryan Sessegnon ambaye ndiye atakuwa mbadala wa Rose na tayari wameshafikia makubaliano binafsi ya kutua hapo London Kaskazini.







# RONALDO AFUTIWA SHTAKA LA UBAKAJI

**LAS VEGAS,** Marekani

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo, hatakabiliwa na shtaka lolote baada ya kutuhumiwa na madai ya unyanyasaji wa kingono, waendesha mashtaka wa Marekani wamesema.

Mwanamke mmoja, Kathryn Mayorga mwenye umri wa miaka 34, alidai kuwa mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid alimbaka katika hoteli moja mjini Las Vegas mwaka 2009.

Iliripotiwa kuwa Kathryn alikubaliana na nyota huyo kusuluhisha kesi hiyo kimya kimya nje ya mahakama mwaka 2010.

Lakini aliamua kufungua tena kesi hiyo mwaka 2018, baada ya Ronaldo kupinga madai hayo.

Katika taarifa iliyotolewa siku ya Jumatatu, waendesha mashtaka wa mjini Las Vegas walisema madai hayo hayakuweza kuthibitishwa.

"Hakuna shtaka litakalotolewa," taarifa hiyo ilisema.

Gazeti la kila wiki la Ujerumani Der Spiegel, lilichapisha taarifa kuhusu madai hayo mwaka jana.

Gazeti hilo liliandika kuwa Kathryn, alitoa ripoti katika kituo cha polisi cha Las Vegas muda mfupi baada ya tukio hilo.

# *Arsenal yakaribia kumsajili Ceballos*

**LONDON,** England

ARSENAL inakaribia kuthibitisha kumsajili kwa mkopo kiungo wa Real Madrid, Dani Ceballos.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania chini ya umri wa miaka 21 atatangazwa wakati wowote ndani ya saa 24 kutua Arsenal kwa mkopo wa muda mrefu na wamewapiku wapinzani wao wa jiji la London, Spurs kuchukua nyota huyo wa Real Madrid.

Arsenal pia imemsajili beki wa kati, William Saliba mwenye umri wa miaka 18 kutoka St Etienne, ambaye jana alitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya.

Kocha wa Arsenal, Unai Emery amesema: "Tunazungumzia uwezekano wa kumsajili tena mchezaji mmoja kwa mkopo. Tuna majina tofauti. Klabu inalifanyia kazi hilo.

"Ceballos ni mchezaji mzuri. Namjua tangu akiwa Real Betis na baadaye akatua pale Real Madrid.

"Alicheza vizuri mno katika timu ya taifa ya Hispania chini ya umri wa miaka 21, ambapo timu yake ilishinda kwenye mashindano.

"Ni mchezaji ambaye atakuwa msaada mkubwa kwetu na nina imani kubwa kwamba ataisaidia timu msimu ujao."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YAKARIBIA KUMSAJILI DYBALA

●●● Ni pale vigogo hao wa England watakapokubali kutoa dau lililotajwa na...

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus itakubali kumuuza mshambuliaji wake, Paulo Dybala kwa Manchester United katika kipindi hiki cha majira ya joto endapo mahitaji yao yatafikiwa na timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England.

**Mabingwa hao wa Serie A hawaamini kama kuna mchezaji yeyote, isipokuwa Cristiano Ronaldo, wako tayari kusikiliza ofa ambazo zitatua kwa ajili ya kuwasajili, na sasa wako tayari kwa ajili ya Dybala.**

Thamani ya mshambuliaji huyo imetajwa kuwa ni kati ya pauni milioni 70 na 90 na klabu yake haitakuwa tayari kukaa mezani ili kujadili uhamisho wa Dybala endapo hakuna ofa rasmi yoyote ambayo imewasilishwa.

Ole Gunnar Solskjaer anamhitaji zaidi mchezaji huyo ambaye pia anaichezea Timu ya Taifa ya Argentina ili kuongeza nguvu katika kikosi chake baada ya kuwapo kwa mchakato wa Romelu Lukaku na Paul Pogba kutajwa wanataka kuondoka katika klabu hiyo katika kipindi cha majira ya joto.

Kocha huyo wa United anaamini kwamba ana idara nzuri ya ulinzi ambayo itatumika kupenya katika ngome za wapinzani na endapo watafanikiwa kumnasa mchezaji huyo, atamtumia kama mchezaji wa mbele ambaye atakuwa na jukumu la ushambuliaji.

Licha ya United kukutana na ushindani katika vita ya kuwania saini ya mchezaji huyo dhidi ya Paris Saint-Germain na Inter Milan, ingawa inaelewa kuwa Dybala anatarajia kujiunga hapo baadaye.

Huku Maurizio Sarri tayari akiwa ameshaweka wazi mipango aliyokuwa nayo kwa ajili ya msimu ujao, lakini ameamua kubatilisha uamuzi wake kwa kumwondoa Dybala kwenye mipango yake ya kukitumikia kikosi hicho.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea alikuwa ameshamwondoa Dybala katika mipango yake ya ndani na nje kwenye idara ya kupachika mabao, kama alivyokutana na hali hiyo kwa Dries Mertens alipokuwa Napoli.

Na kwa wakati huo huo, Sarri hajaonekana kukata tamaa kufuatia uamuzi huo wa kumuuza Dybala uliofanywa na Juventus atafurahi kuona kama itatumia fedha itakazopata kwa ajili ya kusajili mchezaji mwingine ambaye ana kipaji katika nafasi ya kiungo mshambuliaji.

## ZISIKUPITE

### POGBA MAMBO BADO

REAL Madrid imesema kuwa mchakato wa kumwania kiungo wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (26), utatokana na hatima ya mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale (30), ambaye anatakiwa kuondoka katika klabu hiyo ya Hispania. ***(AS)***

### BALE KUIKAMUA MADRID

GARETH Bale, ambaye mshahara wake kwa wiki ni pauni 550,000, na mkataba wake na Real Madrid unatarajiwa kumalizika 2022, anataka mshahara wake wote kwa pamoja ili aweze kuondoka klabuni hapo, taarifa kutoka kwa mtu wa karibu wa nyota huyo Wales imesema. ***(Sky Sports)***

### BALE ANUKIA CHINA

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Gareth Bale, atakusanya kiasi cha chini cha bonasi ya pauni milioni 20, kama atajiunga na Ligi Kuu China. ***(Mail)***

### SPURS KUFANYA KWELI

MABOSI wa Tottenham wanatarajia kutumia kiasi kikubwa cha fedha wiki hii katika kufanikisha kunasa saini ya kiungo wa Real Betis na Argentina, Giovani lo Celso (23), pamoja na beki wa Fulham na England (U-21), Ryan Sessegnon, ambaye ana umri wa miaka 19**.** ***(Mirror)***

### SESSEGNON SOKONI

WAKATI Fulham inahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 40 na Spurs ili kumuuza Ryan Sessegnon, imeelezwa kuwa Spurs inajiamini itampata beki huyo kwa dau la pauni milioni 25 kwa sababu mkataba wa nyota huyo umebakia mwaka mmoja. ***(London Evening Standard)***

### SANE AENDELEA KUVURUGA

MANCHESTER City imekanusha madai ya Bayern Munich kuhusu klabu hiyo kufanya mazungumzo juu ya uhamisho wa winga Mrejumani Leroy Sane (23), kwa dau la thamani ya pauni milioni 100 ili kuondoka katika Ligi ya Bundesliga. ***(Mirror)***

### TOBY HAKIJAELEWEKA

TOBY Alderweireld anatarajia kuendelea kubakia Tottenham, licha ya kuwapo na tetesi za kuhusishwa kuhamia katika klabu ya Roma ambayo inaamini inakaribia kukamilisha mchakato wa kumnasa beki huyo ambaye dau lake lililotajwa kwenye mkataba ni pauni milioni 25. ***(Telegraph)***

### SARRI AMTAKA DANNY

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri anajiandaa kumsajili beki wa Tottenham, Danny Rose, ambaye ana umri wa miaka 29, katika timu yake mpya ya Juventus. ***(Mail)***

### RODRIGUEZ AKARIBIA ATLETICO

ATLETICO Madrid inajiimarisha katika mchakato wa kumwania kiungo mchezeshaji wa Real Madrid na Colombia, James Rodriguez (28), kuliko katika kumsaka kiungo wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27). ***(Marca)***

### BARCA, MESSI KUTETA

BARCELONA inajiandaa kuanza mazungumzo mapya na mshambuliaji wake na Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi (32), kwa ajili ya kuongeza mkataba mpya wa miaka minne. ***(ESPN)***

# MTIBWA SUGAR KUSAKA 'MAKALI' KWA WARUNDI

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Mtibwa Sugar inatarajia kuwavaa Eagle Noris kutoka Burundi katika mechi ya kirafiki itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi jijini Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, alisema mchezo huo in mwendelezo wa maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA.**

"Kesho (leo), tutakuwa na mchezo wa kirafiki na dhidi ya timu kutoka Burundi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao, tunaamini mchezo huo utatusaidia kiufundi kujua tulipofikia," alisema Katwila.

Kocha huyo alisema kuwa wachezaji wake wako katika hali nzuri na wamekuwa wakijituma kwenye mazoezi ya timu hiyo kila siku, isipokuwa nyota wanne ambao ni wagonjwa.

Alisema kuwa wanajiimarisha kwa kucheza mechi mbalimbali za kirafiki kwa sababu wanafahamu, msimu ujao unatarajiwa kuwa na ushindani zaidi kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu.

"Msimu ujao utakuwa mgumu kwa sababu timu zote zimejiandaa kwa muda mrefu, itakuwa ni zaidi ya ushindani ulioonekana katika msimu uliopita," alisema kocha huyo.

Aliwataka mashabiki wao kuendelea kuwapa ushirikiano msimu ujao kama ilivyokuwa msimu uliopita.

"Tumefanyia kazi upungufu ulioonekana katika msimu uliopita, pia tumesajili baadhi ya wachezaji ili kukiimarisha kikosi chetu, yaani tutaingia msimu mpya tukiwa imara zaidi, malengo yetu ni kunyakuwa ubingwa," alisema Katwila.



Wachezaji wa timu ya soka ya watoto ya Magnet, wakiwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam juzi, wakitokea nchini Sweden, ambako walikuwa wakishiriki mashindano ya Kombe la Gothia (2019). Magnet iliwakilishwa na timu 4 za watoto kuanzia umri wa miaka 11 mpaka 15, ambapo timu ya watoto chini ya miaka 11 walifanikiwa kushika nafasi ya tatu na chini ya miaka 15 waliweza kufika hatua ya 16 bora. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Waamuzi Ligi Kuu kunolewa Jumapili*

**Na Shufaa Lyimo**

ZIKIWA zimebaki siku 29 kabla ya kuanza kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Bara, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limeandaa kozi maalumu kwa waamuzi watakaochezesha ligi hiyo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi Tanzania, Salum Chama, alisema, kuwa kozi hiyo imepangwa kufanyika Jumapili kwenye ukumbi wa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Chama alisema kuwa kozi hiyo inatarajiwa kushirikisha waamuzi 48 wakiwamo wenye beji zinazotambuliwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) na wale wa Ngazi ya Daraja la Kwanza.

"Jumapili tutakuwa na kozi ya waamuzi wote watakaochezesha Ligi Kuu Tanzania Bara, maandalizi ya kozi hiyo yamekamilika na itafanyika kwenye Ukumbi wa Uwanja wa Taifa, italenga kuondoa lawama ambazo huwa wanatupiwa waamuzi," alisema Chama.

Alisema kuwa waamuzi watakuwa wanakumbushwa zaidi kutekeleza majukumu yao vema kwa kuzitekeleza kwa vitendo sheria 17 za mchezo huo.

"Msimu uliopita kulikuwa na matatizo mengi ya waamuzi, tunaahidi kuyafanyia kazi mapungufu yote ambayo yalijitokeza na kupunguza ladha ya ligi ili yasiweze kujitokeza tena," alisema mwenyekiti huyo.

Aliwataka pia wachezaji, viongozi na wadau wengine wa soka nchini kujifunza sheria hizo za soka kwa ajili ya kuacha kulalamika hata pale waamuzi wanapotafsiri vema sheria hizo.

Msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utaanza ifikapo Agosti 23, mwaka huu, wakati mechi ya Ngao ya Jamii itachezwa Agosti 17 mwaka huu kati ya mabingwa wa ligi hiyo, Simba dhidi ya wafalme wa michuano ya Kombe la FA, Azam FC.

## JKU yawatema wachezaji saba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa JKU umesema kuwa imewapeleka kwa mkopo wachezaji wake saba katika timu za Polisi Zanzibar inayoshiriki Ligi Kuu visiwani hapa na Kilimani City iliyoko Ligi Daraja la Kwanza.

Alitaja wachezaji watano waliopelekwa Polisi Zanzibar ni pamoja na Aley Suleiman, Khamis Abdallah (Teri, Edward Peter Mayunga, Ali Vui Hassan na Mbarouk Chande huku waliokwenda Kilimani City ni Is-haka Othman (Bopa) na Hassan Bamzu.

Katibu Mkuu wa JKU, Saadu Ujudi, aliliambia gazeti hili kuwa lengo la kuwatoa wachezaji hao ni kutokana na kushuka kiwango chao, na hivyo wanatakiwa wakapambane kurejea kwenye ushindani.

"Tumewatoa kwa mkopo ili wakajiimarishe, tunataka wawe na kiwango kizuri, kiwango walichokionyesha msimu uliopita hakiendani na kasi ya timu yetu, tunaamini na ni matumaini yetu huko watafanya vema," alisema Ujudi.

Ujudi alisema kuwa JKU inahitaji wachezaji wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani katika mechi zote watakazopangwa, na wachezaji hao iliyowahamisha, hawakufanya vema katika msimu uliopita.

## Z'bar yajipanga kuepuka vijeba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesema marekebisho madogo yaliyofanywa ya kanuni ya mashindano kwa klabu za madaraja ya chini yanalengo la kuendeleza na kukuza soka la vijana visiwani hapa.

Ofisa Habari wa ZFF, Adam Natepe, alisema jana kuwa marekebisho hayo yanakwenda sambamba na malengo ya kukuza soka la vijana ambapo msimu huu watahakikisha yanashirikisha wachezaji ambao wana umri mdogo.

Natepe alisema kuwa mara kadhaa klabu zimekuwa zikidanganya umri wa wachezaji na kuleta matatizo wakati wa kutengeneza kikosi cha Timu ya Taifa ya Vijana.

"Baadhi ya viongozi wa timu za vijana wanachangia katika udanganyifu wa umri, utakuta mchezaji wa timu kama Central umri wake umeshapita kucheza katika timu hiyo, lakini hawamtoi, jambo hilo linapelekea hata timu za taifa zinapochaguliwa kukosa wenye umri sahihi kulingana na umri wa mashindano husika," alisema Natepe.

Alieleza kuwa kanuni mpya inataka timu za vijana kushirikisha wachezaji wenye umri wa kuanzia miaka 13 hadi 15 na mchakato huo utakuwa unasimamiwa na vyama vya soka ngazi ya wilaya.

# Michezo

Jumatano Julai 24, 2019

Nipashe




United yakaribia kumsajili Dybala UKURASA 30

# Simba SC yaanza kwa kutoa dozi

## ● ● ● Ni salamu kwa UD Songo...

**Na Mwandishi Wetu**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Simba, Crecentius Magori, amesema kwamba timu yake haikutarajia kuanzia raundi ya kwanza ya mchujo ili kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini wanajipanga kuhakikisha wanapenya hatua hiyo.

**Simba imepangwa kuanza raundi ya kwanza ya mchujo kwa kucheza na UD do Songo ya Msumbiji katika mchezo utakaopigwa kati ya Agosti 9 na 11 na ikishinda itakutana na mshindi kati ya FC Platinum ya Zimbabwe na Nyasa Bullets ya Malawi.**

Akizungumza na kituo kimoja cha redio jana, Magori alisema awali walitarajia kwamba wangeanzia kwenye hatua ya makundi, kwa sababu Simba ilitinga robo fainali ya mashindano hayo msimu uliopita.

Lakini akasema anaamini mchezo huo dhidi ya timu hiyo kutoka Msumbjii utakuwa mgumu na kwa sasa wanajipanga kuhakikisha wanafanya vizuri.

"Najua kwamba mchezo hautakuwa rahisi, lakini kwa sasa timu ipo kwenye kambi ya mazoeni nchini Afrika Kusini na tuna imani tutaweza kufanya vizuri na hatimaye kufuzu katika hatua hiyo," alisema Magori.

Aliongeza kusema kuwa, kwa sasa kocha, Patrick Aussems anaendelea na programu yake ya mazoezi nchini Afrika Kusini tayari kwa ajili ya mchezo huo wa kwanza dhidi ya timu hiyo kutoka nchini Msumbiji.


Wakati huo huo, Simba jana ilianza vizuri mechi zake za kujipima nguvu katika kambi yake mjini Rusternburg nchini Afrika Kusini baada ya kuichapa timu ya Chuo Kikuu cha Orbit Tvet mabao 4-0 mjini.

Mabao ya Simba yalifungwa na nahodha, John Bocco aliyefunga mawili dakika ya tisa na 28, Hassan Dilunga dakika ya 23 na mshambuliaji mpya, Wilker Henrique da Silva kutoka Bragantino ya Brazil dakika ya 30.

Baada ya mchezo huo, Simba itashuka tena uwanjani leo Jumatano kucheza na Platinums Stars ya Rusternburg, na pia itakipiga na Township Rollers ya Botswana Jumamosi na Orlando Pirates ya Johannesburg Julai 30.



Mshambuliaji kinda wa Chelsea, Tammy Abraham, akimpita golikipa wa Barcelona, Ter Stegen wakati wa mchezo wa kirafiki baina ya timu hizo, uliopigwa jana mjini Tokyo nchini Japan. Chelsea ilishinda mabao 2-1. **PICHA NA MTANDAO**



# Yanga huko Morogoro utaipenda tu

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Yanga imeendelea kutakata kwenye kambi yake mjini Morogoro baada ya jana kutoa kichapo cha mabao 7-0 dhidi ya timu ya ATN, mchezo uliopigwa uwanja wa Chuo cha Biblia eneo la Bigwa.

Mabao ya Yanga yalifungwa na mshambuliaji wake mpya kutoka nchini Rwanda, Patrick Sibomana (pichani) ambaye alifunga mabao matatu 'hat-trick, huku mengine na yakifungwa na Sadney Urikhob kutoka Namibia aliyefunga mawili.

Mshambuliaji wa kimataifa wa Uganda, Juma Balinya alifunga moja na beki Lamine Moro raia wa Ghana akifunga moja.

Mechi mbili zilizotangulia Yanga ilishinda mabao 2-0 dhidi ya Moro Kids mabao ya Balinya na beki wa kulia, Paul Godfrey.

Na mechi ya kwanza Yanga ilishinda mabao 10-0, kiungo mshambuliaji, Mrisho Khalfan Ngassa akifunga mabao matatu peke yake, mengine yakifungwa na Feisal Salum, Raphael Daudi, Mapinduzi Balama, Papy Tshishimbi, Patrick Sibomana, Issa Bigirimana na Balinya.

Na yote hayo ni maandalizi ya mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga wakianza na Township Rollers ya Botswana kati ya Agosti 9 na 11 mjini Dar es Salaam kabla ya kurudiana nao mjini Gaborone kati ya Agosti 23 na 25.

Ikifanikiwa kuvuka raundi ya kwanza Yanga itakutana na mshindi kati ya Green Mamba ya Eswatini na Zesco ya Zambia.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >